

# **Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA KUMI NA SITA**

**Kikao cha Kumi na Tatu – Tarehe 25 Juni, 2009**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati ifuatayo iliwasilishwa mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:**

Randama ya Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa Mwaka Fedha 2009/2010.

**MASWALI KWA WAZIRI MKUU**

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Sifa moja aliyotuachia Baba wa Taifa katika nchi yetu ilikuwa ni kuwapokea wakimbizi na kuwahifadhi Tanzania na wakaishi kwa amani. Mwaka 2001, Tanzania kwa mara ya kwanza ilizalisha wakimbizi wasiopungua 2,000 na kwa bahati mbaya yakatokea mauaji ya raia wasiokuwa na hatia wasiopungua 23 kutokana na taarifa ya Meja Jenerali Mstaafu, Hashim Mbita, ambayo iliteuliwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali imeandaa jambo gani zuri litakalowahakikishia Watanzania kwamba hatutarudia makosa yale ambayo tuliyafanya 2001?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Hamad, swali lake zuri kama ifuatavyo. Tukio ni tukio na linapotokea unachotazama kwa kweli ni kuona kama ni jambo ambalo lina mwelekeo wa kujirudia rudia au hapana.

Lakini kama ni jambo ambalo limetokea kwa namna ambayo unaona ni *situational* kwa kweli huna sababu ya kujaribu sasa kuanza kujipanga, kutengeneza

utaratibu, kwa jambo ambalo unaona kwa *situation* ilivyokuwa ile kwa kweli ilikuwa ni jambo tu la namna yake.

Lakini mimi nadhani kubwa kwa upande wa Serikali ni kwamba mnipokuwa na jambo kama hili kikubwa ni kwamba Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, ni vizuri muda wote ikakaa ikichukua tahadhari zote zinazohitajika kuhakikisha kwamba hali ile ya ulinzi na usalama inakuwa ni imara na shwari.

Lakini sio rahisi kwa kweli kusema uanze kuitengenezea mkakati maalum, *unless* kama ni jambo linaonekana litakuwa na *trend* ya kujirudia rudia.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, sababu kubwa iliyopelekea matatizo yale ilikuwa ni uchaguzi na ndiyo hatimaye vyama vyta CCM na CUF vikakaa kwa pamoja kutafuta muafaka na kuweza kufikia muafaka na hatimaye wakimbizi wakaweza kurudi. Tume ikaundwa kuchunguza mauaji yale ambayo Serikali iliahidi kuwalipa kifuta machozi lakini mpaka leo hakijapatikana.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa matatizo yaleyale ambayo tulyazungumza na tukasema kwamba yasije yakajirudia bado yanaelekeea kujirudia; kwa mfano, hivi sasa nina orodha ya wapiga kura wasiopungua 3,500 wamenyimwa kuandikishwa kupiga kura kwasababu hawana vitambulisho vyta ukazi. Hizo ni sababu zilizopelekea kwamba kila uchaguzi unapotokea vurugu za aina hii zinatokea.

Je, Serikali inajiendaaje katika matatizo kama haya? Kwamba watu wakikoseshwa haki yao ya kuchagua na kuchaguliwa ni moja katika sababu ya msingi ya kusababisha watu walete vurugu?

Mheshimiwa Spika, Serikali inajiendaaje na hili? (*Makofit*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, bado mimi nafikiri mambo yale mawili unaweza ukayaweka tofauti, unaweza ukayatenganisha kabisa. Hoja yako hii ya pili ni jambo ambalo unaweza ukalitazama kwa namna hiyo hiyo uliviyolieleza. Kama suala lako sasa ni haki ya kunyimwa kupiga kura kwasababu ya jambo ambalo unalieleza la kutokuwa na hati ya ukaazi, sasa hili ni jambo linaweza likatazamwa na Serikali zote mbili.

Tujaribu kuona hilo tatizo likoje, msingi wake ni nini. Je, linaweza likarekebishiwa au ni hatua gani zichukuliwe ili kuweza kulimaliza. Lakini hatuwezi tukasema hiki siku zote kitakuwa ndio chanzo cha jambo kama lililotokea mwaka 2001, ndio maana nilijaribu kusema hapana ile *situation* unaweza ukaitazama pembeni na hili unalolisema nalo lina eneo lake na linaweza likatazamwa vilevile. (*Makofit*)

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Mheshimiwa Waziri Mkuu, walimu wanakaribia theluthi mbili ya watumishi wa Serikali. Walimu wamekuwa wakidai mafao yao kwa kipindi kirefu. Kwa lugha ambayo wameitumia wanasesma sasa

wamechoshwa na porojo za Profesa Maghembe. Na nchi hii imekuwa watu hawapati haki mpaka wafanye maandamano, pamoja na maandamano yao kuzuiwa na Mahakama, watakuwa tayari kufanya maandamano yasiyokuwa halali kwasababu hawajalipwa mafao yao. Lakini wanakuamini sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, uliwalih kushughulikia tatizo la aina hii katika Shirika la Reli. Wafanyakazi walipogoma ulikwenda na ukamaliza tatizo hili kwa kuahidi Serikali kuongezea mishahara yao. Unasema nini kuhusu matatizo ya mafao ya walimu?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba nimjibu Rafiki yangu Mheshimiwa Arfi, Mbunge mwenzangu kutoka Wilaya ya Mpanda kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza siyo sahihi kujaribu kutumia mfano wa wafanyakazi wa Kampuni ya Reli na walimu. Kundi la walimu wewe umefikiria ni karibu theluthi mbili, ni zaidi ya 50% ya utumishi wa umma ndani ya Serikali. Matatizo ya walimu yanajulikana na tumekuwa tunayashughulikia muda wote. Na hivi ninavyozungumza naweza nikakuhakikishia kwamba jitihada ambazo zimefanywa mpaka sasa na kiwango pengine cha matatizo yaliyobaki si makubwa ukilinganisha na huko tulikotoka. Tumeshafanya kazi kubwa sana.

Mimi nataka tu niwaombe walimu na pengine kwa maswali haya tusije sasa tukawa tunafanya kama tunataka sasa wafanye hilo unalolifkiria wanaweza wakafanya. Waiamini Serikali kwamba kazi tunayoifanya ni nzuri, tunajua wanafanya kazi nzuri sana kwa Watanzania lakini ni vizuri vilevile kukubali kwamba tatizo la walimu ni kubwa na ndio maana imetuchukua muda mrefu kidogo kujaribu kuandaa mikakati mizuri ya namna ya kumaliza tatizo hili moja kwa moja. Na mimi ninaamini tutafika hapo kwa hatua ambazo naona zinaendelea Serikalini. (*Makofi*)

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, nakushukuru kwa hatua hizo ambazo mmechukua mpaka sasa hivi. Unasema nini kuhusu madai ya Askari Polisi?

**SPIKA:** Aah! Hilo halistahili kwasababu swali la nyongeza ni lazima liambatane na swali la msingi. Mheshimiwa Salim Hemed Khamis. (*Makofi/Kicheko*)

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nimwulize swali Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mheshimiwa Waziri Mkuu, tangu ulipochaguliwa kuwa Waziri Mkuu umejizolea sifa nyingi sana kutoka kwa wananchi kutokana na namna unavyofuutilia matatizo ya wananchi na kuyapatia ufumbuzi wa haraka.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, katika Bunge la Bajeti lililopita la 2008/2009 nilikuuliza swali hapa Bungeni katika kipindi kama hiki cha maswali ya papo kwa papo kwa Waziri Mkuu kuhusu utekelezaji wa ahadi za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kutoa kifuta machozi kwa wahanga wa maandamano ya terehe 26 na 27 kule Zanzibar na Pemba. Na katika jibu lako uliniambia kwamba nikupe muda utafutilia.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, mwaka umepita sasa na waswahili wanasema muungwana ni vitendo.

Mheshimiwa Spika, je, unawapa matumaini gani wananchi hawa ambao wameanza kukata tamaa baada ya kusubiri utekelezaji wa ahadi za Serikali kwa miaka minane bila mafanikio? Ahsante.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, rafiki yangu Salim angemsikiliza Mheshimiwa Hamad, nilidhani sehemu ya jibu amenijibia moja kwa moja maana amesema sehemu kubwa walishafidiwa. Kwa hiyo, kuna hatua zilishachukuliwa. (*Makofi*)

Kwa hiyo, kama kuna maeneo ambayo yanahitaji kufanyiwa kazi zaidi pengine kwa maana ya mapunjo au kuna wengine ambao bado ni kweli hatujafanya hilo jukumu hilo linaweza likaangaliwa. Lakini mimi najua kwamba hatua fulani fulani zilikwisha kuchukuliwa.

**MHE. CHARLES N. MWERA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii, napenda nimwulize Mheshimiwa Waziri Mkuu swali. Kemikali imekuwa ni tatizo kubwa katika mgodi wa Nyamongo ambao wananchi wengi wa Kata ya Kemambo, Nyamwaga, Nyarukoba, Kibasuka, imeleta madhara makubwa sana kwa wananchi. Je, Serikali ina tamko gani kuhsu hili?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, anayosema rafiki yangu ni kweli na mimi nimeliona kwenye vyombo vya habari, nadhani jana au juzi walijaribu kuonesha tatizo kwa namna ambayo kidogo ilinitisha, ilinishtua. Lakini nilichofarijika nimeona tayari jamii imeshapata Mwanasheria ambaye anajaribu kuwasaidia kuona ni hatua gani za kicheria zinaweza zikachukuliwa. Lakini hiyo ni kwa upande wao, na sisi kama Serikali tunao wajibu vilevile wa kulifuatilia jambo hili kwa karibu sana.

Kwa hiyo, nitajaribu kumwelekeza Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi washirikiane pengine na sekta nyininge tuweze kutafuta kila mbinu pengine kwenda pale haraka tuone ukubwa wa jambo lile maana kidogo limenishtua na limenitisha kweli kweli. Tuweze kuona ni hatua zipi zinaweza zikachukuliwa kwanza kwa ajili ya hawa ambao wanaonekana wameathirika. Lakini kubwa kwa maana ya kutazama tatizo kwa upana wake. Limekuwa likishughulikiwa lakini nilipoona juzi nadhani ipo haja ya kufanya kazi ya ziada kidogo. (*Makofi*)

**MHE. CHARLES N. MWERA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa majibu hayo. Je, Waziri Mkuu utakuwa tayari kumtuma Waziri wa Afya, Waziri wa Madini na Waziri wa Mazingira kufuatana na mimi kwenda kuangalia hilo suala hapo kesho. (*Kicheko*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, nikisema kesho wakati mwingine naweza nikakudanganya. Lakini niachie nakuhakikishia tutalifanyia kazi kwa haraka sana. (*Makofi*)

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi niulize swalii moja. Mheshimiwa Waziri Mkuu, ukifuatilia michango humu Bungeni wiki iliyopita wakati wa kuchangia Bajeti na michango katika wiki hii tukichangia Bajeti ya Wizara yako, pamejitokeza maoni mbalimbali kutoka kwa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge, wakitilia mashaka utendaji kazi wa baadhi ya Mawaziri. Na kwa kuwa, Wabunge wa *CCM* tunayo imani kubwa sana na Mawaziri waliopo sasa wewe ukiwa kama kiongozi wa shughuli za Serikali Bungeni na kwa maneno mengine Msimamizi wa Mawaziri, unawaambia nini Watanzania kuhusu jambo hili linaloendelea? (*Makofi*).

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba nimjibu ndugu yangu Mheshimiwa Ndugai, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nawashukuru kama Wabunge wengi mna imani na Baraza aliloliunda Mheshimiwa Rais, mimi pia naungana mkono na ninyi kabisa. Yako mambo mawili niliyoyaona yamejitokeza katika suala hili; unaweza kusema matatu. Moja; upande mmoja ni haki ya kila Mbunge. Unajua unapokaribia kwenye Uchaguzi *pressure* inapanda *pressure* inashuka. Kwa hiyo kila Mbunge ana namna ya kujieleza na kuibana Serikali ili wananchi kule waseme naam, hapa Mzee tumeona umefanya kazi. Kwa hiyo, hilo kama Mawaziri tunalielewa na wakati mwingine halitipi shida sana kwa sababu tunajua hata ingekuwa mimi bado ningefanya hivyo hivyo kama ningekuwa *back bencher*. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, lakini la pili ni kuijuliza kama yale yanayosemwa na Waheshimiwa Wabunge, kwa kiwango gani yana ukweli ndani yake. Kwasababu kama yana ukweli ni changamoto kwa Baraza la Mawaziri ninalolisimamia. Kwa hiyo mimi ninataka nikuhakikishie tu kwamba sikutishika sana sana na kauli hizi lakini nimejiuliza sana kwamba hili ni kweli au si kweli? Je, linaweza kuwa lina ukweli ndani yake? Tufanye nini ili tuweze kufanya marekebisho yanayostahili. Mawaziri hawa ni wasikivu sana na mimi naamini kwa yale ya kweli tutayafanyia kazi. (*Makofi*).

Mheshimiwa Spika, lakini la tatu, unaposimama na kuanza kutoa madai fulani ni vizuri uwe na uhakika na unalolisema. Kwa sababu unaweza uka-*charge* kwelikweli halafu nikimruhusu Waziri naye aje kujibu, anakujibu kwa namna ambayo inaonekana wewe kumbe hukufanya kazi yako vizuri. Sasa hiyo nayo ina hatari zake hata kwa wapiga kura wako.

Kwa hiyo, mimi ninadhani ni vizuri katika jambo hili tukajipanga vizuri na si lazima vilevile ukakunja uso, umekasirika, unafoka, unajaribu kumkemea Waziri wako, tena wakati mwingine kwa lugha ambayo si nzuri sana, si ya staha. Wakati jambo unalotaka kufanya ni kupeleka tu ujumbe kwa Serikali yako kwamba huridhiki na jambo fulani, na jambo fulani na jambo fulani. Mimi naamini kama Bunge tukitumia lugha ya staha, ya kuheshimiana, ya utulivu, ujumbe utafika vizuri zaidi kuliko unapotumia ukali

ambao sio wa lazima sana. Lakini nataka niwahakikishe wote tumesikia na nimewaambia Mawaziri kwa yale yote ambayo tumeshitakiwa nayo, jipangeni tuyajibu. (*Makofi*).

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuwa ni haki ya kila Mtanzania kupata Cheti cha Kuzaliwa. Na kwa kuwa, kumekuwa na urasimu mkubwa hapa nchini hasa kwa watu wazima kupata vyeti hivi ambapo ukikitaka unachukua muda mrefu na hivyo kuweza kuwakwamisha hata wengine kuweza kupata kazi. Je, Serikali ina utaratibu gani wa kuhakikisha kwamba vyeti hivi ambavyo ni haki ya kila mtu vinapatikana maeneo yote kwa muda mfupi na kirahisi?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, bahati nzuri Mheshimiwa dada yangu Sakaya, amelieleza vizuri. Tatizo ni kubwa kwa watu wazima, hatuna tatizo kubwa sana kwa wale wanaozaliwa leo kwasababu wazazi wengi wamepata uelewa wa kutosha na wengi wanafuata taratibu zile ambazo haziwapi matatizo makubwa. Lakini kwa wale ambao ni watu wazima ni kweli mchakato wake ni mrefu kidogo. Lakini umefanywa vile kwa nia nzuri tu kwa lengo la kutaka kujiridhisha kwamba kabla hujatoa cheti basi tuwe na maelezo ya kutosha kuhusiana na ukweli juu ya jambo ambalo unataka kulisema. Kwasababu cheti kile ndio msingi wa baadaye wa kitambulisho chako, ndio msingi wa baadaye wa wewe kupata hati ya usafiri, kwahiyo kidogo kuna usumbufu.

Mheshimiwa Spika, lakini ninataka nimhakikishie dada Sakaya kwamba jambo hili tumeshalionia, tumeyaona mattatizo yako wapi na wakati mwingine hata viwango vya fedha ambavyo tumeweka kwa ajili kumwezesha mtu huyo kuweza kupata cheti nayo kidogo inaonekana kubwa katika mazingira fulani fulani. Kwa hiyo, Serikali inakubali tutalitazama, tutaliangalia, tuone kama kuna namna ya kuweza kulirekebisha pengine likaribiane na utaratibu ambao tunautoa sasa kwa watoto wadogo ili tuweze kurahisisha kazi ya kuwapa vyeti; ambayo kusema kweli ni kama haki yao. (*Makofi*)

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, nina swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa, imeonekana kwamba huduma hii inaweza kupatikana kirahisi kwa kutumia Shirika la *RITA*, lakini inaonekana inakuwa na ufanisi kipindi cha maonesho ya wiki ya Utumishi wa Umma tu kiasi ambapo mtu anaweza akachukua muda wa siku moja mpaka siku tatu anakuwa ameshafanikiwa. Je, Serikali ipo tayari kuliwezesha shirika la *RITA* liweze kufungua matawi mbalimbali maeneo yote ya Tanzania ili waweze kutoa huduma hii kirahisi?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Dada Sakaya, ni ushauri mzuri. Lakini vilevile nataka niongezee kwamba hata kwa sasa utaratibu ulivyokuwa zamani na ulivyo sasa ni tofauti kidogo. Sasa hivi tumeteremsha madaraka haya ngazi za Wilaya na kwa kweli tumekwenda sasa kwa mfumo ulivyo tunakwenda mpaka kwenye ngazi ya Tarafa na hata kwenye ngazi ya Kata na Kijiji. Mimi naamini utakapokamilika utaratibu ule utaongeza ufanisi mkubwa sana katika upatikanaji wa hati zote ambazo zinahitajika. Rai yako ni nzuri lakini nadhani vilevile ni lazima tuteremshe madaraka haya chini zaidi ambako ndio wengi tunakozaliwa na ndio wengi tuliko huko. (*Makofi*)

**MHE. DR. ALI TARAB ALI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Mheshimiwa Waziri Mkoo, tumewahamasisha wananchi kujiunga na Polisi Jamii. Je, kuna mpango madhubuti wa matibabu pindi pale wanapojeruhiwa wakati wa kutekeleza majukumu yao au kufidiwa kwa warithi wao kama wakipoteza maisha na vilevile labda kuwapa motisha pale wanapofanya vizuri? Ahsante.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu ndugu yangu Dr. Tarib Ali... (*Kicheko*)

**MHE. DR. ALI TARAB ALI:** Mheshimiwa Spika, jina langu ni Tarab.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, unajua niliogopa kulitaja kwasababu taarab juzi lilileta zogo hapa. Mimi nafikiri kwanza nikubaliane na wewe kwamba ni jambo la msingi unalolieza. Polisi Jamii ni jambo la msingi sana kwa sasa na tayari tumeshaona matunda yake ni mazuri sana katika maeneo yale ambako imetumika vizuri. Lakini Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi inajua vilevile kwamba katika utekelezaji wa majukumu haya iko hatari vilevile ya hawa wanaotusaidia wanaweza kupata matatizo ya hapa na pale, ni jambo linaloangaliwa. Hatuwezi kuahidi moja kwa moja kwamba tutakuwa na mfumo wa haraka iwezekanyo juu ya namna gani tuweze kufanya kama tulivyofanya kwa upande wa askari wa mgambo. Lakini vilevile umegusa kidogo pale mwishoni, naona uliamua uchomekee tu vizuri tu pale, nayo wakati mwingine hata namna ya kufanya, unafanya-fanyaje ili waweze kuwa na ari ya kufanya kazi zaidi?

Mheshimiwa Spika, jambo hili tulitaka zaidi liwe ni la kijamii kwa sababu tunategemea sana nguvu ya kijamii na Watanzania wanajua kwamba ulinzi kwa sehemu kubwa uko chini ya mikono yao na ni kwa manufaa yao wao vilevile. Lakini hili la kuumia nadhani ni la msingi lakini la pili tutaendelea kwanza kutoa hamasa wajue kwamba ulinzi ni jukumu letu sisi wote. Na wengi wako tayari kufanya hiyo kazi bila kinyongo chochote na bila kudai maslahi fulani fulani. Kwa hiyo, bado tutahitaji elimu kubwa lakini tunakubaliana na wewe kwa hili la kwanza hatuna budi kuliangalia.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Nataka kumuwliza Mheshimiwa Waziri Mkoo, wakati tukifunga Bunge lako la mwisho mwezi wa nne, Waziri wa *TAMISEMI* Mheshimiwa Celina Kombani na Waziri Mkoo, alielezea juu ya kusitisha zoezi la wafugaji amba walikuwa wametokea katika wilaya ya Kilosa, wilaya ya Mpanda pamoja na wilaya ya Urambo. Na akasema kwamba kuna taarifa ambayo alikuwa ameunda Tume kwa ajili ya kuangalia kilichojirini na kwamba katika Tume hiyo basi zoezi hilo lisitishwe na wale wafugaji waliokuwa wameathirika warudishiwe pesa zao na mifugo yao. Kwa taarifa ambazo tumezipata kutoka kwa wafugaji hao wa wilaya hizo, hizo pesa na mifugo wao bado hawajarudishwa.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali imechukua hatua gani na itachukua hatua gani kuhakikisha kwamba haki ya wafugaji hao inarudishwa na wale amba walichukuliwa kinyume na taratibu wamechukuliwa hatua za kisheria?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lucas Selelii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza tunakubali mimi kwa niaba ya Serikali nilitoa kauli hiyo na hata Mheshimiwa Kombani naye aliongezea nguvu. Ni kweli kabisa tulisitisha lile zoezi baada ya kuagizwa na Rais baada ya kushauriana naye, naye akakubali.

Na msingi wake mkubwa ulikuwa ni kwamba tungoje ile timu tuliyokuwa tumeiunda ikamilishe zoezi lake. Timu imeshakamilisha zoezi hilo, imeshawasilisha ripoti kwangu na hivi sasa ile ripoti tunaifanyia kazi. Matokeo ya ile taarifa yatatuwezesha sasa kuchukua hatua zote ambazo tunadhani ni stahiki.

Mheshimiwa Spika, lakini labda niongeze vilevile kwamba mimi nilipoipitia nimeona kwamba itatusaidia vilevile pengine tupate nafasi sasa ya kuzungumza kwa upana suala la wafugaji. Kwa sababu mimi bado naamini mtiririko tunaokwenda nao si suluhu kubwa na la kudumu kwa maana ya matatizo yanayojitekeza kati ya wakulima na wafugaji. Nimeona mambo mazuri sana pale na tukiyatumia vizuri tunaweza tukajipanga vizuri tukaja na mikakati mizuri na endelevu zaidi ambayo itapunguza kwa kiasi kikubwa sana matukio ambayo yanaendelea sasa. (*Makofi*)

Kwa hiyo, tutatumia matokeo ya Kamati ile na taarifa ile kujaribu kujipanga vizuri ndani ya Serikali. Lakini niliwaahidi hapa Wabunge kwamba ni dhamira yangu vilevile katika Bunge hili hili nikutane na Wabunge kutoka kwenye mikoa ya wafugaji ili tuweze kuzungumza kwa kina na nipate mawazo yao lakini vilevile tuyachanganye na mawazo baadaye ya wafugaji kutoka mikoa inayohusika tuone namna tunavyoweza kwenda mbele kutatua tatizo hili kwa mfumo ambao ni mzuri zaidi kuliko ilivyo sasa. (*Makofi*)

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana, kidogo sana. Hajafafanua juu ya zile mali, pesa na mifugo ya wahusika. Bado na hiyo bado isubiri taarifa ile ya Tume au ile ambayo ina ushahidi wa kutosha. Kwa mfano pesa ambazo zina ushahidi wa risiti na ng'ombe ambao wana ushahidi wapo; na yenyewe isubiri au wanawenza kurejeshewa?

**SPIKA:** Nadhani Mheshimiwa Selelii, ulikuwa hufuatilii vizuri, kwa sababu ile Tume ndio imekusanya yote hayo unayoyasema. Hakuna hatua yoyote inayoweza kuchukuliwa kabla ya uchambuzi wa taarifa ya Tume ambayo ndio imemfikia Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwa hiyo, nadhani hilo si sahihi. Kwa hiyo maswali kwa Waziri Mkuu yamekwisha na kwa mara nyinge tena namshukuru ..... (*Makofi*).

#### **KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu.

**SPIKA:** Kuhusu Utaratibu Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, kifungu cha 68. Wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu, anamjibu Mheshimiwa Salim, alisema kwamba hili la kifuta machozi kama nilivyosema mimi limeshashughulikiwa. Nilichosema mimi kimeshughulikiwa ni suala la Wakimbizi walioko kule, suala la kifuta machozi ya wale walioathirika mpaka leo bado halijashughulikiwa. Nilitaka ili rekodi iwe *proper*, pengine hakunisikia vizuri tu Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**SPIKA:** Kwa maana ya kusahihisha kile ulichosema ama kukiweka sawa ni sawa tu. Natumaini na wawakilishi nao watauliza kule kwenye Baraza la Wawakilishi kwa sababu mambo haya yanapoletwa hapa kidogo hata sijui Serikali ya Muungano na, aah! Ni vizuri tu yaulizwe pande zote na ndio maana Mheshimiwa Waziri Mkuu amesema Serikali zote mbili zitakaa pamoja ili kuweza kuondoa utata katika suala hili na kutenda haki tu. Kwasababu ni kawaida ya Serikali zetu kujitahidi kusikiliza na kutenda haki na kurekebisha pale palipo na matatizo.

Nilikuwa nimesimama tu kumshukuru tena Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa jinsi ambavyo anadhihirika kabisa kwamba anayajibu maswali haya vizuri sana. Waheshimiwa Wabunge, ni vizuri ukikaa tu huku unaangalia, lakini ungewekwa pale na hujui swali linaweza kuwa linahusu wafugaji, fidia kwa wahanga wa Zanzibar, kwa kweli ni kazi ngumu sana.

Mimi nadhani tuna kila haki ya kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu. Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, tunakuombea afya njema na maisha marefu, unatuongoza vizuri. (*Makofi/Kicheko*).

Katibu, kwa hatua inayofuata tuendelee.

### **MASWALI NA MAJIBU**

Na. 104

#### **Ubadhirifu wa Mali za Umma Katika Halmashauri Nchini**

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI** aliuliza:-

Kwa kuwa, ubadhirifu wa mali za Serikali ni kosa bila kujali kosa hilo limefanywa na kiongozi au Mwananchi wa kawaida; na kwa kuwa baadhi ya viongozi wa Halmashauri hushindwa kuweka bayana makosa hayo kwa wahalifu hazina:-

- (a) Je, Serikali inasemaje kuhusu hili?
- (b) Je, Halmashauri inaruhusiwa kuzima uhalifu wa aina yoyote?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, kwanza naomba niungane na wewe kwamba na mimi napenda kuungana na wewe kusema kwamba nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa namna anavyojibu maswali vizuri kwa ufasaha hapa Bungeni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwanawetu Said Sarafi, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Spika, ubadhilifu wa mali za umma ni kosa bila kujali kosa hilo limefanywa na kiongozi au mwananchi wa kawaida. Fedha za Serikali za Mitaa zinasimamiwa na sheria ya mwaka 1982 na sheria ya makosa ya jinai ambapo ikibainika mtumishi anakosa la kufanya ubadhilifu atachukuliwa hatua za kinidhamu.

Mheshimiwa Spika, halmashauri kama mamlaka ya kinidhamu zimekuwa zikuchukua hatua mfano katika kipindi cha mwaka 2006 hadi mwaka 2008 watumishi wapatao 625 walichukuliwa hatua ya kinidhamu kutokana na makosa mbalimbali yakiwemo ya ubadhilifu. Kwa upande mwingine Halmashauri zimekuwa zikiwafikisha mahakamani watumishi au watu waliofanya ubadhilifu wa mali za umma kwa mujibu wa sheria ya makosa ya jinai. Mfano katika halmashauri za Lindi, Hanang na Ngorongoro walichukua hatua kama hizo ninazozungumza.

Aidha, sheria ya TAKUKURU nayo hutumika kutumia kushughulikia ubadhilifu wa mali za umma chini ya makosa ya uhujumu wa ucuhami.

Mheshimiwa Hakuna mtu au taasisi yoyote nchini inayoruhusiwa na sheria zilizotajwa hapo juu kuzimauarifu wa aina yoyote, suala la msingi ni ushahidi wa kutosha kumtia mtuhumiwa hatiani kwani kwa upande mwingine ni lazima kuhakikisha kuwa wananchi wetu hawaonei wala kukandamizwa kwa kutumia sheria hizo. Naomba nitoe rai kwa wananchi kwamba wasisite kutoa taarifa za ubadhirifu kwa kuanzia ngazi ya Halmashauri, wilaya mikoa na hata katika ofisi yangu kwani wakati wote uongozi katika ofisi hizo upo tayari kuzifanya kazi taarifa hizo.

Mheshimiwa Spika, pale inapoonekana halmashauri imezima uarifu wa aina yoyote naomba ijulikane wazi kwamba ofisi ya mkuu wa mkoa inao uwezo wa kuingilia kati na kushauri kwa mujibu wa sheria za Serikali za mitaa namba tisa ya mwaka 1982 na kama Halmashauri itakaidi badi mkuu wa mkoa atatoa taarifa kwa mamlaka husika ili ifanyiwe kazi.

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI:** Mheshimiwa Spika, asante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza, kwa kuwa uzimaji na ubadhirifu wa mali za umma katika wilaya ya Kilwa imekuwa ni kitu cha kawaida na hasa pale yanapofanywa na wenyewe au viongozi wa chama tawala, na kwa kuwa kampuni ya Nongwa imefanya ubadhirifu huo na ushahidi tunao na tumepeleka sehemu husika sasa yapata kama miaka miwili hakuna jibu. Na kwa kuwa, Mheshimiwa Naibu Waziri alipokuwa anazungumza

hana kwamba ukiwa na ushahidi basi upeleke kwake, na tumeshafikisha hili, anasemaje ubadhirifu huu uliofanywa na diwani ambaye mwenye kampuni hiyo hadi sasa hajachukuliwa hatua yoyote?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, wakati anauliza swali la nyongeza nilishindwa kupata *connection* ile anapozungumzia chama cha Mapinduzi katika suala hili nilishindwa kuelewa kwamba anaunganishaje unganishaje hapo. Lakini mimi nataka nisema hapa nasema taratibu zimewekwa vizuri sana akitoka mtu anaitwa *controller and auditor general* mkaguzi wa hesabu wa mahesabu ya Serikali akaenda Kilwa akafika pale akakuta hela zimetumika vibaya au kuna fraud imefanyika pale.

Kazi yake ya kwanza kwa kutumia sheria namba tisa ya mwaka 1982 ni kutoa taarifa hiyo kwa mkuu wa mkoa na kumwarifu kuwa kuna ubadhirifu umetokea pale ndivyo inavyosema sheria hiyo akimaliza pale, mkuu wa mkoa anawasiliana na Mwenyekiti wa Halmashauri inayohusika na Mwenyekiti yule anachukua hatua hapo hapo kuzungumza na Kamati iliyoko katika Halmashauri ya mipango na fedha uiarifu kuhusu ubadhirifu umetokea pale Kamati ile ikikutana ikikaa (sauti hii mzee wangu ni ya kwangu ya kawaida tu sio kwamba nataka kufoka, nataka tu kueleza wenyewe naomba uniwie radhi). (*Makofi/Kicheko*)

Kamati ikishapokea hiyo inakwenda inaketi kwa niaba ya Halmashauri na kazi ya kwanza ni kumshauri Katibu Mkuu wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kumwambia kwamba wao wanafikiri hatua gani zichukuliwe pale. Kwa hiyo kama kuna diwani amefanya hivi amesema hapa kuna kampuni inaitwa Nongwa, huo ndiyo utaratibu unaotakiwa, na kama atasema kwamba kuna barua zimeshakuja na kuna ushahidi umeletwa hapa nataka niithibitishie nyumba hii nakuthibitishia kwamba tutachukua hatua na tutatoa taarifa kuhusu jambo hili analolizungumza hapa. (*Makofi*)

**MHE. DR. WILLIBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza, kwa kuwa katika kesi nyingi alizozitaja Mheshimiwa Waziri kesi nyingi tumezipoteza na sababu kubwa zilizonekana za kupoteza kesi hizo ni kwa nyaraka muhimu kutowasilishwa mahakama au kwa viongozi husika kutokuhudhuria kwenye kesi hizo na hivyo kesi kufutwa.

Je, Serikali iko tayari kuwakemea wale wote na kuwachukulia hatua wale ambao wanafanya hujuma za kutopeleka nyaraka hizo na kutokwenda mahakama inavyotakiwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwanza na katiba ya nchi na labda hii nikumbushe hapa kama watu hawakumbuki na wananchi wakumbuke hili. Mwananchi yeoyote ile katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa sheria za nchi yetu akikuta uhalifu umefanyika mahali popote sheria inamruhusu kumtia hatiani yule ambaye amehusika na ile hatia pale. Na kwa taratibu za nchi yetu kama umelijua kosa limefanyika na ukalinyamazia hilo pia ni kosa sasa akitokea mtu ana nyaraka ambazo

zinathibitisha jambo lile akizificha ili kuzuia jambo lile lisijulikane, anafanya makosa makubwa na kwa kweli Serikali inatakiwa imchukulie hatua mara moja. (*Makofi*)

Na. 105

### **Mpango wa Upandaji Miti Nchini**

#### **MHE. MWANAKHAMIS KASSIM SAID aliuliza:-**

Kwa kuwa, nchi yetu ni kubwa na kuna tofauti ya hali ya heswa kwa mikoa yake. Na kwa kuwa upo utaratibu maalum wa kupanda miti kila mwaka kwa nchi nzima ambapo mikoa mbalimbali hupata mvua za vuli na masika kwa viwango tofauti:-

- (a) Je, kwanini tutangaze upandaji miti kwa nchi nzima wakati tofauti hizo zinajulikana?
- (b) Je, kwanini usiwepo utaratibu wa kuweka kalenda ya kila mwaka inayotofautiana upandaji wa miti kulingana na hali ya hewa na upatikanaji wa mvua katika nchi yetu?
- (c) Je, kwanini kalenda hiyo isionyeshe upandaji wa mara mbili kwa mwaka au ikasisitiza upandaji kulingana na upatikanaji wa mvua?

#### **NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said, Mbunge wa Viti Maalum swalii lake lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tunavyofahamu, tarehe mosi Januari kila mwaka ni siku ya Taifa ya kupanda miti. Chimbuko la kupanda miti kila Januari mosi lilikuwa ni kuikaribisha milenia, na Serikali iliwhamasisha wananchi kupanga miti milioni mia moja mwaka 2000.

Kutokana na tukio hilo la milenia ofisi ya Waziri Mkuu ilitoa waraka wa Serikali namba 1 wa mwaka 2000 wa kuifanya kila Januari mosi kuwa siku ya Taifa ya kupanda miti. Kwa mara ya kwanza maadhisho ya siku ya Taifa ya kupanda miti yalifanyika kitaifa mwaka 2001 katika eneo la Jangwani Mkoani Dar es Salaam. Mwaka 2002 iliadhimishwa kitaifa mkoa wa Pwani katika eneo la Tumbi Kibaha. Siku hiyo iliadhimishwa tena mkoani Dar es Salaam mwaka 2003 katika shule za Majimatitu iliyoko Mbagala Charambe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa siyo mikoa yote inayopata mvua mwezi Januari, tangu mwaka 2004 maadhisho ya siku ya taifa ya kupanda miti yanaandaliiwa na kuratibiwa katika ngazi za mikoa. Hivyo kila mkoa umepewa fursa ya kupanga siku yake ya kupanda miti kulingana na majira ya mvua.

Kwa hiyo, tarehe mosi Januari, kama siku ya taifa ya kupanda miti, ni siku ya kuzindua maadhisho kitaifa. Katika siku hii wananchi wanaoishi katika mikoa inayopata mvua mwezi Januari wanahamasishwa kupanda miti kwa wingi.

Aidha, katika mikoa ambayo haipati mvua mwezi Januari wananchi wanapanda miti michache kama ishara ya kuzindua maadhisho haya. Miti mingine inapandwa wakati muafaka kufuatana na majira ya mvua.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, uzinduzi wa mwaka 2009 wa siku ya Taifa ya kupanda miti ulifanyika mkoani Dar es Salaam wakati Mheshimiwa Rais alipokuwa Mgeni Rasmi. Hata hivyo, Dar es Salaam, kama mkoa, unayo siku yake ya kupanda miti kwa wingi ambayo ni tarehe 10 Aprili kila mwaka. Kwa hiyo, hata mikoa ambayo inapata mvua mara mbili kwa mwaka inayo fursa ya kuamua kupanda miti katika kila msimu wa mvua.

**MHE. ALHAJI MANJU S. O. MSAMBYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza, zoezi la kupanda miti ni zoezi nzuri na la faida kwa taifa letu. Kwa bahati nzuri Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwa mara ya kwanza upandaji miti ulizinduliwa Jangwani Dar es Salaam lakini pale ambapo uzinduzi ulifanyika hapaonekani kama kuna dalili kwamba zoezi hili lilifanyika. Je, Mheshimiwa Waziri anaweza akalieleza Bunge hili na Taifa na kwa ujumla ni miti mingapi au ubora gani umepatikana katika zoezi la kupanda miti katika Taifa la Tanzania?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri sidhani ni lazima useme idadi ya miti sijui lakini unaweza tu kuupima tu ufanisi nadhani.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, survival rate ya miti inatokana na eneo ambako imepandwa hasa kutokana na mazingira ya mvua. Lakini nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tokea mwaka 2000 tulipozindua zoezi hili miti zaidi ya bilioni 1, na milioni 200 imepandwa sehemu mbalimbali za nchi na miti mingi katika eneo hilo la Jangwani hivi sasa ipo ingawa kwa sababu ilipandwa michache kwa ajili ya kuadhimisha sehemu ambako kumepandwa miti mingi sana kwa mfano mkoa wa Tanga umepanda zaidi ya miti milioni 300 katika kipindi hiki. Kwa hivyo miti imepandwa mingi, *survival rate* imetofautiana kutokana na mazingira ya mvua, lakini kwa wastani ni zaidi ya asilimia 80 miti inayopandwa ina survival.

**MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuweza kunipa nafasi kwa kweli ni muda mrefu bila kuuliza swali lolote hapa Bungeni.

Kwa kuwa wananchi wa barabara ya Mwandiga mpaka Manyovu, wamepanda miti, na kwa kuwa utathimini unaopitishwa sasa hivi wanaambiwa kuwa ile miti haiwezi ikapewa fidia. Je, hawaoni kuwa Serikali sasa hivi inawanyanyasa wananchi hawa?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, miti kwa kawaida inakuwa inamilikiwa na mtu na pale ambapo tunahitaji kuondoa miti ile kwa ajili ya matumizi ya jamii kama kuitisha barabara hakika miti hiyo inahitaji kuvunwa kwa ajili ya matumizi. Kwa hivyo kwa sababu miti inathamani, inaweza kutumika kwa mbao kwa kuni au kwa shughuli yoyote nyingine. Kwa hivyo tunafikiri pengine kuivuna miti hiyo na kuiondoa ili kutoa nafasi kwa barabara kupita ni jambo la busara na kwa maana hiyo si lazima kutoa fidia kana kwamba mwenye nayo hawezi akaruhusiwa kuitumia.

Na. 105

**Kujenga Chuo Kikuu cha Kilimo na Utafiti wa  
Wavuvi Kigoma**

**MHE. PETER J. SERUKAMBA-(K.n.y.) MHE. DANIEL  
NSANZUGWANKO)** aliuliza:-

Kwa kuwa, mkoa wa Kigoma umejaliwa kuwa na hali ya hewa nzuri, udongo wa rutuba na mito mingi:-

(a) Je, ni kwanini Serikali isifikirie kuanzisha Chuo Kikuu cha Kilimo na Utafiti wa Uvuvi mkoani Kigoma na kwamba ardhi ya kutosha ipo?

(b) Je, kwanini Serikali isikope kutoka taasisi za kimataifa, benki ya Dunia, Jumuiya ya Ulaya na nchi marafiki ili kutekeleza azma hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE.  
GAUDENTIA M. KABAKA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Daniel Nsanzugwako, Mbunge wa Kasulu Mashariki, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua hali nzuri ya hewa, udongo wa rutuba, mito mingi na neema za ziwa Tanganyika katika mkoa wa Kigoma. Hivyo nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa ubunifu wake wa mapendelezo mazuri yaliyoko kwenye swalii lake. Aidha, tutaendelea kujadili suala hili na uongozi wa mkoa wa Kigoma, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika pamoja na Wizara ya Mifugo na Maendeleo ya Uvuvi ili kuona namna bora ya kutumia fursa nzuri zilizopo mkoani Kigoma.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa hivi sasa, Serikali imeweka nguvu kubwa katika kujenga kwa nia ya kukamilisha mradi mpya wa chuo kikuu cha Dodoma na kujenga kampasi mpya ya chuo kikuu cha tiba na sayansi za afya Muhimibili (MUHAS) katika eneo la Mlonganzira, Dar es Salaam. Kwa sababu hiyo, hivi sasa haina uwezo wa kukopa

fedha kwa ajili ya ujenzi wa chuo kikuu cha kilimo mkoani Kigoma. Hata hivyo, ni vizuri uongozi wa mkoa ukaanza matayarisho ya awali ya chuo kikuu Kigoma kwa kutenga eneo kwa ajioi ya kuanzishwa chuo hicho hapo Serikali itakapokuwa na uwezo wa kufanya hivyo.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nilikuwa na maswali mawili ya nyongeza, swalii la kwanza wilayani Kasulu kuna chuo cha Mubondo ambacho kimekuwa chuo cha kilimo kwa muda mrefu sana, ambacho sasa kimebadilishwa kuwa shule ya sekondari. Katika hali ya sasa ambayo tunasema kilimo kwanza.

Je, Serikali haioni kuwa ni busara sasa ili iwasiliana na Halmashauri ili tuibadilishe ile shule ya sekondari ijengwe kwingine kile chuo cha Mubondo sasa kiweze kufanya hii kazi ambayo sasa tunaihitaji kwa maana ya hili suala la kilimo kwanza.

Ni kweli kwamba Serikali inafanya kazi ya chuo cha Dodoma, na chuo cha Muhibibili, lakini kupanga ni kuchagua ukiangalia sasa mahitaji ya sasa kilimo kinakuwa ni agenda namba one, kwanini sasa Serikali isianze kufikiria angalau kuanza kufikiria kwa ajili ya kujenga hicho chuo katika mkoa wa Kigoma?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA M. KABAKA):** Mheshimiwa Spika, nakubaliana naye kabisa kwamba kupanga ni kuchagua na ndiyo maana tumelema tumelema na tumechagua kwamba kwanza tujenge chuo kikubwa cha Dodoma, kwa sababu pamoja na fani nyingine pia fani za sayansi *ICT* na mambo mengine ya ardhi yatafundishwa katika chuo kile na ni mradi mkubwa sana. Na pia kubadilisha hivi vyuo vidogo kuweka chuo kikuu kwa kweli Serikali sasa hivi isingependa kubadilisha vyuo vyote vidogo na kufanya chuo kikuu lakini tutakapokuwa tumejipanga vizuri tumelema kwamba kwa kweli tunaomba mkoa wa Kigoma utenye ardhi, kama wana nia thabiti kwamba baadaye tuwe na chuo kikubwa kinachohusu masuala ya kilimo katika mkoa huo.

Na. 107

**Ahadi ya Kuwapatia Wananchi wa Lamadi  
Maji Safi na Salama**

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI** aliuliza:-

Kwa kuwa, mji mdogo wa Lamadi umepanuka kwa kasi na una idadi kubwa ya Wakazi na kwamba haujapata kuwa na chanzo chochote cha maji safi na salama tangu kuanzishwa; na kwa kuwa, mwezi Mei, 2007 Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati akihutubia mukutano wa hadhara aliahidi kuwa mji wa Lamadi utapatiwa maji safi na salama:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais kwa wananchi wa Lamadi?

(b) Kwa kuwa, pamekuwepo na ahadi kila mara za kusaidia kupatikana maji katika mji huo na kwamba hakuna utekelezaji wake. je, Serikali haioni kuwa, ipo haja ya kufanya mkakati wa dharura ili kuwanusuru wananchi hawa na shida ya maji haraka? (*Makofii*)

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swal la Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni, Mbunge wa Busega, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua tatizo la upatikanaji wa maji safi na salama katika kijiji cha Lamadi. Tatizo hili limeongezeka zaidi baada ya pampu mbili za visima vifupi kuibowi.

Katika kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kuwapatia maji safi na salama wananchi wa kijiji cha Lamadi, Serikali kwa kushirikiana na Halmashauri ya wilaya ya Magu ililingiza kijiji cha Lamadi katika vijiji 10 vilivyopo kwenye mpango wa maji na usafi wa mazingira vijiji.

Napenda sasa kumwarifu Mheshimiwa Mbunge wa wananchi wa Jimbo la Busega kwa ujumla kuwa, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Magu imekwishaajiri Mhandisi Mshauri ambaye ni *COWI Consulting Engineers* ambaye tayari ameshaanza kazi ya kusanifu miradi ya maji ya vijiji 10 pamoja na Lamadi. vijiji vingine vitakavyonufaika na mradi huo ni Lugeye, Kigangama, Nkungu, Nsola, Bubinza, Nyanguge, Yichobela, Lubugu, Misambo, Kisesa B, Manala na Nyangili.

(b) Mheshimiwa Spika, wakati mradi wa maji wa vijiji 10 unaendelea kutekekelzwa, Wizara yangu imeamua kuchukua hatua za haraka ili kurejesha upatikanaji wa maji safi katika kijiji cha Lamadi. Tarehe 15 – 16 Juni, 2009 Wizara yangu iliteua kikosi kazi cha wahandisi wa maji kuandaa mkakati wa dharura wa kuwapa maji wakazi wa vijiji vya Lamadi na Lukungu ambao ni kweli wana matatizo makubwa ya maji kutokana na kuongezeka kwa watu na shughuli nyingi za biashara.

Napenda pia kumwarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba Wahandisi wa Wizara yangu kwa kushirikiana na Serikali ya Kijiji wamebaini chanzo kipy cha maji katika Ziwa Victoria sehemu ya Kungoma katika kitongoji cha Itongo. Hatua inayofuata ni kwamba katika mwaka 2009/2010, Wizara yangu itafunga pampu ya kuzamisha majini *submersible pump* na kujenga tanki la maji na bomba za kusambaza maji. Miundombinu hii ikikamilika itawawezesha wananchi wa Lamadi kupata maji kwa haraka chini ya mkakati wa dharura.

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yenye kutia moyo na faraja kwa wananchi wa Busega.

Sambamba na pongezi hizi napenda vilevile nimpongeze Waziri mwenye dhamana hii kwa sababu ni moja ya Mawaziri ambao wamethubutu kutekeleza ahadi ya Rais kama ambavyo ilivyoahidiwa mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili madogo ya nyongeza, kwa kuwa hali ya maji katika mji wa Lamadi Kitete kutokana na kukosa huduma ya maji kwa muda mrefu na kwamba wananchi wamekuwa wakihangaika kwa muda mrefu sana. Sasa ningependa kufahamu kwamba mkakati wa dharura huu sijui ni kiasi gani cha pesa kimetengwa ili kuweza kuboresha mradi wa dharura.

Lakini pili mimi naomba nisema kwamba Mheshimiwa Waziri Prof. Mwandsosya amethibitisha uthubutu wake kwa sababu hali iliyokuwa Lamadi ilivyosasa hivi si nzuri sana na kwamba ameamua kuunda kikosi kazi baada ya kuwa tumewasiliana, na ndani ya kikosi kazi, je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana na mimi kwamba na ye ye atakuwa sehemu ya kikosi kazi na atakubali mwaliko kuja ili kuiona Lamadi na hali ilivyo ya maji?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kama nilivyosema katika majibu ya msingi kwamba katika mwaka huu 2009/2010 kazi hizo za kurejesha huduma za maji zitafanyika.

Naomba tu niseme si rahisi sasa kumwambia kwamba tunatumia kiasi fulani naomba aamini kwamba pesa zitatengwa katika mwaka 2009/2010 na wakati baada ya bajeti yetu kusomwa nitakuwa tayari kabisa kumwambia kwamba sasa kazi yako inatarajia kutumia kiasi fulani pamoja na kwamba pesa zinaweza zikabadilika zikaongezeka au zikapungua.

Lakini kwa ajili tu angalau ya kumpa picha kwa sababu naona anapenda kufuatilia sana suala hili miradi ya namna hii kwa uzoefu wangu mara nyingi inatumia kati ya milioni 150 na milioni 200 kwa ajili ya dharura. Kwa hiyo naomba aichukue tu kwamba hayo ni makisio lakini baada ya Bajeti kusomwa atajua kwa hakika kwamba ni kiasi gani kimetengwa.

Kuhusu ombi lake au mwaliko wake wa kwenda kutembelea kuwa kikosi kazi, naomba niseme kwamba kikosi kazi mara nyingi tunatuma wataalam, wahandisi, wanakwenda na sisi wenyewe kama Mawaziri tunakwenda kujiridhisha kuona kwamba kazi zinaendelea kufanywa kama tulivyoagiza.

Lakini nimthibitishie kabisa kwamba kama Waziri wangu hatakwenda na mimi mwenyewe nitakwenda kwa Dr. Chegeni ili nione kazi yake inavyofanyika, Dr. Chegeni, namheshimu sana ni *sanzi* wangu (wameoleana).

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, mwaliko wa kwenda kuwa katika kikosi kazi ulielekezwa kwangu moja kwa moja nadhani Mheshimiwa Mbunge angependa kunisikia vilevile pamoja na wananchi wa Lamadi.

Naomba kumhakikishia Mheshimiwa Dr. Chegeni kwamba mimi ni rafiki wa jimbo lake anakumbuka nilishafika Badugu, nilishafika Kaloleli, namhakikishia kwamba nitafika Lamadi ili kuhakikisha kwamba tunatekeleza mradi huu ahsante.

**MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swalii moja la nyongeza kwa kuwa matatizo ya maji katika nchi hii ni makubwa kwa kiasi fulani kwamba wananchi wana shida ya maji lakini programu za maji katika wilaya zetu, Wizara ya Maji inakamilisha miradi na inatakiwa na Wizara nyingine kama ya Nishati na Madini ili iweke umeme na hatimaye wananchi wapate maji.

Je, kuna ushirikiano gani kati ya Wizara ya Maji na Wizara ya Nishati na Madini kuhakikisha kwamba miradi ya maji ambayo Wizara ya Maji imekamilisha na sasa Wizara ya Nishati na Madini iweze kuleta miundombinu ya umeme ili tuweze kuwanufaisha wananchi kwa maji?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, Serikali ni moja Wizara zote zinafanya kazi kwa ajili ya watu wale, tunachokifanya ni hicho ni kwamba tunaangalia Wizara hii inatoa huduma gani.

Lakini kwa upande wa maji naomba nimhakikishie kwamba pale ambapo labda umeme haujafika katika eneo fulani basi na sisi tunaangalia kwamba katika kutengeneza miradi hiyo basi tunaweka nishati nyingine kama ya mafuta, kama ya upepo, ili iweze kutangulia wakati ile miradi mingine nayo inatekelezwa. Lakini nataka nimhakikishie kwamba yote Serikali inatazama mradi wetu kwa pamoja na tunashirikiana wakati tunapanga.

**MHE. JUMA S. KABOYONGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swalii moja la nyongeza, niseme kwamba tatizo la maji linafanana sana na tatizo la mjini Tabora, lakini nikiri kwamba Serikali sasa hivi kwa kushirikiana na Serikali ya Uswisi, ina mradi mkubwa wa kurekebisha tatizo la maji mjini Tabora. Tatizo ni *speed* mradi unasuasua sana mwaka wa tatu.

Je, Serikali inatoa kauli gani juu ya kucheleweshwa wa utekelezaji wa mradi wa maji mjini Tabora?

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Kaboyonga kama ifuatavyo, kuhusu Tabora, tuna mkakati ufuatao ambao tunautekeleza, kwanza nikupitia msaada wa washirika wetu shirika la maendeleo la wa *SWISECO* ambao tumechelewa kidogo kwa sababu ya kuitafiliana kimkakati hapo mwanzo kwamba walitaka tuanzishe mfumo wa kuwa na

shirika binafsi pale liweze likauzia maji shirika letu la maji safi na maji taka la Tabora, tuliona tusiweke Tabora kama ni chambo au ni kitu cha kuanzia zoezi.

Kwa hiyo, tuliiitirafiana lakini sasa tunakubali kwa hiyo *SECO* itaendelea kutoa fedha kwa ajili ya Tabora kama ilivyotoa kwa ajili ya Dodoma. (*Makofit*)

La pili, ni mpango wa maendeleo wa Sekta ya Maji ambao tumeajiri Mhandisi Mshauri wa *Cluster* ya Tabora na *Cluster* ya Tabora inahusu Miji ifuatayo; Tabora, Urambo, Sikonge, Nzega, Igunga na Isikizye. Maana yake ni nini? Maana yake ni kwamba huyu Mhandisi atafanya kazi ya upanuzi wa mfumo wa maji Tabora pamoja na miji mingine yote hii niliyoitaja kuhakikisha kwamba maji yanapatikana kuanzia sasa mpaka mwaka 2020. Ni mradi mkubwa ambao tayari una fedha kwa hiyo tutautekeleza.

Lakini tatu, katika mkakati huo tutahakikisha kwamba utendaji wa Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Tabora unaboreshw. (*Makofit*)

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Waziri kwa jibu zuri sana, swali la mwisho kwa Wizara hiyohiyo litaulizwa na Mheshimiwa Juma Said Omar wa Mtambwe. (*Kicheko*)

Na. 108

### **Wizi wa Vifaa vya Miradi ya Maji Nchini**

**MHE. JUMA SAID OMAR** aliuliza:-

Kwa kuwa, kumejitokeza wizi wa vifaa katika miradi mbalimbali ya maji hapa nchini jambo linalokwamisha kufikia malengo yaliyokusudiwa na hivyo kuleta kero kwa wananchi;

Je, Serikali ina mikakati gani ya kupambana na tatizo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Juma Said Omar, Mbunge wa Mtambwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, dhamira ya Wizara yangu ni kuhakikisha raslimali za maji zinasimamiwa, zinaendelezwa na kutumika kwa njia endelevu na shirikishi ili kukidhi mahitaji ya Sekta mbalimbali kwa kusimamia raslimali za maji, kuboresha miundombinu ya usambazaji maji safi na uondoaji wa majitaka na kuboresha miundombinu ya umwagiliaji. Ili kufikia malengo hayo, Serikali inaendelea kutekeleza *Program* ya Kuendeleza Sekta ya Maji inayokadiriwa kugharimu *USD* milioni 940 na *program* ya kuendeleza Sekta ya Kilimo (Umwagiliaji) ambayo inatarajiwa kugharimu Trilioni 1.967.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba pamoja na juhudii kubwa zinazoendelea kufanywa na Serikali, viwo vikwazo kadhaa vinavyojitokeza

kurudisha nyuma maendeleo ya maji hususani uharibifu wa miundombinu ya maji na wizi wa vifaa vyake unaofanywa na watu wachache kutokana na kukithiri kwa biashara ya chuma chakavu. Uuzaji wa chuma chakavu ni biashara inayofanyika kwa kasi hivi sasa nchini kote.

Biashara hii imeleta athari kubwa katika maendeleo ya Sekta ya maji ambapo wauzaji wamefikia hatua ya kuharibu mitandao ya mabomba ya usambazaji majisafi, pampu, dira, viungio vyake na mifuniko ya *Chamber* za majitaka na kuuza kama chuma chakavu.

Mheshimiwa Spika, athari zilizopatikana kutokana na biashara hii mpaka sasa ni pamoja na:-

1. Kukosekana kwa huduma za majisafi kwa wananchi katika maeneo yaliyoathirika hivyo kusababisha magonjwa ya mlipuko.
2. Kuharibiwa kwa mifumo ya uondoaji majitaka na uchafuzi wa mazingira.
3. Upotevu wa fedha kwa kuwa Serikali, Taasisi na watu binafsi hulazimika kununua vifaa viliyoibiwa ili kurejesha huduma kwa wananchi, na hivyo kuzorota kwa utoaji wa huduma pale fedha hizi zinapotumika kwa matumizi yasiyopangwa.

Mheshimiwa Spika, hatua zinazoendela kuchukuliwa na Wizara yangu pamoja na Taasisi zake katika kudhibiti hali hii ni kama ifuatavyo;

1. Kutoa Elimu kwa wananchi kwa njia ya Redio, Magazeti, Luninga pamoja na warsha mbalimbali juu ya utunzajiwa miundombinu ya maji.
2. Kushirikisha wananchi katika ulinzi wa miundombinu.
3. Kutoa motisha au vivutio kwa wananchi wanaotoa habari zitakazowezesha kuwakamata wahujuamu wa miundombinu ya usambazaji maji.
4. Kujenga chemba maalum za kuzuia vifaa vya majisafi na dira na viungio.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mbinu shirikishi za ulinzi, Serikali imepitisha Sheria mbili za maji ambazo ni *The Water Supply and Sanitation Act, No.12/2009* na *The Water Resources management Act, No. 11/2009*. Sheria hizi zinalenga kudhibiti vitendo vinavyosababisha uharibifu wa miundombinu na vyanzo vya maji na kusababisha wananchi kukosa maji. Chini ya Sheria hizi mtu ye yeyote atakayepatikana na makosa ya uharibifu wa makusudi wa miundombunu ya maji anaweza kutozwa faini hadi shilingi milioni tano au kifungo gerezani kisichozidi miaka mtiano au vyote kwa pamoja.

Aidha, Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko imeandaa Muswada utakaowasilishwa Bungeni kwa lengo la kutunga Sheria itakayodhibiti mfumo mzima wa

uzalishaji (Ukusanyaji), Uyeyushaji na uuzaaji wa bidhaa ya chuma chakavu ndani na nje ya nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kesi kadhaa zinazohusu uhujumu wa miundombunu ya maji zimefungulwia na Mamlaka za Majisafi na Majitaka katika Mahakama za Mikoa ya Sinyanga, Dodoma, Tabora, Mbeya, Moshi na Dar es Salaam na ziko katika hatua mbalimbali za kusikilizwa.

Mheshimiwa Spika, mwisho. Kwa kuwa, suala hili haliwezi kumalizwa na Wizara yangu peke yake, natoa wito kwa wananchi, kushikiana na Wizara yangu, Jeshi la Polisi, Polisi Jamii na Serikali za Mitaa kudhibiti uharibifu wa miundombinu ya maji na umwagiliaji.

**MHE. JUMA SAID OMAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, ni watu wangapi ambao hadi sasa wamefikishwa kwenye vyombo vy ya Sheria na ni hasara kiasi gani iliyopatikana kutokana na wizi pamoja na uharibifu wa miundombinu ya maji katika maeneo mbalimbali?

Swali la pili, pamoja na juhudini inayochukuliwa na Serikali lakini bado kuna maeneo ya mijini na vijijini ambapo maji ni tatizo? Wananchi wanayasikia maji kwenye matangazoya redio, kusoma magazeti nakuona kwenye luninga miradi ya maji ikifunguliwa katika maeneo ya mbali na kwao. Je, Serikali inawaambia nini wananchi ambao hadi sasa mijini na Vijijini maji kwao ni tatizo? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Juma Said Omar kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu takwimu hizi za watu wangapi na hasara kiasi gani labda niseme sitakuwa nazo hapa kama nilivyosema katika Mikoa hiyo, hiyo ni Mikoa tu michache ambayo nimeitaja lakini kesi zinapojitokeza zinaendelea kushughulikiwa. Basi mimi nitatafuta taarifa hizi maana nitazipata halafu nitampatia Mheshimiwa Mbunge ikiwa ni pamoja na kwamba hasara zilizokwisha jitokeza kutokana na uharibifu huo ni kiasi gani.

Kuhusu Serikali inasemaje kuhusu wananchi ambao wanayaona maji kwenye Luninga, jana Mheshimiwa Waziri alitoa kauli kuhusu utekelezaji wa miradi yetu huhusani mradi mkubwa huu wa vijiji 10 na mingine.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutekeleza hii program ya kuendeleza sekta ya maji na haiwezekani kabisa tukawa tumefikia wananchi wote kwa siku moja. Kama tulivyosema *program* hii inaendelea mpaka mwaka 2010-201.

Mheshimiwa Spika, tunaomba Mungu *Inshallah* itakapofika wakati huo tulivyokwisha jipangia wenyewe angalau basi 65% ya wananchi walioko huko vijiji tuwe tumewafikia, naomba avute subiri kwa kuwa tunaendelea kutekeleza program hii kwa ajili ya kuwafikia wananchi ambao hatujawafikia. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umeshapita, sasa ni matangazo, nikianza na wageni.

Wageni wa Mheshimiwa Sigifrid Seleman Ng'itu wa Ruangwa ni mdogo wake anaitwa Dickson Ng'itu ambaye amefuatana na Mkewe Lena Ng'itu. Naomba wasimame pale walipo. Karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni wa Mheshimiwa Anthony Diallo, Mbunge wa Illemela, wageni kutoka soko la Samaki Mwaloni, Mwanza ni Ndugu Novalt Manoko na Ndugu Jacob Mgomi. Karibuni sana na ahsante sana.

Mgeni wa Mheshimiwa William Shellukindo ni Ndugu Paul Twakyondo, Katibu wa Itikadi, Siasa na Uenezi wa CCM Wilaya ya Lushoto, kumbe wako wawili, karibuni sana.

Wageni wa Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu ni wanafunzi 25 kutoka Shule ya Sekondari ya Azania Dar es Salaam wakiongozwa na Mwalimu Msuya pia na Kiongozi wa wanafunzi Abdul Mohamed na Khamis Kundya, Katibu CCM Kata ya Upanga. (*Makofi*)

Ahsante Mwalimu na Vijana mnasoma shule nzuri tunawaombea mfanye vema katika masomo yenu. Tanzania inawahitaji nyote katika fani mbalimbali. Karibuni sana na Mungu awabariki sana. (*Makofi*)

Wageni wa Mheshimiwa Teddy Louise Kasella-Bantu, ambao ni Madiwani. Mheshimiwa Fatma Omar, Mheshimiwa Pelle Izengo, Mheshimiwa Kagheme Magaka ambaye pia ndiyo *Head Master* wa *Mogwa Secondary School*, Mheshimiwa Mihayo John, Mheshimiwa Juma Maduku na Mheshimiwa Lawrence Mashenene.

Wapo pia Walimu na Wanafunzi wa *English Medium Primary School* ya Bukene, labda hawakupata nafasi.

Walimu na Wanafunzi wa Shule ya Msingi Ilagaja, Viongozi wa Chama cha Mapinduzi ambao ni Wenyeviti na Makatibu wa Kata kule Nzega. Karibuni sana na ahsante sana. (*Makofi*)

Bwana Babu Raja Katibu wa *TFF* Wilaya ya Nzega, karibu na ahsanteni sana na Ally Mwinyimvua ambaye ni Katibu wa Mbunge. Katika msafara pia wapo wale wajukuu wote wa Mheshimiwa Mbunge wasimame. Karibuni sana. (*Makofi*)

Mgeni wa Mheshimiwa John Momose Cheyo na Mheshimiwa Andrew Chenge Wabunge wa Bariadi ni Ndugu Sylvester Maghembe Cheyo, naomba asimame pale alipo. Karibu sana. (*Makofi*)

Nadhani huyu hana upande wowote ni mgeni wa CCM na *UDP*. (*Kicheko*)

Wageni wa Mheshimiwa Feteh Saad Mgeni, Mheshimiwa Ephraim Nehemia Madeje na mwenyeji hapa Dodoma Mjini ni Wanafunzi 20 wa *Madrasah Mubarak Islamic Centre Dodoma*. Hakika mmependeza kweli kweli na mavazi yenu, karibuni sana na tunawatachia mema hasa ninyi kwa sababu mnajifunza pia si masomo tu lakini mnajifunza maadili. Tunawapongeza sana Walimu na wanafunzi wa *Madrasat Mubarak*. (*Makofi*)

Wanaongozwa na Shehe wa Madrassa yaani Shekh Abdallah Ally Athuman na Naibu Mudiri wa Madrasa Ustaadh Mohamed Ally Kerry. Naomba wasimame, karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni wa Mheshimiwa Jenista J. Mhagama ni Victor Mhagama ambaye ni mwanaye na pia Leonard Mhagama ambaye ni Shemeji yake. Karibuni sana. (*Makofi*)

Pia wapo wageni wa Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir na Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa wa kwanza ni Msanii maarufu sana huyu, Ndugu Masoud Kipanya, karibu sana Masoud tunafurahia sana ubunifu wako katika kitu kipyaa umeleta nchini kinachoitwa, *Maisha Plus*.

Sasa yupo pia Ndugu David Sevuri ambaye Mratibu wa Maisha Plus, Francis Bonda ni Mratibu mwingine, Sizza Mwakisopile *Camera man* yaani mpiga picha na sasa huyu mumshangilie vizuri Waheshimiwa Wabunge. Huyu ndiye Abdul Hafidh, mshindi wa *Maisha Plus*. Abdul hongera sana wewe unadhihirisha vipaji ambavyo Watanzania tunavyo, kijana mtanashati wa Zanzibar umefanya mambo mazuri sana.

Kwa taarifa tu Abdul anajiandaa kupanda mlima Kilimanjaro ili kukusanya fedha za kujenga clinic ya wagonjwa wa kisukari Zanzibar kwa kushirikiana na *Diabetic Association of Zanzibar*, anatuomba Wabunge tumuunge mkono. Basi Masoud Spika anapenda kutangaza hapa kuwaunga mkono kwa shilingi 300,000/= uje uzichukue kabisa mara ukiniona nimetoka hapa uje uchukue mambo mazuri haya watu wanafanikiwa, tukajenge clinic ya Kisukari kule Zanzibar. Ahsante sana na mmetufurahisha sana. (*Makofi*)

Wageni wa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo Dr. Mathayo David Mathayo ni Ndugu August Kessy Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Same karibu sana Mwenyekiti.

Mwenyekiti wa *VUASU Cooperative Union* Ndugu Khamis Msuya, karibu sana. Natumaini mnaendeleza kilimo cha Kahawa. Nilipokuwa Mkoo wa Mkoa huko mwaka 1990 – 1991 nilihimiza sana kilimo cha Kahawa kule Upareni. Pia Meneja Mkoo wa

*VUASU* Mheshimiwa Diwani John Kiure. Karibu sana. Huo ndiyo mwisho wa matangazo ya wageni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Job Ndugai, Mwenyekiti wa Ardhi, Maliasili na Mazingira anaomba Wajumbe wote wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira wakutane leo Saa Saba mchana, katika ukumbi namba 231 jengo la utawala.

Waheshimiwa Wabunge, mnatangaziwa kwamba kesho jioni baada ya kuahirishwa Bunge kutakuwa na tafrija ya Wabunge katika viwanja vya Bunge itakayofadhiliwa na Kampuni ya Simu ya *Zain*. Aidha, kutakuwa na *dance* itakayotumbuizwa na Mwanamuziki Mbillia Bell. Hii ni kweli hii? Mbillia Bell yuko hapa? Aisee kesho ni kazi hata wazee tutajikongoja. Kwa hiyo, *dance* kesho kwenye sehemu yetu ya tafrija pale. (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, nawatangazia kwamba kutakuwa na uchaguzi mdogo wa Wajumbe wawili wa Tume ya Utumishi wa Bunge, kama mnavyokumbuka nilitoa taarifa tarehe 10 Juni, 2009 kwamba kutakuwa na uchaguzi mdogo wa kuziba nafasi mbili za uwakilishi kwenye Tume ya Utumishi wa Bunge. Sasa, uchaguzi huo kwa mujibu wa Katibu wetu wa Bunge utafanyika Jumatatu tarehe 6 Julai, 2009 sasa wale wanaotaka kugombea itabidi wakachukue *form* hivi sana na wazireshe kabla ya saa 10.00 jioni siku ya Ijumaa tarehe 3 Julai, 2009.

Kwa hiyo, kabla ya saa 10.00 tarehe 3 Julai, 2009 wale wanaogombea ambao kwa taarifa yenu ni Wanawake tu mmoja kutoka Chama cha Mapinduzi (CCM) na mmoja kutoka Kambi ya Upinzani, wanaume msijishughulishe hammo kwenye hiyo aliyeingia ni kiongozi wa Kambi ya Upinzani na kwa kuweka usawa wa Jinsia. Waheshimiwa Wabunge Wanawake wawili wa vyama mbalimbali. Kwa hiyo, siku ya uteuzi tarehe 3 Julai, 2009 kabla ya saa 10.00 form ziko tayari zikachukuliwe, Jumatatu tarehe 6 Julai, 2009 Bunge litapiga kura kuwachagua hao.

Waheshimiwa Wabunge, naomba sasa Kamati ya Uongozi tukakutane hapa *Speakers Lounge* kwa dharura kuzingatia mabadiliko ya ratiba kama tulivyokubaliana. Kwa hiyo, mara nikimaliza kusoma matangazo haya tukutane Ukumbi wa Spika, Kamati ya Uongozi wote tafadhali ili tuweze kupata uamuzi na tuwatangazie Wabunge wenzetu.

Baada ya matangazo hayo namwomba sasa Mheshimiwa Mwenyekiti Job Y. Ndugai, aje aendeshe shughuli hadi hapo baadaye.

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti*

## **HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2009/2010  
Ofisi ya Waziri Mkuu na Tawala za Mikoa na  
Serikali za Mitaa**

(Majadiliano yanaendelea)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, majadiliano yanaendelea na mchangiaji wetu wa kwanza ni Kiongozi wa Kambi ya Upinzani na atafutiwa na Mheshimiwa Juma Njwayo.

Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed karibu!

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Awali ya yote naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waziri wa Nchi na Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kusimamia kwanza utekelezaji wa maamuzi ya Serikali lakini vilevile kusimamia *program* mbalimbali ambazo Waziri Mkuu aliziwasilisha katika Bajeti yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza nianze na kusema kwamba niiombe Serikali baada ya Baraza la Mawaziri kutoa maamuzi, lile Baraza la Mawaziri la Kazi liweze kusimamia hizi kazi kwa ufanisi zaidi. Nasema hivi kwa sababu moja katika matatizo tuliyogundua na ambayo kila Mbunge ananyanya kusema hapa tuna wasiwasni na namna ya utekelezaji.

Kwa hiyo, suala la utekelezaji ndiyo tatizo la msingi tulilonalo hapa kwetu, nafikiri hili linataka kusimamiwa vizuri na ningombwa Waziri Mkuu kama Kiongozi katika Baraza la Mawaziri la Kazi hili lisimamiwe kwa ukaribu zaidi.

Lakini la pili, ni suala zima la kuziwezesha Halmashauri zetu. Bado katika Halmashauri kuna uwezo mdogo sana na mpaka sasa hatujafika mahali tukasema Halmashauri fulani angalau imefikia asilimia fulani na ikawa kigezo ni kigezo kwa Halmashauri nyiningine.

Mimi nafikiri twende na utaratibu wa kusema angalau mwaka huu katika Halmashauri 130 tulizonazo basi angalau 10 zimefikia kiwango gani kwa sababu ukisoma taarifa ya Mdhhibit na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali bado unaona matatizo ni yale yale bado yanajirudia. Mimi nilifikiri katika maeneo hayo mawili ni vizuri sana Serikali ikajielekeza.

La tatu, ni masuala ambayo bado Serikali haijatoa majibu sahihi. tumekuwa kila wakati tunarudi katika Bunge tunazungumzia masuala hayo hayo, kwa mfano hii mradi ambayo ilianzishwa na Serikali kwa nia nzuri lakini kwa bahati mbaya wajanja katikati wakatumia nafasi hiyo vibaya.

Sasa hapa mimi nataka kusema mambo mawili. Wakati mwingine tunavitumia vyombo vyya Ulinzi na Usalama kwa maslahi binafsi, tukielewa kwamba vyombo hivi ni nyeti haviwezi vikazungumzwa sasa tusichanganye mambo haya mawili yaani unyeti

wa chombo na mtu anayetumia fursa ya chombo akaiba fedha sasa akapata kivuli cha kutumia chombo, nasema hili ni tatizo ambalo nalionna mbele yetu litatupa matatizo.

Nakumbuka mwaka 1980 Jeshi la wananchi baada ya kukaguliwa na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na baadaye *PAC* ikagundua kama kuna baadhi yao walifanya vibaya, Mwalimu alichukua hatua ya haraka sana kwa wale waliofanya vibaya wala hakuona taabu. Sasa mimi nasema tutenganishe baina ya chombo chenyewe na mtendaji aliye ndani ya chombo chenyewe na mtendaji aliye ndani ya chombo akifanya ubadilifu halafu asivae kofia ile ikaonekana hilo jambo ni nyeti, haliwezi kujadiliwa, hapana! Tunafanya kosa. Anayevunja Sheria achukuliwe hatua kwa mujibu wa Sheria. Kwa hiyo, tumesema suala la Meremeta limekwisha na kadhalika lakini ukitazama sana pengine si Jeshi lililofaidika. Kuna mtu alifaidika tunamlinda pengine. Sasa hili ndilo tatizo ambalo mimi nalionna Serikali lazima ijielekeze tutofautishe baada ya kosa la chombo na tatizo la mtu binafsi aliyefanya kosa katika chombo. Mimi nafikiri hii ni kasoro moja ambayo naiona ni vizuri tukaielekeza katika hii. Kwa mfano kampuni yenewe *CIRCE Mauritius* aliyeipeleka Mauritius ni nani? Siyo Jeshi! Kwa hiyo, nasema haya ni mambo ambayo yanahitaji tupate maamuzi na maamuzi yapatikane. Hili lilikuwa ni jambo moja ambalo nilikuwa nataka kulisemea. La nne, ni suala la matumizi ya manunuvi. Kama kuna *area* ambayo Serikali ingekuwa makini tungeweza kupunguza matatizo makubwa ya rushwa, manunuvi hewa na upotevu wa fedha na vifaa katika manunuvi.

Mwaka 2005 tulishauri sana juu ya matumizi ya *electronic procurement*, Serikali imefanya *studies* miaka yote hii mpaka leo hajaja na jibu na sababu yake ni moja tu nakumbuka Mheshimiwa Mkapa aliwahi kuniuliza katika Viwanja hivi vya Bunge, hivi kwa nini Hamad tunashindwa kuitekeleza ile *electronic procurement*? Nikamwambia ni kwa sababu inazuia rushwa! Na ninarudia ni kwa sababu inazuia rushwa, ukishatumia ule utaratibu maana yake ni *transparent* kila mtu anauona. Sasa *studies* zimefanywa miaka na miaka *billions of money* tunazipoteza kwa sababu ya kwenye *procurement* hivi ni kwa nini Serikali haifikii maamuzi katika suala la *electronic procurement* leo *PPRA* bado inaitegemea Serikali kuipa ruzuku, wakati ikianzisha utaratibu huu *PPRA* yenewe inaweza kujitegemea na ika-generate revenue ikaisaidia Serikali. Sasa mimi nasema haya ni maeneo ambayo Serikali inatakiwa kuyaangalia na kuyatolea ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la maeneo ambayo tunaweza kuvuna kwa haraka. Suala la uvuvi tumelisemea humu Bungeni mpaka tumechoka, leo imetokea boti moja ya *South Africa* ndiyo imemsaidia Waziri Magufuli ndiyo wakakamata meli moja. Hivi kweli kama kuna *seriousness* ya kusema hizi raslimali zetu zinachukuliwa hatuwezi tukatenga fedha sisi tukakiwezesha kikosi chetu cha *Marine* au cha *Navy* au cha Polisi au vyote viwili tukapata boti ya kufuutilia hizi raslimali zetu zinazopotea? Hii inashindikana nini? Ikiwa meli moja tu kwa taarifa za Mheshimiwa Magufuli ni zaidi ya milioni mbili na kitu dola, meli moja tu lakini yeye amesema milioni 200 hebu tupige mahesabu. *Are we serious* katika kutafuta revenue za nchi?

Mimi nafikiri bado hatujawa *serious* na hili ningeomba kabisa Serikali ijielekeze hapa ni kuvuna, hapa ni mahali pa kuvuna, siyo mahali pa kuwekeza, hapana! Ni mahali

pa kuvuna tu, tumsaidieni Magufuli akafanye hiyo kazi tupate revenue. Leo ni aibu kwa Tanzania ile *spirit ya self reliance* haipo, tukija hapa tunapiga Makofi tumepata msaada hapa, kofi! Ndiyo kazi yetu tu sasa kupiga Makofi kwa kuomba misaada *self reliance concept* imekufa wakati tunazo *resources* ndani ya nchi za kutosha kabisa hatuhiji misaada, *resource* tunazo zaidi kuliko Kenya mara kumi, Kenya wamejielekeza ndani kusimamia bajeti zao, sisi bado tunapiga Makofi nani katusaidia, kofi! Kenya wamejielekeza ndani kusimamia bajeti zao, sisi bado tunapiga Makofi, nani katusaidia, kofi! Si fahari, ni aibu kwa nchi ambayo raslimali.

Tujielekeze katika *resources* zetu tulizonazo ndani na uwezo wa kufanya hivyo tunao ni suala la maamuzi tu, ningeomba suala la wavuvi lisimamiwe sana. Suala lingine ni mifugo. Mifugo ni eneo lingine la mavuno tu, milioni 13 ya mifugo iliyopo Tanzania ni mavuno. Saudi Arabia wanaagiza mifugo kwa ajili ibada ya Hijja si chini ya milioni 5 au 6 kila mwaka wanatoa Australia na kadhalika. Juzi Uganda wamepata *contract* ya mbuzi tu 10,000 hivi sisi Tanzania hatuna mbuzi 10,000? Tunao na masoko yako hapo.

Mheshimiwa mwenyekiti, mimi nilishawahi kusafirisha Mbuzi, Uarabuni hapo Dubai ambapo ilikuwa ni dola 100/= kwa mbuzi mmoja, *live!* hapa ni 15,000 au 20,000 ni suala la kuwatuza miezi mitatu au sita mahali ukaweza kupakia vizuri wakaenda wanakwenda hata kwa Ndege siyo lazima kwa meli. Hatuna tu ile tufikiri kwamba ni namna gani tutumie raslimali hizi tuondokane ya matatizo ya ombaomba, hatufanyi! Hebu tujitahidi kujielekeza katika maeneo haya mawili ya Uvuvi na Mifugo tunaweza tukavuna hiyo itawasaidia hata wenzetu wanaochunga kwa wingi wakishajua kuna soko la hakika watapunguza mifugo yao badala ya kusumbuana sumbuana nayo. Hilo la pili!

Lakini la tatu, tunataka kuwabdalisha hawa wafugaji, wawe wafugaji wazuri, mfugaji mzuri anajifundisha kutokana na kitu ambacho amekiona ndiyo tatizo la wafugaji, ni lazima aone.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi mimi nilikwenda Pemba kwenye jimbo langu, kuna Mchima mmoja amenifundisha utaratibu wa kuvua Kaa, sijui kama mnawajua Kaa, *crapes*. Watu wangu wanajua kuvua Kaa, wanachukua hours *and hours* kuvua, ye ye alikwenda pale na mitego ile, dakika 20 tumevua kilo Tatu, *twenty minutes*, akatupa mitego 40. Kumbe tukiwa na teknolojia ndogo tu ambayo ni *manageable*, tunaweza tukaongeza *revenues* zetu. Haya yote yapo, lakini hatuyafanyii kazi, tunazungumza tu, ukitazama miradi hiyo fedha zinazokwenda kwa *Administration* ni asilimia 60, hebu tuangalie, hii *Administrationi* kweli inahitaji Milion 60? Asilimia 60 inakwenda kwenye utawala kwa hivyo mtu wa kawaida huku chini hii haimfikii hata kidogo.

Ndiyo maana tatizo la wafugaji, wafugaji wanasantaa kwa sababu hakuna pahala pa kuogesha ng'ombe wake, hapana pahala ambapo atapata madawa ya uhakika. Kwa hivyo atatangatanga tu, kutafuta majani kwa sababu *only solution* aliyonayo ni majani, na kama majani hayapo, na maji atatafuta tu, atahangaika tu. Kwa hivyo hata yale maeneo ambayo hayajafikiwa na wafugaji wazuri, hawa tunaowataka, nayo vilevile sasa tumeyasambazisha maradhi yaleyale ya kufuga kwa kuchunga. Sasa mimi nasema, bado

mipango yetu haijakuwa vizuri ya kuangalia *area* gani tunaweza ku- *concentrate* na mavuno ni ya haraka, tukaweza kuyapata. Mimi nafikiri hilo tungeweza kuliangalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jingine ambalo lingeweza kutusaidia, ni suala la maamuzi ya Serikali. Hivi unaandika barua serikalini hupati majibu na Serikali inaenda kwa nyaraka tunategemea ufanisi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi mwenyewe nimekwishaandika barua nyingi sana, bahati nzuri Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Pinda, ni mwepesi kidogo wa kujibu, lakini wengine wazito wa kujibu. Kama mtu hajibiwi barua, hata kusema tu kwamba mimi sitaki, basi nayo ni majibu, au usiniandikie tena sitaki tena kupata barua yako, nayo ni majibu, *government goes with the papers*, kama hakuna, Serikali haitembe na makaratasi, Serikali haifanyi kazi, hili ningeomba sana tulifanyie kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jingine ambalo ningependa kuwaambia wenzangu ni kwamba, sisi tuna utaratibu wa vikao vya *briefing* halafu tuna vikao vya *caucus*. Mambo mengine hebu tuyazungumze kwenye vikao vya *caucus*. Maana sie tumefunzwa kule nyumbani kwamba, kama mkigombana na Mama, ugomvi haukulalizika katika kile chumba mnachokaa, mkiutoa nje huo ugomvi una matatizo makubwa zaidi. Hiyo ndoa haipo.

Tumalize mambo ndani, tuna kikao cha *briefing*, tuna vikao vya *Caucus* yale mambo yanayotuhusu sisi binafsi, tukayazungumzie kule ndani, ndiyo ushauri wangu, kama mtu mzima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Kilimo Kwanza. Tumezungumza sana suala la Kilimo, miaka mingi sana, hebu *tu-zero in*. Serikali ilikuja na mpango wa kuwa, Morogoro ni ghala la chakula, na ukatangazwa na Rais akatwambia bwana sasa Morogoro utapata 25 bilion, ni ghala la chakula, programu imekufa.

Lipo tatizo la kuwa na programu nyingi katika nchini. Hebu *tu-minimize* hizi programu, MKUKUTA, MKURUBITA, *VISION* ngapi. *Tu-zero in* kwa sababu moja tu ya msingi, *capacity* yetu ya kutekeleza ni ndogo. Ukitizama kitabu cha *Auditor General*, anatueleza hata Serikali Kuu uwezo wa kutekeleza ni asilimia 65, nenda kwenye Halmashauri huku chini hali ikoje? Hasa unapokuwa na programu nyingi uwezo wa watu kutekeleza ni mdogo. Kwa hivyo unafika wakati hakuna programu ambayo inamalizika. Tuwe na programu chache, ambazo zinaweza kutekelezeka, zina usimamizi mzuri ili tuweze kufika ambapo tunataka kwenda, vinginevyo tutakuja hapa kila siku, Bajeti yetu kubwa, na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabisa ningeomba Wizara ya Fedha, ijitahidi sana kuangalia haya mafungu ya Bajeti. Ukiyachambua mle ndani utapata matatizo sana, na tulilizungumza hili, kuna haja ya kuangalia mfumo wa *Budgeting System* yetu, vifungu vina-*overlap*, vinajirudiarudia kwa hiyo matumizi mengine ya ovyo ovyo mengi tu yako ndani. Sasa wakati mwingine unaposema inaonekana kama unataka kushambulia, hapana! Ni jambo ambalo ni letu sote, tuna wajibu kwa *resources* ndogo tulizonazo, zitumike vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi kutumia *resources* vizuri kama unazitawanya kama karatasi. Kama unazo pesa za kununua matrekta 2000, nunua matrekta 2000 ukalime, acha mambo mengine.

Wenzetu Kenya hapo wamekata *furnitures*, wamekata chai, wamekata mambo mengi, hata gari ile ya kuendea Waziri siku ya Bajeti, mnaona gari nyininge kabisa ambayo inalingana na hali halisi waliyonayo. Hebu tufanye hivyo. Mheshimiwa Waziri, kakaeni kitako muangalie *Budget System* yetu bado ina matatizo, kuna *loop holes* nydingi, kuna pesa nydingi zinazagaa ovyo ovyo. Tuzielekeze ziende kwenye Halmashauri zikafanye kazi. Kule chini kwenye Halmashauri ndiyo muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, namwomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, wakati mwingine tumefanya chaguzi halafu matokeo yanabadilishwa, hebu tuiambie Tume ya Uchaguzi ya Taifa, ishirikiane na hizi chaguzi za Halmashauri. Tuwe na watu wa kuajiriwa wa tume hata wa muda, kwamba kipindi hiki cha uchaguzi kimefika basi hawa ni watumishi wa tume, hawa maafisa ambao wameajiriwa na Serikali, chama kilichopo madarakani kwa vyovoyote vile katika hali ya kawaida ya kibinadamu atapendelea tu, uwezo wa kutoa haki utakuwa ni asilimia ndogo sana. Ni ndogo sana! Ni kama vile ambavyo tulitoka na mfumo wa chama kimoja tukawaambia askari wote wawe wanachama wa chama cha siasa. Sasa tumebadilisha leo kila mtu anaona wasiwasi kutoka kuingia kwenye chama kingine, kwa sababu tu ya mawazo tuliyokuwa nayo ndiyo maana unapata migongano huko Zanzibar haishi kila siku majeshi mengi yanapelekwa wakati wa Uchaguzi na kadhalika. Haya ni mambo ambayo yanahitaji kuangaliwa upya. (*Makofi*)

Kwa hiyo, mimi ushauri wangu ni kwamba, kwenye Halmashauri kwanza, wafundishwe Wakurugenzi wa Halmashauri kwamba, wao wanayo *role* ya kufanya kazi na kuwapelekea Madiwani watoe maamuzi. Unapokuta kama *adimistration* ni mbovu, Madiwani wanapata nafasi nao kuingilia maamuzi, hii si sahihi. Ule utendaji ufanywe na watendaji na baraza la maamuzi litoe maamuzi, mimi nafikiri hili linahitaji kusimamiwa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuru sana na nategemea kuiunga mkono hoja hii. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru kwa mchango wako, Mheshimiwa Hamad Rashid, Kiongozi wa Kambi ya Upinzani. Atafuatiwa na Mheshimiwa Juma Njwayo, Mbunge wa Tandahimba na baada yake atafuatia Mchungaji Luckson Mwanjale, Mbunge wa Mbeya Vijijini. Mheshimiwa Njwayo endelea.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi asubuhi hii ili niungane na Wabunge wenzangu kutoa mchango wangu kwenye hotuba ya Waziri Mkuu. Awali ya yote, naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa namna anavyoweza kumudu majukumu yake ya kazi, naomba pia kumpongeza

Waziri wa nchi TAMISEMI, na Naibu Waziri wake, Waziri wa nchi Sera, Uratibu na Bunge, Watendaji mbalimbali walioko chini ya Waziri Mkuu, kwa ufanisi wa mambo mengi wanayoyafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hotuba hii ya Bajeti na kwa kweli napenda kuipongeza kwa mipango mizuri ya kuiendeleza nchi yetu ikiwa ni pamoja na Mpango maalum wa kutenga Bilioni 7 kwa ajili ya kurekebisha tatizo la umeme la Nyangao-Ndanda, ambao kwangu nadhani utakuwa ukombozi wa huduma nyingi za kijamii katika Mikoa ya Mtwara na Lindi, hasa Wilaya ya Newala, Tandahimba, Mtwara, Masasi, Ruangwa na Nachingwea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi ni wazuri sana wa kupanga mipango, tatizo letu ni urasimu tu wa utendaji na utekelezaji wa mipango hiyo. Naona sasa wakati umefika kuweka jitihada za makusudi kuepukana na mambo haya ya urasimu. Kuna mambo mengi ya urasimu ambayo yanatufikisha pabaya bila misingi na sababu yoyote, tuamke sasa tuanze upya, tukikubaliana tukifanya maamuzi ya msingi, pia utekelezaji wake ufanywe mara moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nina mifano. Kwenye *Finance Act* ya 2006 tulipitisha hapa suala la *export levy* na kwamba, Wilaya zinazolima Korosho zingepata asilimia 6.5 ya mauzo ya nje ya Korosho. Hivi sasa ninavyoongea Wilaya hazijapata hadi leo, ukimwona Waziri wa Fedha, utaongea naye vizuri, akiwaagiza watendaji wake kesho, kesho kutwa, subiri, subiri, subiri wakati wa kufanya *dusting* ndiyo huu, wakati wa kupalilia ndiyo huu, na tumesema Kilimo Kwanza, hivi tusipoweka mikakati ya makusudi ya kuendeleza na kufanya utekelezaji, mambo haya yatafanikiwa? Mimi nafikiri tuachane na tabia hii hasa kwa watendaji wetu, watendaji wetu ndio wanaotuangusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nitoe mfano mwengine. Tumepitisha maamuzi mengi sana hapa ya kuendeleza bandari zetu, lakini mambo yaleyale yako shaghlabagala, katika utekelezaji utaambiwa, watu wa bandari watakwambia hili, watu wa Wizara ya fedha pale watakwambia hivi na hivi, mimi labda nimwombe Mheshimiwa Waziri Mkuu, atusaidie na kutusaidia kwenyewe aige mfano wa bosi wake, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alipokuwa anaweka jiwe la msingi la mradi wa umeme wa *ARTUMAS* kule Mtwara. Kulikuwa na mpango wa kuepeleka umeme Lindi, akawaambia, ilikuwa Mwezi Novemba, mimi nitakuja wakati wa Krisimasi Lindi, mwezi Desemba, kama kuna mtu hapa anadhani hatatekeleza hilo, aseme sasa hivi. Lakini mimi mwezi Desemba nitakapofika nataka nikute umeme, jambo ambalo lilifanikiwa. Watu walihangaika, umeme ukawepo. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, ufanye kazi karibu na hawa, uwabane wakati mwengine uwalazimishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hii mipango mizuri ya kuondoa *steve doring charges* kwenye bandari zetu, wala hazitafanikiwa kwa ubabaishaji uliopo pale bandarini. Namimi nataka niseme watu hawawezi kutoka pale bandarini kwa sababu wana mipango yao binafsi ya kupata fedha mifukoni mwao, habari ya utaifa umepungua kwa kiasi fulani. Kwa hiyo tusipowakazania, tusipoweka mikakati pale, tutaendelea, leo

watatabadilishia lugha hii, kesho watatupa lugha hii, Mtwara hawatakwenda, Tanga hawatakwenda, Mwanza hawatakwenda na mahali pengine, lazima tuwabane hawa ndipo tutafanikiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, uko mfano niliwahi kusoma mahali miaka ile ya 1966 aliyekuwa Rais wa Nigeria, baada ya vita ya Biafra Rais Gowon, alimtaka Waziri wake wa bandari na Mawasiliano, amwambie ana mikakati gani ya kupunguza msongamano kwenye bandari ile ya *Port Harcot* pale Nigeria. Brigedia Adimkule, ndiye alikuwa Waziri wakati ule, maarufu kwa *jina la Black Scopion*. Baada ya kupewa maagizo yale na Rais wake, alirudi kwa Wataalam, Watendaji wake, wakamwambia bwana, msongamano pale hauwezi kuisha mpaka miaka tisa (9), ndiyo mkakati uliopo. Lakini ye ye akasema hamna, miezi Sita tu. Kwa kuwabana, jambo hili lilifanikiwa, msongamano ukawa umepungua kwa kiasi kikubwa sana. Mimi nadhani *ideas* zile, mawazo yale, yatumike hapa kwetu. Bandari ndugu zangu, ingeweza kuchangia robo ya uchumi wetu. Tunacheza tu na bandari wakati inaweza ikatuletea mambo mengi ya manufaa? Mimi nafikiri tubadilike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa na la utaifa zaidi, sasa nirudi jimboni kwangu. Jimboni kwangu kuna matatizo kweli, ya watumishi, matatizo makubwa. Mimi naomba Serikali inisaidie, nafa jamani, tatizo kweli watumishi kule. Natambua jitihada za Serikali katika jambo hili na nimeona kwenye Ibara ya 39 *page 32* ya Mheshimiwa Kombani, anavyotaka sasa wafanyakazi hasa Walimu, waende kwenye Halmashauri za Wilaya. Ni mpango mzuri, lakini kama nilivyotangulia kusema, tutabadili hapa, wala yanaweza yasiwe yamekamilika. Mimi naomba mnipe kipaumbele katika jambo hili nina tatizo sana la watumishi.

Nataka kuwaonyesha tu mfano wa baadhi ya sekta mbili tu, nitatoa mfano wa sekta ya elimu na afya. Pale kwangu Tandahimba mahitaji ni Madaktari Watano, lakini waliopo ni wawili, kwa hiyo ni upungufu wa asilimia 60. Madaktari Wasaidizi wanahitajika 10, waliopo ni wanne (4) nina upungufu wa Madaktari Wasaidizi Sita (6), asilimia 60 vilevile, Matabibu mahitaji ni 78 waliopo 32, nina upungufu wa 46, karibu asilimia 60 hivyo hivyo. Maafisa Wauguzi, mahitaji ni 40 waliopo ni 10, 38 sina, upungufu wa asilimia 79.2, Wauguzi wa kawaida, wanahitajika 128, waliopo 39, nina upungufu wa Wauguzi 89, asilimia 70. *Medical technicians*, wanahitajika 49 waliopo ni wanne (4) nina upungufu wa 45, asilimia 81, hii ni hatari hii. Hapa mambo hayaendi hapa, hakuna maendeleo kwenye hali ya namna hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu elimu. Maafisa elimu afadhali kidogo, maana wanahitajika wanne (4) wapo watatu (3), upungufu wa mmoja, lakini Maafisa wa elimu Wasaidizi nao kidogo wameniondoa tatizo maana wanahitajika 27 lakini waliopo 39, nina ongezeko la Tisa (9) nafuu. Lakini Walimu wa *primary* wanahitajika 1151, nina 828 upungufu wa walimu 323.

Walimu wa Sekondari, wanahitajika 403 nina Walimu 117, upungufu wa Walimu 286, karibu asilimia 71. Nimechukua mifano miwili tu, kwenye eneo hili muone tatizo

nililo nalo, ni kubwa, nilikuwa naomba Serikali inipe kipaumbele katika jambo hili, angalau upungufu huu wa watumishi upungue.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, inataka kuhakikisha kwamba, katika muda huu wa miaka mitano kwa maana ya kufikia 2010, tumepunguza tatizo la maji vijijini kwa asilimia 65. Mimi kwangu hali ni mbaya sana, nina asilimia 33 tu ya upatikanaji wa maji na hata wilaya jirani zinazonizunguka hali ni hivyo hivyo. Ombi langu ili kuufufua mradi wa Makonde, ili usaidie Newala, Tandahimba na Mtwara Vijijini, kunahitajika kama bilioni 4, Serikali inatusaidia, imeishaleta mashine mpya kule Nne, nawashukuru sana, imeishaleta pesa karibu milioni 800 mwaka huu, lakini hizi hela kidogokidogo hizi hazileti *impact* na inachukua muda mrefu sana. Mimi naomba tutafute bilioni 4 za pamoja, mara moja tupeleke kule, tufanye mambo mara moja ya ishe, kama tulivyofanya Shinyanga, Maswa, tuondoe tatizo mara moja badala ya polepole hivi. Mimi nadhani Serikali haiwezi kukosa bilioni 4 ya kumaliza tatizo hili moja kwa moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa hali ni mbaya kwa sababu Tandahimba na Newala, ndoo ya maji ni shilingi 500/=, na labda nimekosea jambo moja hapa niliseme, mimi ni Mwenyekiti wa Bodi ya Maji ya Makonde, na unapokuwa Mbunge, Mwenyekiti wa Maji ya Makonde na mambo hayaendi vizuri nadhani mnajua, wote ni viongozi hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Elimu. Nashukuru jitihada za Serikali tumefika mbali, mimi wakati naingia kuwa Mbunge, tulikuwa na shule Tisa (9) tu za Sekondari, sasa nina shule 26, Serikali imetusaidia sana, mambo mengi mazuri yanaendelea na kule ilikuwa kwenda *Form Five* mpaka usome nje. Kwa mara ya kwanza, mwaka huu vijana wanaotokana na shule Tano zilizofanya mtihani wa *Form Four* kule watoto 40 ndani ya Tandahimba wameenda *form Five*, jambo kubwa. Kwa wilaya kama zile za Kilimanjaro unaweza ukachecha maana hilo ni suala la kijiji kimoja tu, lakini kwetu ambako kulikuwa hakuna shule, sasa kuna shule una watoto 40 ni maendeleo makubwa, nataka niipongeze Serikali kwa jambo hili, lakini iko mikakati lazima ifanyike. Mikakati yenyewe ni ya kuhakikisha kama niliviyotangulia kusema, Wataalamu, Walimu, Maabara na vitu vinavyoendana na kupandisha elimu yetu, lazima vipatikane kwa haraka ili tuweze kusonga mbele. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia niiombe Serikali kwenye Ilani mle tulisema, chuo cha ualimu Mtwara, tunakifanya chuo Kiambata, hatua hiyo hatujafikia na umebakia mwaka mmoja tu, leteni hiyo sheria. Niliuliza hapa mwezi wa nne nikaambiwa ooh, Sheria, kuna ugumu gani, tunaopitisha Sheria si sisi? Leteni hiyo Sheria tuipitishe hapa, hili jambo tuendane na Ilani ndiyo ilikuwa ahadi yetu kwa wananchi, tunangoja nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiko chuo cha Ualimu Kitangari, Wilaya ya Newala, Mtwara kinatusaidia sana kupata Walimu katika mikoa ile ya Mtwara na Lindi, wa *Primary*, lakini tangu kimeanzishwa kilichukuliwa kwa wenzetu Wamisionari, tukakiwekaweka vizuri kidogo lakini hakuna ukarabati wa maana pale, nimefika pale

chuoni, wanafunzi wanaazima mpaka nyumba za wananchi walioko jirani pale, na Father Philip aliyeko pale karibu, mimi nafikiri wakati umefika sasa tusaidie pale, tupakarabati tupaweke sawasawa ili vijana wanaoenda pale wasome angalau katika mazingira ya kuridhisha. Naambiwa mpaka watoto wa kike pale wana-share vitanda, jambo ambalo si zuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kuupongeza uongozi wa Chuo Kikuu cha *Saint Augustine*, Mwanza, kwa kuamua kwa makusudi kuja Mtwara. Wameanza kukarabati majengo ya Umisionarini pale, *Shangani Parish*, na Mungu akipenda mwezi wa Tisa wataanza kuchukua *intake* ya kwanza ya wanafunzi wa pale Mtwara watakaoingia Chuo Kikuu. Mimi nashukuru kwa uamuzi huo wa busara uliofanywa na viongozi wa *Saint Augustine University*, na nashukuru pia Serikali yetu kwa kuwapa mazingira mazuri ya jambo hili kukamilika. Lakini niwaombe tuwape ushirikiano wa kutosha, tuwape misaada ya kutosha ili jambo hili lifanikiwe kwa mafanikio mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo tatizo la barabara. Kwetu barabara ya uchumi ni kutoka Mtwara -Tandahimba-Newala - Masasi. Barabara hii ndiyo inachangia uchumi wa Mkoa wa Mtwara na uchumi wa taifa. Asilimia Nne ya pato la taifa la nchi hii linatokana na pato la Korosho, ambazo korosho hizo zinapitishwa kwenye barabara hiyo niliyoitaja. Sasa *tonnage* ya korosho inayopita kule ni kubwa mno, huu ukarabati tunaoufanya huu wa kawaida hauisaidii, kila siku barabara ile tutaikarabati na itaendelea kuharibika. Kila mvua itakapokuwa inanyesha barabara inadai pesa, ombi langu tuiwekee lami ndiyo itakuwa suluhisho la mambo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Njwayo kengele ya pili.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nashukuru naunga mkono hoja. (*Makofî*)

**MHE. MCHUNGAJI LUCKSON MWANJALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nichukue nafasi hii, kukushukuru wewe kunipa nafasi hii, ya kuongea kwa mara yangu ya kwanza katika Bunge hili, hasa katika mfumo wa kuchangia, maswali nimewahi kuuliza lakini kuchangia ni mara yangu ya kwanza. Lakini, kwa sababu ni mara yangu ya kwanza, nilikuwa naomba niwashukuru wananchi wangu wa Mbeya Vijijini, ambao kwa kweli walinipa kura nyingi sana katika uchaguzi uliopita.

Pamoja na wanachi wa Mbeya Vijijini, lakini kipekee nawashukuru sana viongozi wangu wa Chama cha Mapinduzi, kutoka ngazi ya Shina mpaka Taifa. Walifanya kazi kubwa kuhakikisha kwamba, ushindi unapatikana na kwa kweli ushindi nilipata. Tatu niwashukuru ndugu zangu Wabunge wa Mkoa wa Mbeya, ambao kwa sehemu kubwa kwa kweli nao walichangia sana, walifanya kazi kubwa wakihakikisha kwamba, ushindi wa Chama cha Mapinduzi (CCM) kinaupata. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, na pamoja na kwamba, ni mara yangu ya kwanza, ninaomba niipongeze hotuba ya Rais, ambayo aliitoa pale katika ukumbi wa Kilimani. Hotuba ile ilikuwa ni nzuri, hotuba ambayo kwa kweli niliona kwamba, Mheshimiwa Rais, kwa kweli ana uchungu na wananchi wa Tanzania. (*Makofi*)

Pili ningependa kumshukuru, Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa hotuba yake nzuri pia ambayo kwa sehemu kubwa iligusa sana maisha ya mwananchi wa Tanzania. Iligusa kwa sababu alizungumza maeneo mengi ambayo karibu kila Mbunge anahusika au anaguswa kwayo na iunaonyesha wazi kwamba, kwa kweli Mheshimiwa Waziri Mkuu, anatembea pamoja na watu. Labda nitoe mfano mmoja tu. Kulikuwa na Nabii mmoja alikuwa anaitwa Ezekiel, akiwa huko nchi ya uhamisho Babeli huko, mpaka wakamwita ni mlinzi *yaani Watchaman Prophet* ) ametembea na watu mpaka ana angalia matatizo yao, na kwa hotuba ambayo Waziri Mkuu, aliisema hapa inaashiria wazi kuwa, huyu mtu ni kweli anatembea na sisi, amejitahidi kwa kila hatua kuhakikisha anatembelea kila maeneo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kipekee tena, niweze kuipongeza Serikali kwa kurudisha misamaha ya kodi kwa Mashirika ya dini, naamimi kama Mchungaji kwa upande mwagine nilikuwa na weza kuhusika. Kwa hiyo, nashukuru sana kwa serikali kuondoa tatizo hilo. Sasa naomba nichangie kidogo kwa yale ambayo ninayo. Kwanza, nilikuwa naomba nianze kwa kushukuru kwanza. Najua kulikuwa na maswali ambayo niliuliza hapa, hasa yaliyohusu maji, yaliyohusu umeme na namshukuru Kaka yangu, ndugu yangu Waziri wa Maji, Profesa Mwandosya, pamoja na Naibu wake, walinijibu vizuri sana na baada ya majibu yale nilipigiwa simu nyingi sana kutoka Mbeya vijijini. Wakinishukuru na wakimpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Maji, pamoja na Mheshimiwa Ngeleja. Lingine ambalo nilikuwa naomba kulizungumzia hapa ni kuhusu ule Mgodi wa Songwe. Mgodi ulikuwa unafanya kazi miaka ya nyuma kabla ya uhuru. Ni juzi juzi tu nilikuwa nimekutana na watu wanasema kwamba, walitoka huko Ikulu, na walitoka kwa Waziri wa Nishati, wakazungumza naye kwamba wangeweza kuufufua ule Mradi au Mgodi. Nilikuwa ninaiomba serikali kama kuna uwezekano, hawa watu wapewe nafasi hiyo ya kuuendeleza ule Mgodi, ambao una madini mengi sana. Madini ambayo ni adimu sana hapa duniani. Kwa hiyo nilikuwa naiomba serikali, itusaidie au isaidie kufufua ule mgodi, kwa kushirikiana na hao wawekezaji ambao nafikiri mmeishawasiliana nao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine ambalo nilikuwa nataka kuzungumza ni kuhusu fidia ya Wananchi wa Songwe. Kila wakati wamenipigia simu wakiomba msaada wa kufidiwa hela zao, kuna watu ambao maeneo yao yamechukuliwa mwaka 2007 mpaka leo hii bado hawajalipwa haki yao na wanahangaika ni vipi wataishi maisha kwa sababu hawajui waende wapi, hawana fidia yoyote na miaka inazidi kwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nilikuwa naomba Serikali ijaribu kuwafikiria tena hawa wananchi waweze kulipwa haki yao. Wako wananchi wale ambao walikuwa wamefidiwa, lakini ile fidia ina utata kidogo na bado wanaleta maswali mengi sana kwetu, na nilikuwa naomba labda utafiti wa uhakika ufanywe ili ijulikane ni vipi walilipwa na ni vipi wanaweza kulipwa tena, wale waliobaki. Kulikuwa na mapungufu

fulani, lakini hao wengine ni watu wa upande mwingine ambao wamechukuliwa maeneo yao juzi juzi tu na wangeliomba kwamba, wangelipwa hela zao ili wajue mahali gani wataelekea baada ya hapo, kwa hiyo ilikuwa ni sehemu hiyo. Lingine ambalo nilikuwa naomba nizungumze ni kuhusu shamba moja liko pale katika Kata ya Tembela, sehemu za Kemondo. Kulikuwa na shamba ambalo Wizara ya Kilimo, ilikuwa inashughulika nalo, wamenipigia simu jamaa wa kule, Wizara ya Kilimo ilikuwa inafanya utafiti wa Pareto. nafikiri pale sasa hili eneo limekaa bure na wananchi walifikiri kwamba, ingekuwa vizuri wangelipata maana kwa muda mrefu halijatumika tena na wananchi wana shida. Kwa hiyo, ingelikuwa vyema kama wangepewa waweze kujenga Zahanati pale. Kwa hiyo, nilikuwa naomba, Waziri anayehusika bila shaka atalipata, hasa Serikali kwa ujumla wake itanisaidia kuhakikisha kwamba, hawa wananchi wanaoomba eneo lile waweze kupewa.(*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine, niishukuru tena Serikali, hasa kwa malipo ya Kahawa, madeni ya mwaka 1995. Wananchi wale wamesubiri pesa hizo kwa muda mrefu, lakini juzi juzi tu, wakanipigia simu kwamba, wamepewa hizo pesa.

Lakini pia kuna mapungufu, nilikuwa ninaomba serikali ijaribu kutafiti, kwa sababu kuna watu wengi wameachwa na hawajalipwa na walikuwa kwenye orodha na sasa hawakulipwa hela. Kwa hiyo, nilikuwa naomba labda hapo tena paangaliwe kuhakikisha kwamba, hawa wananchi ambao wana kilio, kilio hicho waweze kupewa fedha hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado nina mengine ya kusema hasa kwa ajili ya zao la Pamba. Mbeya kulikuwa na sehemu ilikuwa inalima Pamba, hasa katika Kata ya Ikukwa na maeneo mengine ya Mshewe.

Kwa kweli ulimaji wa pamba katika maeneo yale ulisitishwa kwa miaka mingi iliyopita na ilisitishwa kwa misingi kwamba, kulikuwa na magonjwa fulani yameingia na wale wananchi wamesubiri kwa muda mrefu kupata jibu la kuwaeleza kwamba, je, wataendelea kulima au hawataendelea kulima? (*Makofi*)

Nilikuwa naomba kama utafiti umefanywa, kwa miaka hii, zaidi ya miaka 10, na ikaonekana kwamba, labda magonjwa hayo yametoka, kwanini wale wananchi wasiweze kuendelea kulima mashamba ya Pamba? Pamoja na kwamba, bei inazidi kupungua lakini ndiyo ilikuwa utamaduni wao, wanaofanya pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nilikuwa naomba nizungumze kidogo kuhusu Kata ya Ilungu katika jimbo langu. Kata hii ni wakulima wakubwa sana wa zao la viazi, viazi ambavyo vinasafirishwa mpaka Dar es Salaam na sehemu yao ile ya makao makuu ya Kata, wananchi wale ni kama huko nyuma walikuwa wameahidiwa kwamba, watapata umeme.

Lakini mpaka leo hii hawana umeme na waliishafunga nyaya katika nyumba zao. Nilikuwa ninaomba Serikali inapoendelea kutekeleza hii miradi basi iwakumbuke wananchi wa Kata ya Ilungu, Tembela na Inyala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini narudi nyuma tena kumshukuru Waziri wa Maji na Umwagiliaji na Waziri wa Nishati na Madini kwa ahadi zao ambazo kwa kweli walishaahidi hapa katika Bunge lako hili hili na nategemea kwamba kuanzia mwezi Septemba kutakuwa na mambo ambayo yataendelea kufanyika pale, kwa sababu wananchi wa Mbeya Vijijini wamesubiri umeme kwa miaka zaidi ya 10, wacha ya kwamba nguzo wanazonia zimesimama pale lakini umeme hakuna. Kwa hiyo naamini na ni tumaini langu kwamba Waziri anayehusika bila shaka hatasita kutekeleza mradi huu mkubwa ambao ulikuwa ni sehemu ya ahadi ya Serikali. Naomba sana hawa wananchi wa kutoka Kata ya Igale, Iyunga Mapinduzi, Isuto, Santilia, Ilembo na Iwiji wapewe umeme mwaka huu kama Waziri alivyosema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine la mwisho ambalo nilifikiri niongelee lilikuwa ni kuhusu barabara, ndugu yangu hapa mwingine aliyetangulia alisema kuna barabara zingine za kiuchumi. Barabara ya kutoka Makete kuja mpaka Isionje inaunganisha na Kata yangu ni barabara muhimu sana kwa ajili ya uchumi hasa katika Halmashauri yetu ya Mbeya Vijijini kwa sababu asilimia kubwa ya viazi vinalimwa katika maeneo yale. Nilikuwa naomba kwamba barabara ile ingelimwa iwekwe lami kwa sababu kuna milima pale na magari yale ya viazi ni mazito yanaharibu barabara kila wakati ikinyesha mvua.

Nilikuwa naomba kwamba Serikali itufikirie ikiwezekana iunganishe na Makete kuweka lami. Halafu tena ni mahali pazuri kwa sababu ndio mahali ambapo ni *National Park* ya Kitulo ipo. Lakini barabara nyingine ni kutoka Mbalizi kuelekea Ileje ni barabara muhimu sana kwa uchumi wa Mbeya. Ukipandisha kule mlimani siku moja mtu yoyote ambaye anataka afike kule mlimani Umalila sehemu za *plateau* ile utashangaa kulivyokuwa kuzuri na watu wanalima mahindi kwa wingi sana na ndio inalisha Mji wa Mbeya kwa sasa.

Naomba ile barabara ingetengenezwa kwa kupitika kwa mwaka mzima. Barabara nyingine kutoka Mbalizi kuelekea Mkwajuni ambazo ni barabara muhimu sana kwa uchumi wa Mbeya. Nilikuwa naomba Serikali itufikirie kutengeneza barabara hizo ambazo kwa kweli ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nisingetaka nigongewe kengele mapema nasema naunga hoja mkono, ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. AL-SHYMAA JOHN KWEGYIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya na uzima kuweza kusimama mbele ya Bunge hili, nashukuru sana. Naomba nianze kwa pongezi na shukrani. Nianze kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Celina Kombani na Naibu Waziri Mheshimiwa Aggrey Mwanri na watendaji wote wa Wizara ya TAMISEMI na Waziri Mkuu nawapongezeni sana kwa hotuba zote mbili zilikuwa ni nzuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa shukrani nyingi za dhati zaidi kwa Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuwa msitari wa mbele kwenye janga lililokuwa janga kubwa sana la Kitaifa la mauaji ya albino. Kwa kweli viongozi hawa wamekuwa msitari wa mbele mno, walikuwa ni majemadari wameongoza hili suala hadi kufikia kura za maoni na sasa hivi kesi zipo Mahakamani. Tunashukuru sana juhudzi za Serikali ya Chama cha Mapinduzi, kesi ziko Mahakamani na tunasubiri matokeo yake *inshallah* Mwenyezi Mungu atajalia. (*Amin*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi zangu nyingine napenda kumpongeza Waziri Mkuu. Waziri Mkuu alikuwa na ziara mikoa 4 ya Kanda ya Ziwa na mimi nilishirikishwa kwenye ziara hiyo, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kunishirikisha kwa kweli ile ziara ilikuwa na *impact* kubwa sana kwa sababu tumezunguka kule na ziara ile ilikuwa nia na madhumuni ni katika kupambana na hili janga la mauaji ya albino, pale ndipo nilipoweza kumfahamu vizuri Mheshimiwa Waziri Mkuu. Ni hodari, mchapakazi, hachoki kwa kweli mtu huyu achagui na wala abagui. Tulipofika Chato Mheshimiwa Waziri alidiriki kumchukua mtoto George, huyu mtoto ni mtoto wa albino. Mheshimiwa Waziri Mkuu alimchukua huyu mtoto kumlea kitendo hicho tu kinaonyesha imani yake na yule mtoto anaye mpaka hii leo na jana Mheshimiwa Waziri Mkuu ameniambia George yupo Dodoma. Sasa hii unaona kwamba imani yake sio yaku-*act* ni imani ya kweli, anamchukulia mtoto George ni mtoto wake wa kumzaa yeze mwenyewe. Nakupongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa moyo huo, Mwenyezi Mungu akujalie. (*Amin*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Celina Kombani nilikwenda naye ziarani Mkao wa Mara alinipa ushirikiano mkubwa sana. Nimefika Mkao wa Mara heshima niliyopewa kule na mkoaa ule kwa kweli siwezi kusahau, nampongeza sana Mkuu wa Mkao wa Mara aliyekuwa wakati huo Mheshimiwa Issa Machibya alinipa heshima kubwa sana na nilitembelea vijijini nilimaliza vijiji vya Mara nilikwenda Bunda, Tarime, nimefika kwenye vijiji ndani (*in deep*) vijijini huko nimepitaa na nimekutana na watu wenye ulemavu wa ngozi kule wana hali ngumu. Nimekuta kule kuna familia moja wote familia nzima ni albino wanaishi kwa Katibu Kata kwa kweli linaniuma sana lakini namshukuru Mheshimiwa Mkono amekubali kuwajengea nyumba ile familia amekubali kabisa na amesema atawajengea namshukuru sana sana kwa kujali familia ile kwa sababu wana hali ngumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado naendelea na shukrani na pongezi. Shukrani nyingine naipongeza Kamati ya *SCOUT* ya Bunge inayoongozwa na Mheshimiwa Abdulkarim Shah. Kamati hii kwa kweli wana moyo wamediriki kuwa pamoja na sisi na mpaka leo nina salamu zao nyingi kutoka kwa vijana, akinamama, watoto wanaifahamu kuwa Kamati hii ilifanya kazi kubwa. Pia nawashukuru Wabunge wote wa Bunge hili kwa ushirikiano wenu kwa sababu na nyinyi kwenye Majimbo yenu mmeshiriki katika tatizo hili. Kwa njia moja au nyingine mmeshiriki nashukuru sana. Nashukuru vyombo vya habari, TV, magazeti wametoa elimu kubwa kwa jamii mpaka hivi sasa watu wamebadilika wakimwona mtu mwenye ulemavu wanaona ni kitu cha kawaida, wanamwona ni mwenzao hakuna ubaguzi hata watoto shulenii wamekuwa na mapenzi makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi binafsi kuna watoto wawili nimewachukua ambao ni albino, mmoja alikatwa mguu, nimewachukua wamekuwa ni watoto wangu kama wa kuzaa mwenyewe wanavyonichukulia. Nimewapeleka shulenii, watoto pale wana mapenzi makubwa nao, ile ni mabadiliko makubwa kwa sababu hapo zamani wangenyanyapaliwa wale watoto. Lakini sasa hivi wanalelewa kwa mapenzi makubwa kwenye ile shule na wale watoto waliokuwa nao pale wanawapa mapenzi makubwa kabisa. Nawashukuru Watanzania wote, wadau mbalimbali kwa kuwa karibu katika hili jambo ambalo linaendelea na kesi ziko Mahakamani, namshukuru sana. Lakini yote haya ni juhudii ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi (CCM). (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze mchango wangu kwanza kabisa naomba nilenge kwa masuala ya sensa, *survey* nashukuru imefanyika Mheshimiwa Waziri Mkuu alizungumza kwamba sensa imefanyika, lakini sensa hii inahitaji mikakati iboreshwe. Mikakati iboreshwe kinachotakiwa ni *Participatory Methodology* kwa sababu inatakiwa kwenye ile *survey* wale watu wenyewe ulemavu wenyewe washirikishwe kwenye lile jambo, washirikishwe kwa maana kwamba wao wanafahamiana nyumba hadi nyumba nani yupo nyumba hii, nani yupo nyumba ile wanafahamiana. Kwa hiyo, wakishirikishwa inaleta *impact* nzuri kwa sababu ile takwimu inakuwa ya uhakika sio ile ya kukadiria, inakuwa ni takwimu ya uhakika kabisa. Kwa hiyo, hilo ndilo ombi langu kwamba watu wenyewe ulemavu washirikishwe wakifika kwenye mikoa kuna Shirikisho la watu wenyewe ulemavu, kuna vyama vya watu wenyewe ulemavu wawashirikishe katika ile *survey*, nafikiri itakuwa na *impact* nzuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa pili nitazungumzia uwakilishi na naiomba Serikali waongeze watu wenyewe ulemavu washirikishwe kwenye maamuzi mbalimbali, Serikalini. Nashukuru Bungeni sasa hivi kuna hali nzuri na nategemea kwamba itazidi kuwa nzuri, lakini kwenye maamuzi mengine tunaomba na watu wenyewe ulemavu washirikishwe katika maamuzi mbalimbali ili wigo upanuliwe zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu mwagine unagusa kwenye bajeti ijayo. Mwenyezi Mungu akijalia bajeti ijayo tunaomba Serikali waongeze ile *fund* kwa ajili ya watu wenyewe ulemavu. *Fund* inayotoka ni ndogo, mwaka 2007/2008 kila *society* ilipewa shilingi 2,500,000. Mwaka 2008/2009 walipewa shilingi 2,000,000/= hazitoshi. Nitembelea mikoani kwenye yale Mashirikisho wanalamika wanasesma Mheshimiwa tunasikia kuna fedha zinatoka lakini hatujawahi hata kuiona hiyo fedha tunaisikia tu.

Kwa hiyo haitoshi ni ndogo sana wataigawanya vipi. Kwa hiyo nasema hapa Mheshimiwa Waziri Mkuu ananisikia tunaomba ombi letu ni hilo kile kiwango kiongezwe kidogo ni kidogo mno, tunaomba angalau kiongezwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa elimu kuna tatizo la masuala ya miundombinu hazikidhi haja kwa masuala ya watu wenyewe ulemavu. Miundombinu bado ni tatizo, walimu wenyewe elimu maalum ya kufundisha watu wenyewe ulemavu bado ni wachache, juzi juzi tulikuwa pale Miiji palikuwa na Sherehe ya Siku ya Mtoto lalamiko lilikuwa ni hilo mojawapo la walimu wa elimu maalum ni tatizo. Nakumbuka bajeti

iliyopita nilichangia kwenye Wizara ya Elimu nilimwomba Waziri wa Elimu katika ziara zake anishirikishwe, japo ziara mbili au moja tuwe pamoja nipaye kuona jinsi hali halisi hasa kwa watoto wenye ulemavu wa ngozi. Unajua tatizo kubwa kwa albino ni *vision*, tatizo la kuona, ni tatizo kubwa sana, kwa hiyo wengi wana-*give up* wanaona kwamba siwezi kuendelea, anaona kwamba darasani sioni, nikifika mle nitaambwa hivi, nitaambwa hivi anakata tamaa. Kwa hiyo, ninahitaji mwalimu anayefundisha watoto wa aina hiyo awe na imani ya hali ya juu na uvumilivu mkubwa. Inahitajiwa moyo sana kufundisha watoto wa aina hiyo, ndiyo maana nilimwomba Mheshimiwa Waziri wa Elimu japo ziara moja, mbili na mimi nishirikisheni wakaniahidi. Lakini tumemaliza mpaka tuko kwenye Bajeti hii. Nawaombeni mnishirikishe kwenye hizo ziara mnazotembelea kwenye mashule na mimi nione, nitatoa mchango wangu pia unawezza ukasaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la afya. Nilimwomba Mheshimiwa Waziri wa Afya kwamba suala la dawa zile za *Sun Skin* kwa ajili ya kukinga jua zitolewe bure, gharama yake ni kubwa mno. Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii Prof. Mwakyusa analijua hilo nililizungumza bado naendelea kuomba tena zile dawa ni ghali wengi wao ni *dhofrihali* hawana kitu, hawawezi kununua zile dawa. Kwa hiyo tunaomba Serikali zile dawa zitolewe bure kwa sababu bei yake ni kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa naomba nimalizie kwenye kitabu cha hotuba ya Waziri Mkuu ukurasa wa 41 na 42 kuna masuala ya viwanja vya ndege. Mimi ni mdau wa viwanja vya ndege sidhani kama kuna Mheshimiwa Mbunge asiyefahamu mimi ni mdau kule, nyote mnanifahamu asilimia sijui niseme 90 mnanifahamu kwamba mimi ni mdau. Naipongeza sana Serikali kwa uboreshaji niliouona umeleewa humu na maboresho haya ya mitambo nimesoma humu kwa kweli naifurahishwa sana kwa sababu mimi mdau pale. Lingine nampongeza Mheshimiwa Dr. Shukuru Kawambwa kuna tatizo nilimpelekea kuhusiana na wafanyakazi wa Viwanja vya Ndege. Hilo tatizo nashukuru limefanyika nusu bado nusu halijafanyika lakini nashukuru Mheshimiwa Kawambwa nimeshamfikishia na nina imani kabla ya mwezi huu wa Juni kwisha lile tatizo litakuwa limekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine kwa wafanyakazi hawa wa Viwanja vya Ndege ni vyeo. Kuna watu wana miaka mingi pale hawajapanda vyeo tunaomba Mheshimiwa Waziri hilo pia uli-*note* kwamba wamewijibika pale muda mrefu, vyeo hawajapata. Kuna wengine wanakuja juzi wanapata vyeo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri Kawambwa naomba hilo. Naomba niwashukuru sana, pamoja na shukrani zangu naomba ntilie msisitizo suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, nashukuru sana, na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, nakushukuru sana Mheshimiwa Al-Shymaa Kwegyir, Mbunge wa Kuteuliwa na mimi kwa niaba ya Waheshimiwa Wabunge wote tumpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kumlea mtoto George. (*Makofi*)

Nilisema kwamba atafuata Mheshimiwa Charles Mwera, baada ya hapo atafuata Mheshimiwa Christopher Ole- Sendeka na Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir aendelee kujiandaa.

**MHE. CHARLES N. MWERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii nami nichangie hii hotuba ya Waziri Mkuu. Kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi hii na nikupongeze kwamba vazi lako hilo limekupendeza sana na huyo fundi anastahili sifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kukushukuru hotuba ya Waziri Mkuu pamoja na wasaidizi wake kwa kweli zilikuwa na hotuba nzuri na ndio hasa tunaanza kujadili.

Pili nimshukuru Mkuu wa Mkoa ambaye amepangiwa mkoani kwetu Mheshimiwa Kanali Mfuru nimwahidi kwamba tutashirikiana katika kutetea wananchi wa Mara, tulikuwa na kikao cha muhimu jana usiku chini ya Mheshimiwa Prof. Sarungi na tulifanya kikao kizuri kwamba tunataka tushirikiane. Nimshukuru na nimkaribishe kwamba tutashirikiana kwenye kazi ambazo ziko mbele yetu. (*Makofi*)

Vile vile nimshukuru aliyejewa Mkuu wa Mkoa wa Mara Machibya tumefanya naye kazi kwa kweli kwa muda mrefu na kule alikokwenda basi afanye kazi ambazo ni nzuri ili afanye uwakilishi mzuri. Nimshukuru sana aliyejewa *DC* wangu pale Tarime Stanley Kolimba tumeshirikiana naye kwa kufanya kazi kubwa na kwa niaba ya wananchi wa Tarime nichukue nafasi hii kumpa pole sana alifiwa na mke wake *inshallah* hayo ndio mambo ya kidunia na napenda nichukue nafasi hiyo kumpa pole sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwashukuru kwanza Waheshimiwa Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Tarime ambayo mimi ni Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo tumefanya kazi kubwa sana kwa kushirikiana na Madiwani pamoja na Mkurugenzi na Watendaji wote wakiongozwa na Mkurugenzi Kagenzi kwa kweli tumefanya kazi kubwa.

Nafikiri kila Mbunge alipokuwa akisimama hapa anaelezea mambo ya shule na sisi mashule tumejenga, niwapongeze sana wananchi wa jimbo langu kwa ushirikiano mkubwa ambao tumekuwa nao tumefanya maendeleo makubwa katika mashule na mjue kwamba kwa kila Kata tuna shule zingine kwa mfano ya Nyarero ina shule 3 na Kata zingine zina shule mbili.

Kwa hiyo niwashukuru sana wananchi na niwaahidi kwamba tutashirikiana. Ni mara yangu ya kwanza kuhutubia au kuongea katika bajeti napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru sana wananchi wangu wa Tarime kwa kazi kubwa mliyofanya kwa kunichagua kuwa mwakilishi wenu mnafahamu kazi iliyofanyika pale sisi tulikuwa na helikopta moja na CCM ilikuwa na helikopta mbili lakini tuliwashinda, nawashukuru

sana wananchi wa Tarime. Kazi kubwa iliyofanyika pale ni kazi ya kuonyesha kwamba mna imani kubwa na mimi, mna imani kubwa na chama cha CHADEMA niwaahidi kwamba nitawawakilisheni vizuri. Niwashukuru viongozi wangu wa Chama Freeman Mbewe, Katibu wangu wa Chama Dr. Willibrod Slaa na Naibu Katibu Mheshimiwa Kabwe Zitto. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuchangia nianzie upande wa elimu. Elimu ndio kitu cha msingi na mambo yote tunaweza tukayaongea mengi lakini kama huna elimu watoto wetu hatuwapi elimu hatuwezi tukasema kwamba tunaweza kukapeleka maendeleo kwa wananchi. Kwa upande wangu ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Tarime nikwambie kwamba kwa mwaka huu tulitenga shilingi 140,000,000 na tumewalipia watoto karo kwa ajili ya watoto wote wa shule katika Shule ya Sekondari kwenye Shule za Kata. Kazi hiyo tumekuwa tukiisimamia na nitumie Bunge lako Tukufu niwaambie wananchi pamoja na Madiwani na watendaji kwamba hizo fedha zitumike vizuri na tuhakikishe kwamba watoto wamelipiwa karo na niwaombe Waheshimiwa Madiwani, Waheshimiwa Wabunge upande wa Chama cha Mapinduzi na upande wa Upinzani tunahitaji wanafunzi wetu wasome.

Shule hizi tumekuwa tukizijenga sisi wazazi lakini mjiulize wakati umefika wananchi wetu ambao ni wakulima wengine ni wafugaji wamefanya michango mikubwa wametoa ng'ombe lakini ujiulize inakuwaje mtoto anapokuwa anakwenda pale shulenii anarudishwa kwamba hana karo wakati yeye ndio aliyojenga pale. Wakati umefika tuseme kwamba Taifa lina uwezo, tuna rasilimali nyingi, tuna madini, mbuga zetu zipo tutoe maazimio tuungane kwamba elimu ya sekondari Taifa liweze kugharamia karo ya wanafunzi Tanzania nzima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiongelea kwenye upande wa elimu kwenye shule zetu za Kata ambazo tumezijenga ambazo nichukue nafasi hii kuwapongeza Watanzania wote walioshiriki katika ujenzi huu wa shule hizo. Lakini tuijulize Waheshimiwa Wabunge, Waheshimiwa Mawaziri, Wakurugenzi Wakuu wa Idara ni mtoto gani wa Waziri, mtoto gani wa Mbunge anayesoma katika shule hizo, kila mtu amekuwa akiongea hapa anapongeza shule tumejenga lakini shule hazina walimu. Mambo ya kujenga jambo lingine tunahitaji tuwapeleke walimu katika mashule hayo tuweze kuhakikisha kwamba watoto wanasoma. Tunaweza kuwa na mashule mengi lakini kama hatuna walimu hatuwezi tukafanya kitu chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ningetaka tueleze kwamba nchi yetu pengine haina walimu. Tumekuwa tukiongea sana kuhusu wakulima na tunaongelea sana mambo ya muhimu sana lakini hatujaangalia wafanyakazi, je, mshahara wao unakuwaje.

Kwa hiyo tuiagize Serikali maana kila Mbunge anapokuwa anazungumza anaomba Serikali, Serikali ni wajibu wake iwajibike kwa wananchi wake. Ni kuiagiza Serikali kwamba wafanyakazi walipwe mshahara wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine tuna upungufu mkubwa wa walimu kwa ajili ya shule zetu, tutafanyaje sasa walimu wawepo. Sasa hivi tunakwenda kwenye zoezi la

kuingia kwenye JKT, JKT utakwenda utatumia miaka 2 mwalimu atakwenda miaka 2 je, hii nafasi ya kujaza wataingiaje hawa walimu ili waweze kuingia katika ualimu. Nchi ya Kenya sisi tumewahi kuwatangulia katika kupata uhuru, Tanzania tusione aibu twende Kenya tuwaombe walimu waje waajiriwe hapa watufanyie kazi, Kenya walimu wamejaa watusaidie katika kufanya kazi hiyo tusione aibu. Tulikaa muda mrefu tangu tumepata uhuru kama hatukuweza kufanya zoezi namna gani nchi iendelee hatuwezi tukawa tumekaa tu kwenye shule zetu za Kata. Ukienda kwenye Wilaya yangu ukichukua kwa mfano shule ya Nyanungu uende Mwema, Pemba unakuta kuna walimu wawili, hawa walimu wawili watafanyaje kazi shuleni pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye shule zetu za Kata watoto wanasona, ndio wanamaliza Kidato cha Nne, lakini katika kumaliza Kidato cha Nne unakuta kwamba hakuna mwanafunzi yoyote aliyefaulu pale, wazazi wanashindwa hata kuchangia maendeleo pale. (*Makofî*)

Kwa hiyo lazima tulione hili na Taifa ni lazima liangalie tunapokuwa tumepungukiwa na kitu basi tuombe jirani zetu. Sasa hivi tunaingia katika *East African Community* tuwaombe hata kama ni ndugu zetu wa Uganda mbona tuliwasaidia vita vyatya Kagera tuwaombe walimu waje kutusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee suala la maji. Kuna tatizo la maji katika mji wa Tarime ambao imekuwa ni shida kubwa. Mji wa Tarime aliyekuwa Rais kwa awamu ya pili, Mheshimiwa Mkapa alikuja pale Tarime akaahidi kwamba maji yangeweza kupatikana wakati anaomba kura, Rais wetu Kikwete amekuja pale akaahidi wananchi wangu kwamba mkinichagua nitawaleteeni maji.

Tumemchagua sasa tunahitaji maji pale mjini, maji yaje pale Tarime na kwa bahati nzuri tumeshajenga tanki la maji, nilikuwa naongea na Waziri wa Maji wananchi wa pale wanahitaji shilingi 30,000,000 za fidia na nafikiri hilo Waziri utoalitekeleza ili maji yaweze kufika Tarime Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siwezi nikaacha kuongelea sehemu ya madini kwa sababu mimi ninatoka huko. Nikitoka hapa bila ya kuongelea mambo ya madini Waheshimiwa Wabunge wa Geita mnawenza mkanishangaa sana na Watanzania.

Nchi yetu imeingia kwenye mikataba ambayo sio mizuri tumekuwa na uadui mkubwa na wawekezaji, mimi wakati mwininge huwa nakaa ninapokuwa na mikutano na wawekezaji ninawaambia kwamba hii hali ya madini inakuwaje. Mambo ya madini tumeingia mikataba ambayo sio mizuri lakini namna gani wale wananchi wako pale wanafaidi kwenye ile migodi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wanahitaji wapewe fidia kwa mfano Mheshimiwa ambaye ni Diwani ambao uwanja wa ndege umejengwa kwenye eneo lake anadai karibu ya shilingi bilioni moja.

Wananchi wanaumia pale hawajalipwa fidia zao, wachimbaji wadogo Waziri anayehusika tunaomba kwamba wapewe sehemu ya kuchimba wachimbaji wadogo.

Hali ya mazingira pale kwenye mgodi, nimeangalia kwenye vyombo vya habari hali ni mbaya, tulikuwa tukisema kwamba maji yanaingia ndani ya Mto Tigite pale wananchi wameumia sana. Ndio maana nilikuwa nauliza kwenye swali langu kwamba itakuwaje wananchi wale muda mwingine tumeongea sana. Ndani ya Halmashauri niliongea sana tukaenda pale na Waheshimiwa Madiwani lakini unapokuwa unauliza wanasema kwamba yale maji hayana kemikali. Kwa hiyo tunaomba Serikali iliangalie hilo na tuhakikishe kwamba wananchi wetu wanaumia na m aji machafu yenyemikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo ya vita ambavyo viko pale ndani ya Wilaya yangu, vita vya koo ambavyo kwa kweli tumefanya juhudi kubwa, Waziri wa Mambo ya Ndani nimpongeze kwamba alikuja pale tukakaa tukaliongelea hilo, lakini kitu cha msingi ambacho ningeongea ni kwamba viongozi wanapokuja wakija ndani ya Halmashauri pale wao hawaendi kwenye sehemu za matukio tunakuwa ndani ya Ofisi, ndani ya Halmashauri ambayo haisaidii kitu, tunatakiwa twende sehemu zile ambazo zinahusika.

Kwenye suala hili kumetokea na kundi dogo ambalo limehusika la ujambazi ambao nilikuwa naomba Waziri Mkuu naomba kwanza unisikilize kwa makini kuna kundi dogo ambalo linashirikiana na Wakenya lina silaha kubwa sana ambazo zinatoka kwenye vita wanakuja wanavamia ng'ombe wanaua jamaa zangu wanakwenda nazo ng'ombe Kenya. Serikali ituambie watu wa Tarime Je, sisi ni Watanzania au ni Wakenya na kama wameshindwa kulinda watupe bunduki tulinde watu wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wamekuwa wakipigwa pale risasi na ng'ombe zinakwenda Kenya, watu wengi wameuawa, Serikali hailindi mipaka, mipaka yetu iko wazi ng'ombe zinachukuliwa zinakwenda Kenya. Lile kundi limekuwepo kundi dogo na wakati mwingine wanatumia silaha ambazo ni kubwa sana kama K47, askari wanakwenda wanapigana mara nyingi wanashindwa.

Mchana wanapiba ng'ombe wanaswaga ng'ombe nikiuliza wanajibu Mbunge hatuna gari wakati mwingine wanasema silaha hazitoshi, hawana silaha za kuweza kupambana na hawa majambazi.

Kwa hiyo, nimwombe Waziri Mkuu kwa kweli mambo ya ulinzi pale yaweze kuimarika ili wananchi wangu waweze kukaa na amani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vituo vya Nyamwaga, Borega, Nyantira, Kegonga maaskari waongezwe pale ili kuhakikisha kwamba wananchi wanalindwa. Mpaka huu tumekuwa tukiuangalia kati ya Kenya na Tanzania, wakati mwingine mnawenza kuona kwamba Mwenyekiti ni kitu cha kawaida, wakati mwingine tulikuwa tukiongelea mambo

ya kemikali ambayo imekuwa ikiingilia kwenye Mto Mara, Serikali inaona kama sio kitu ambacho kipo.

Lakini kwenye mpaka ambao tuko Kenya na Tanzania Serikali isipoingilia kati kuna siku moja itatokea vita base ya Kenya na Tanzania. Ni lazima tulinde mipaka yetu na wakati unafika maaskari wa Kenya wanatoka Kenya wanavamia Tanzania na Serikali ipo inaliangalia hilo, kwa hiyo nimwombe Waziri Mkuu kwenye hili suala la Tarime lihakikishe kwamba mipaka inalindwa, maaskari waje pale.

Serikali iliahidi kwamba tutakuwa na Kanda Maalum ya Polisi basi waje watekeleze majukumu kwa ajili ya kuhakikisha kwamba amani inapatikana. Kingine cha msingi pale Tarime kumekuwa na *barrier* ya njiani ya vyakula, chakula kinatoka kutoka Mwanza kikifika pale *barrier* imewekwa karibu na Mto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Charles Mwera Mbunge wa Tarime, kama nilivyosema atafuatia Mheshimiwa Christopher Ole Sendeka Mbunge wa Simanjiro baada ya hapo Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, Mheshimiwa Ali Khamis Seif ajipange, Mheshimiwa Ruth Msafiri akae sawa.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ninapenda kuchukua nafasi hii, kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Simanjiro, kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba hii ya kihistoria ya Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo kwa hakika, kila aliyeisikiliza, atakiri kwamba ni hotuba ya viwango lakini iliyozingatia hali halisi ya taifa letu na ambayo kwa kweli imegusa kila eneo muhimu katika sekta zote katika nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuwasilisha kilio. Kama nyote mnavyojua, mwaka huu ni mwaka wa ukame kwa nchi yetu yote lakini katika nyanda zile kame ambazo mnaziita *semi-arid land*, hali imekua mbaya zaidi. Kwa Wilaya kama ya Simanjiro, Longido, Kiteto, Ngorongoro, Mondoli na nyinginezo, hali yetu si shwari kutokana na hali ya hewa ambayo kwa miaka hii mfululizo haikua nzuri kabisa lakini mwaka huu imekua mbaya zaidi. Ukame huu sio tu kwamba umepelekeea kukosa malisho ya mifugo lakini na chakula pia. Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, atutizame kwa jicho linalostahili la huruma kwa upande wa wafugaji, mifugo yetu na wakazi wengine walioko katika Wilaya zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mji mdogo kama wa Mererani ambao mnaujua ni marufu kwa madini ya Tanzanite, hali yetu ni mbaya na pia kutokana hasa na mtikisiko wa kiuchumi ambao umeathiri sekta zote kama alivyosema Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano. Kwa hiyo, hali ya kipato kwa wale wachimbaji ni mbaya na hasa kwa upande wa chakula watizamwe kwa jicho la huruma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina haja ya kurudia kauli iliyozungumzwa na Waziri Mkuu leo kufuatia swali la Mheshimiwa Selelii kuhusu wafugaji, ila ninachotaka kusema

ni kumwomba sana vile vitendo ambavyo vilifanyika kinyume na maadili ya Taifa letu vya kuwadburumu wafugaji, kupora mali zao na kuwafanya wengine sasa washindwe kupeleka watoto wao shule, kama wale wafugaji wa Kilosa, basi utekelezaji wa Kamati hiyo sasa ufanyiwe kazi kwa haraka sana ili watu hawa waweze kupata haki ikiwa ni pamoja na watoto kwenda shule kama ilivyo stahiki kwa Watanzania wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimwombe Mheshimiwa Waziri Mkuu, kama kiongozi mwenye madaraka ya juu katika udhibiti, usimamiaji na utekelezaji wa mambo yote katika Jamhuri yetu, katika mambo haya aongeze ukali kabisa ili haki iweze kutendeka ili watu hawa wajisikie kwamba ni Watanzania sawasawa na Watanzania wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa mwizi wa fadhila kwa kweli kama sitachukua nafasi hii kama sitatambua uelewa na *commitment* ya Waziri wetu Mkuu, wa hali halisi tuliyonayo. Yeye ni shahidi katika suala la kero ya maji pale Orekesmet na Waziri wake wa Maji ni shahidi na mimi nawapongeza sana kwa hatua za awali walizoanza kuzichukua. Nimefarijika sana pamoja na kero hiyo walau tumepata shilingi milioni 200 ambazo zitakwenda kuhangaika pale kuchimba visima katika kijiji cha Orekesmet, Endojingijape na Roromojio katika Kata ya Orekesmet na ambapo ndipo Makao Makuu ya Wilaya kwa nia ya kupunguza adha na kero ambayo imepelekea mifugo mingi ya Wilaya yetu na hasa katika eneo hilo na Tarafa zingine nne kulazimika kuondoka katika Wilaya yetu ya Simanjiro kwenda katika Wilaya za jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee, napenda sana kuupongeza uongozi wa Mkoa wa Tanga na hasa Wilaya ya Kilindi kwa kukubali mifugo ambayo imehamia pale katika janga hili iweze kupata malisho katika maeneo hayo lakini mifugo ya Longido sasa hivi haiko Longido. Kimsingi, mifugo ya Longido na mifugo ya Mondoli kwa sehemu kubwa nayo imehama maeneo yao kutokana na ukame. Napenda Serikali ikae na kutafakari jambo hili kwa uzito unaostahili ili Watanzania wasirudi katika ufukara ambao walikwisha ondokana nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumza hilo la kilio na hasa nikitambua jitihada za pamoja za Waziri Mkuu na Waziri wa Maji Mheshimiwa Prof. Mwandoza na Mheshimiwa Mwangunga ambaye kwa siku mbili amekua akihangaikia kuweza kutusaidia, niruhusu sasa nielekee maeneo mengine ambayo kwa kweli ningependa pia kuyatendea haki.

Mheshimiwa Menyekiti, maendeleo yenye uwiano, ni msingi wa umoja, amani na mshikamano wa dhati katika taifa lolote. Nasema haya kwa sababu iwapo ugawaji wa rasilimali katika nchi zitaelekezwa kuzisaidia jamii zile ambazo ziko nyuma katika huduma za jamii, itawafanya wale waweze kuinuka na kuweza kumudu ushindani na maendeleo yenye uwiano yanaweza kupatikana na itakua ndiyo msingi wa umoja na amani katika nchi yetu. Napenda rasilimali zetu, tunapopitisha bajeti za nchi yetu, tutizame kwamba ni maeneo gani yanayohitaji zaidi msaada. Kwa mfano, katika Wilaya zetu za wafugaji, mnajua dhahiri jiografia inatuweka mahali pagumu. Shule za Kata

tulizojenga zinahitaji mabweni, zinahitaji nyumba za Walimu kama ilivyo katika maeneo mengine. Tunahitaji upendeleo katika hili na ni upendeleo wa haki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, umbali kati ya kijiji na kijiji kwetu ni kilometra 50 hadi 70. Unapojenga Sekondari ya Kata kama maelekezo ya Ilani yalivyo, unahitaji watoto hawa waweze kufika shuleni na namna pekee ya kuwafanya waweze kupata elimu hiyo ni kuwajengea mabweni na kuwajengea nyumba za Walimua ili waweze kutoa huduma hiyo. Kwa maana hiyo basi, namwomba Waziri wa Elimu pamoja na Waziri Mkuu, waone namna bora ya kuweza kutusaidia kupata nyumba za Walimu na mabweni katika shule hizi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kidogo kugusia hili ambalo wenzetu wamekua wakizungumza sana la utekelezaji wa Ilani. Hivi kweli mtu mzima mwenye akili timamu, kwa miaka mitatu na nusu ya uongozi wa Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete, akiwa na timu ya Mawaziri shupavu kama hawa waliopo wakiongozwa na Mheshimiwa Pinda na akiwa na timu ya Wakuu wa Mikoa waliopo hapo juu, mnaowaona na Makatibu Wakuu wa Wizara na Wakurugenzi Watendaji wa Mikoa na Wilaya, hivi kweli Serikali inayosimamiwa na Bunge hili la viwango, mkisema kwamba hajatekeleza Ilani, unahitaji kuwa na sifa zifuatazo. Moja, unahitaji kuikana nafsi yako kwa nia tu ambayo wewe unaipenda, kwa utashi wako mwenyewe kwa kukataa kusema ukweli lakini nyingine ambayo siamini sana kama inaweza kupatikana Dodoma, unahitaji kuwa na upungufu wa akili, lakini hili haliwezi kupatikana hapa kwa sababu Mirembe iko karibu, kwa hiyo, tiba yake inapatikana bure. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais Jakaya Mrisho Kikwete amefanya kazi inayostahili kupongezwa, mimi katika Ilani hii ya uchaguzi, niliamrishwa na Ilani nihakikishe kila Kata ina Sekondari. Tulianza pale alipoachia Mzee Mkapa na mimi nilianzia pale alipoachia Mzee wangu Kone, Mkuu wa Mkao wa Singida. Aliniachia Sekondari tatu leo ninazo 16. Nikisema kidumu Chama cha Mapinduzi katika hili, hakuna anayekataa. Nikisema Mheshimiwa Jakaya anafanya kazi nzuri, leo nenda katika vijijiji vile, nina Kata 15 na nina Sekondari 16. Mimi nimejenga 13 na zimeshaanza nimebaki na moja ya Kata ya Kitwai niwe na 17 nimalize kazi. Anayetaka kuja aje maana Waswahili wanasema kanzu ya Ijumaa hufuliwa Alhamis, nami nimeshaifua, nimeipiga pasi, watatuchagua tu. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usipingika kwamba tulipochaguliwa, Wilaya ya Simanjiro ilikuwa haina umeme. Lakini chini ya uongozi wa Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, chini ya Waziri wa sasa wa Nishati na Madini na chini ya Waziri Mkuu wa sasa na wa zamani, Mheshimiwa Edward Lowassa, jitihada zile zimeendelea leo tunawasha umeme Orkesmet, Ngage na tunatarajia kuwasha Msitu wa Tembo. Hivi katika hili, watakataa kwamba Ilani ya uchaguzi hajatekelezwa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya lami kutoka KIA kuja Mererani, imepandishwa hadhi, kwa mwaka huu imetengewa fedha kidogo, nimemwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, anong'one na Waziri wa Miundombinu, ili ahadi ya

Mheshimiwa Mkapa na Mheshimiwa Rais Kikwete ziweze kutimia. Baada ya kufanya hivyo, watakosa agenda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona niyasema haya kwa sababu ni mambo ya msingi na mimi nawashangaa sana watu ambao wanaweza kusema kwamba hatutatekeleza Ilani ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko jambo moja ambalo si vema sana kusikika katika masikio ya Watanzania kwa sasa. Ni jambo ambalo tumekuwa tukizungumza kwa miaka mitatu hii na nusu na huu ni mwaka wa nne, nalo ni kuitaka Serikali ichukue hatua za makusudi na za haraka, kufunga agenda inayoitwa ya ufisadi. Si jambo jema sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu Waislam katika hadithi za Mtume Mohammed S.W.A., zinasema:-

*“Ukiwa na jambo linalokukera, unaloamini jambo hili ni kero, chukua hatua za kuliondosha jambo hilo na kama huwezi, lisitakie jambo hilo kwa mtu mwenye uwezo na kama hajaweza kuliondoa, endelea kuonyesha hasira kwa kunyooshea vidole jambo hilo ovu ili hatimaye liweze kuondolewa”.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufisadi ni jambo ambalo linanikera mimi na linakikera Chama changu. Baba wa Taifa Mwl. Julius Kambarage Nyerere katika moja ya hotuba yake aliyoitoa Februari 18, 1992 wakati wa kuasisi mfumo wa vyama vingi vya siasa alisema maneno haya akitaka Chama chetu kijipambanue na kujitenganisha na watu waovu, naomba kunukuu:-

*“CCM iking’ang’ania umoja wa bandia na watu wasio na maadili, itanunua umoja huo kwa kupoteza itikadi yake. CCM isiyo na jadi na msimamo katika mambo ya msingi, itakuwa kama gulio tu au soko huru litakalokusanya watu wa kila aina wanaotaka vyeo.”*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwaambieni, sisi wa Chama cha Mapinduzi, suala la rushwa, ni jambo linalokatazwa na ambalo tunakula kiapo ya kulikataa tangu mwanzo. Sasa tunapopiga kelele na kunyooshea kidole uovu huu kwamba sasa tufunge agenda, tuushughulikie na kwa kweli Mheshimiwa Kikwete amechukua hatua za makusudi za kuwashughulikia na ndiyo maana kesi nyingi ziko Mahakamani leo. Kesi za BOT ziko Mahakamani, hakuna atakayesema kwamba hapa hakuna utashi wa kisiasa wa kushughulikia jambo hili. Najua viro viporo. Kiporo cha Kagoda bado, kiporo cha *Deep Green Finance* bado na inakuwa mbaya zaidi kama unazungumza *Deep Green Finance* ambayo imepora bilioni 10 kampuni hii ilikuwa ni wateja wa kampuni moja ya Mawakili maarufu ambayo moja kati ya wamiliki wa kampuni hiyo, ni Waziri katika Serikali hii, tena mwenye nafasi muhimu ya kuwezesha kupatikana kwa wale wateja wao ili waweze kuchukuliwa hatua na kuendelea kujenga imani ya Serikali ya CCM kwa wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tufunge agenda ya ujisadi kwa kushughulika na *Deep Green Finance*, kwa kushughulika na Kagoda na kwa kushughulika na waovu wale bila kitizama sura wala dhamana walizonazo katika Serikali wala kuangalia nyuso za watu hao. Mkitaka agenda hii ife, shughulikeni nao, hamtaki agenda ife, tutaendelea kuzungumza mpaka mwisho na hiyo itakuwa mpaka siku ya mwisho tutakayoacha Ubunge na hatuna mpango wa kuacha Ubunge katika siku za karibuni na hasa ukizingatia kwamba wananchi wanatuamini na tutaendela kuyasema haya. Wale wanaosema Majimbo yetu yako wazi, ni burudani na mimi namshukuru sana Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, ameeleza japokuwa pengine maudhui yanaweza kuwa si mazito sana lakini ukweli ni kwamba wananchi wa Simanjiro wala hawana muda wa kusoma hivyo vigazeti, wanajua wazi kwamba Mbunge wao wa 2005-2010, ni Ole-Sendecka na baada ya yote niliyoyafanya hawana sababu ya kwa nini wasinirudishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawakaribisha wote wanaokuja waweze kunisindikiza kwa sababu wanajua wazi kwamba hatimaye watashindwa tu kwa sababu nitakachoonesha ni kile nilichokifanya toka sekondari tatu kwenda 16 na kesho namalizia ya 17, maji nimechimba katika maeneo mengi na hivi vingine vikesikesi na vingine hivyo tutashughulika navyo kwa utaratibu unaotakiwa. (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kurudia kuzungumza mambo yenye maslahi kwa Jimbo langu na haya ni suala la sekta ya madini. Tuliunda Tume ya Bomani, kabla ya hapo tulikuwa na Kamati ya Bukuku, tulikuwa na Tume ya Masha, tulikuwa na Tume ya Gen. Mboma na kwa kweli nikwambie Tume zote hizi zilitoa matumaini. Wakati umefika sasa wa kuhakikisha kwamba tunawafariji wananchi wa Mererani na Tanzania, kwa kutekeleza mapendekezo ya Tume ya Bomani. Kwenye taarifa ya Tume ya Bomani, wote tutakubaliana kwamba imesema madini ya vito ni kwa Watanzania. Tunataka madini ya vito yabaki kuwa kwa Watanzania, tunataka Tanzanite ibaki kwa ajili ya Watanzania, tunataka wengine wanunue madini ya Tanzanite kutoka kwa Watanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya watu ninaowaheshimu sana katika makala zake, ni Generali Ulimwengu. Katika moja ya makala zake, siku moja alikuwa anachambua kwa kulinganisha mabepari na akasema naomba kunukuu.

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa nguvu zote. (*Makof*)

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijasema chochote katika hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba nitamke wazi kwamba naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafanya hivyo kwa sababu mbili tu. Sababu ya kwanza, ni maelezo ya Waziri Mkuu katika ukurasa wa nane alipokuwa anazungumzia suala la

muungano. Lakini suala la pili ni ukurasa wa 54 ambapo Mheshimiwa Waziri Mkoo alikuwa anazungumzia suala la michezo. Sasa mimi najikita katika mambo haya mawili na nimetamka mapema ninaunga mkono kwa sababu hizi mbili kwa sifa ambazo Mheshimiwa Waziri Mkoo anaonekana ni muadilifu sana katika kufuatilia masuala ya muungano lakini na yale ya michezo ambayo leo atakuwa na darasa zuri katika upande huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimsifu Mheshimiwa Waziri Mkoo, ni msikivu na *speed* yake ya utendaji tangu alipoingia katika Bunge hili ni hali ya juu sana. Ni mtu wa kupigwa mfano katika Jamhuri yetu ya Muungano wa Tanzania lakini nalisema hili kwa sababu kwenye Kikao cha Kumi tulivutanavutana kidogo hapa ndani ya Jamhuri ya Muungano na lilileta matatizo lakini namsifu sana kwa sababu katika kikao kile alitamka wazi kwamba ndani ya madaraka yake atakapokuwepo katika Bunge hili au atakapokuwa Waziri Mkoo, hataruhusu na hatakuwa tayari muungano huu uvunjike ndani ya mikono yake. Hilo ni jambo la msingi na jambo la kishujaa sana. Nimesema hivyo kwa sababu kuna vitimbakwiri wale watatu wanautia maneno katika huu muungano. Sasa kwa msimamo ule, mimi amenipa moyo mkubwa sana na namsifu sana kwa lile. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini najua maelezo yale yanatokana na kipengele kimoja cha hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, naomba ninukuu, Mheshimiwa Jakaya Kikwete alisema kwamba:-

*“Muungano hivi sasa unaimarika lakini ndani ya Muungano huu, kuna wenzetu wanaotaka kuturudisha nyuma ili tuweze kuja kuangaliana kwa sura, kwa rangi au kwa kabila na tutizame huyu anatoka wapi”.*

Sasa kwa kauli hii Mheshimiwa Waziri Mkoo na Mheshimiwa Rais, mimi natoka Zanzibar lakini nawaunga mkono kwa kauli hii na huu ndiyo msimamo wa Chama cha Mapinduzi na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Lakini kuna mambo matatu lazima tuyazingatie ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, muumini wa muungano kufikia hatua katika kuvunja Katiba, si sahihi. Lakini la pili, muumini wa muungano wakawa wanadharau mambo ya muungano au yasiyo ya muungano, si sahihi. Lakini la tatu akatokea mmoja wetu akawa mbabembabe tu humu katika muungano, si sahihi na hili la mwisho nalisema kwa sababu hivi sasa kumeanza vijigazeti fulanifulani kuanza kusema kwamba hivi sasa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inafanya ubabe. Hakuna ubabe hapa, hapa pana utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ushirikiano mzuri wa muungano huu tulianzisha mwaka 1964 kati ya Mwl. Nyerere na Karume, kwa sisi kushikamana kufanya mambo kwa pamoja. Sasa nachotaka kumwambia Mheshimiwa Waziri Mkoo na hili ninawahakikishia atakapoliondoa hili Mheshimiwa Waziri Mkoo atapanda chati. Sisi Wazanzibar kama ataturuhusu tutakuja kumbeba kichwani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inasema kwamba suala la michezo si la muungano. Narudia tena, Katiba ya Jamhuri ya Muungano

wa Tanzania inasema suala la michezo si la muungano. Nchi ya Zanzibar ndani ya Jamhuri ya Muungano, ina Chama cha Mpira wa Miguu kinaitwa *ZFA*. Tanzania Bara ambayo zamani ilikuwa inaitwa Tanganyika ilikuwa na Chama kinaitwa *FAT* na hivi sasa *TFF*. Hivi ni vyombo viwili vinavyofanya kazi ndani ya Jamhuri ya Muungano, vinafanya katika pande mbili bila ya kuwa ndani ya muungano. Lakini Tanzania nje ya Jamhuri ya Muungano inaitwa Tanzania kwa maana ya Jamhuri ya Muungano katika masuala ya michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni mwaka wa 45 hivi sasa, kuna wenzetu wamekuwa wakivunja Katiba hii mfululizo bila woga. Wanavunja Katiba kwa sababu wanajirundikia nyadhifa bila ya ridhaa ya Zanzibar. Narudia tena masuala ya michezo si ya muungano. Mheshimiwa Waziri Mkuu, *TFF* si chombo cha muungano, ni chombo cha Tanzania Bara. Lakini tunapokwenda nje kuiwakilisha nchi, Zanzibar tumekubali kwamba wenzetu wa muungano wajisajili katika vyombo vyta kimataifa nje kwa sababu ndivyo Katiba yetu inavyosema. Wakishamaliza kujisajili huko nje, warudi ndani tushirikiane katika kufanya mambo yetu Kijamhuri ya Muungano wa Tanzania kuelekea nje. Sasa hili halifanyiki. Tunavunja muungano tangu tulivyounsgana mwaka 1964 mpaka leo tunavunja Katiba kwa sababu hakuna mtu anayelishughulikia. Hili tumeliona, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imeandika barua katika Wizara husika kulielezea suala hili ili tukae pamoa. Mimi binafsi nimeshauliza maswali mara tano kuzungumzia suala hili, sina jibu. Mheshimiwa Waziri Mkuu, hii ni dosari kubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale wasioipenda Jamhuri ya Muungano na wasioipenda Zanzibar wanachukua *advantage* kwa hili kusema Zanzibar hatuna kazi wala hatufanyi chochote. Kwa hiyo, suala la michezo si la muungano. Kwa hiyo, ninachokiomba kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, tuwe na *ZFA* na *TFF* lakini tuwe na chombo kimoja cha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kitakachotuwakilisha nje katika mambo ya kimataifa kimichezo. Lakini hilo kama halifanyiki tunakwenda wapi na tunampa nani madaraka hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mimi nitakupa mfano, kitu kinachotokea sasa hivi ni malumbano katika vyombo vyta habari, malumbano mitaani, haifai. Ushirikiano ndani ya Jamhuri ya Muungano, ni jambo muhimu. Nitakupeni mfano. Wakati alipokuwa Mwenyekiti El-Mammry, Mohamed Musa, Ndolanga, Kipingu na Mheshimiwa Missanga, hawa walikuwa wanashirikiana na Zanzibar kimataifa. Walipokuwa wanakwenda nje kuwakilisha Tanzania, *FIFA* walikuwa wanachukua wajumbe kutoka Zanzibar kwa maana ya kuitangaza Tanzania, kuna nini? Juzi gazeti la Juni, 13, El-Mammry kawasihi na kawaomba *TFF* wakiwa chini ya Urais wa Tenga, waendelee kushirikiana na Zanzibar katika suala hili. Tenga hataki, maana Tenga ana kiburi, ana jeuri ana ubabe, sijapata kuona, hataki chochote. Lakini sisi Wabunge humu tuna matatizo, Mheshimiwa Waziri Mkuu unafahamu. Kuna baadhi ya watoto wetu wakati mwingine huva kofia zetu, akiwa mtoto wa Mbunge basi anataka kuva koti la Ubunge, si lako.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hafidh, tunapokuwa tunachangia humu ndani na tuna wagusa watu ambao hawana nafasi wala fursa ya kuweza wala kujitetea, maneno jeuri, wana kiburi na kadhalika si maneno mazuri. Kwa hiyo, naomba uendelee kuchangia nikikukumbusha tu kuhusu masuala ya lugha.

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuelewa, unajua kule Zanzibar huwa tuna mtindo wa mtu akiwa na sifa zake humpa. Sasa mimi nashindwa kuvumilia mtu kumpa sifa yake kwa sababu ndivyo nilivyolelewa. Lakini umenielewa nataka kuelekea wapi. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika suala hili, kauli nazo zina matatizo, unanikataza mimi nisitumie kauli lakini katika kipindi cha michezo tarehe 10 Juni, ndugu yangu huyu amesema wazi kwamba Zanzibar maana yake ni Jamhuri ya Muungano sasa mtu mmoja anapozungumza Jamhuri ya Muungano peke yake si sahihi. Anasema, Zanzibar hawawezi kushirikishwa katika mambo yoyote ya *FIFA* kuitia mgongo wa *TFF*. Twende wapi au atokezee mwendawazimu mmoja aseme tuvunje muungano? Mimi nasema haiwezekani na mimi sikubali. Zanzibar ni sehemu ya muungano tupitie hapo, sasa tushirikine katika hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine tatizo kubwa linalotajwa hapa ni dhambi ya ubaguzi. Dhambi ya ubaguzi kaikataa Mwl. Nyerere, kasema hakuna kitu kibaya kama dhambi ya ubaguzi. Mkianza ubaguzi ndani ya Jamhuri ya Muungano mtakuwa hamuishii hapo, akasema ni sawa sawa na mtu anayekula nyama ya mtu. Sasa huku kuna ubaguzi, kuna ubaguzi kwa sababu hii Zanzibar ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano kwa nini isishirikishwe kwenye mambo haya?

Mheshimwia Mwenyekiti, Rais ninayemzungumza hapa hajaishirikisha Zanzibar katika kombe la Cocacola, hajaishirikisha Zanzibar katika timu ya Taifa wala katika mashindano yaliyokuwepo hivi juzi South Africa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la mwisho, muungano huu una sifa zake, Zanzibar tumemtaka arudishe ligi ya Muungano na hii ni sifa kwa sisi. Sasa huu ubaguzi unatokea wapi? Lakini Mwl. Nyerere alisema hauishii hapo na kweli haukuishia hapo, sasa hivi CHANETA na CHANEZA tayari malumbano. CHANETA kesho kutwa wana kombe la dunia lakini CHANEZA haimo. Sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu tunakwenda wapi, kwa nini tunaachia mambo ambayo tunaweza tukayazungumza? Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano anasema yale mambo yanazungumzika kaeni mzungumze. Wenzetu upande huu, hawataki. Sasa kama hawataki sisi tunakwenda wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine kinachonishangaza, maana kama mtu ukiwa hutaki basi onyesha kile unachoonesha, maana katika mpira wa miguu Tanzania haijachukua kombe hata moja angalau tungkuwa tunasema basi wenzetu huko wameshachukua moja. Katika kombe la *CECAFA* wameshachukua matatu, lakini hakuna chochote kilichofanyika hapa, tangu tumeanza mwaka 1964, Tanzania hatujachukua kikombe hata cha kahawa, haiwezekani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushirikiano gani huu, nani kachukua kikombe hapa? Lakini tunakaa hapa tunajisifu, Tanzania mpira umepanda, mpira umepanda wapi? Tushirikiane tufanye jambo la maana. Rafiki yangu Mheshimiwa Bendera anajua vizuri hatujachukua kombe hata moja, sasa tushirikiane ili tuchukue kombe, tusicifu tu tukapoteza fedha zetu za Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine, hakuna kitu kibaya kinachochonganisha ndani ya Jamhuri yetu kama vyombo vya habari. Mimi vyombo vya habari navistahi sana maana mimi mwenye nilikuwa Mwandishi wa Habari. Lakini kuna baadhi ya vyombo vya habari nilikuwa naviheshimu sana lakini vimeduwa vichochezi ajabu. Mimi naiheshimu *TBC*, naiheshimu *Radio One* lakini kwa kule *Radio One* kuna baadhi ya watangazaji ni wakorofi sana katika Jamhuri hii na wanaleta matatizo makubwa. Juzi anafanya *interview* na kiongozi mmoja wa *ZFA*, anamwambia nyie mnalalamika kwa sababu viongozi wa *TFF* wamekwenda katika nchi za nje kuwakilisha nchi. Akamwambia ndiyo, kwa sababu sisi hatukushikirishwa. Akamwambia, si wanakuwakilisheni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika dini zetu si Wakristo, si Waislam, unapofika pahala unapotaka kuoa, ile siku ya kwenda kanisani kama una dharura basi unamtuma rafiki yako mpenzi akavishe pete na sisi Waislam hali kadhalika tunapokwenda kuoa unamshirikisha mwenzio lakini humshirikishi ukamwambia kaniingilie ndani, haiwezekani! Umepata kuona wapi mambo hayo? Nani keshafanya mambo haya? Sasa yule mtangazaji anamwambia, *TFF* si wanakushirikisheni! Alaah, unatushirikisha kwenye kuingia ndani? Haiwezekani! (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa haya ni mambo ambayo kwa kweli yanaleta adha, yanaudhi na kwa kweli huyu kijana huyu amepata kiburi maana huwa najiuliza mie kiburi hicho kakipata wapi? Hivi kati ya wale viongozi wawili walioungana baina ya Zanzibar na Bara, Mwalimu Nyerere na Karume, hivi baba yake nani? Katika hawa wawili huyu kiongozi niliyemzungumza, ie, baba yake nani? Lakini anashindwa kutekeleza Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, anavunja Mheshimiwa Waziri Mkuu. Sasa ninakuomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, tafadhali suala hili lisimamie na sisi Wazanzibari tuko nyuma yako na tutakupa sifa sana suala la michezo likirudi katika hali yake. Ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tuwe Watanzania, lakini nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tuwe Watanzania Kimataifa.

(*Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha*)

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukinisimamisha, unanionea maana ulinisimamisha pale!

**MWENYEKITI:** Tumeisharekebisha muda tayari!

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii asilimia mia moja. Ahsante!

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, Mbunge wa Dimani. Labda kabla sijamwita mchangiaji mwengine, niweke sawa neno moja tu. Hoja hii imejitokeza mara kadhaa katika Bunge letu na kama nimemsikiliza Mheshimiwa Tahir, pendekezo lake tuwe na ZFA, TFF halafu tuwe na chombo cha kutuwakilisha nje. Swali langu, kwa mtazamo huo sasa, si ndio Serikali tatu, sio ndio kuvunja Katiba? (*Makofi/Kicheko*)

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kuwa mzima na afya njema, nikaweza kusimama katika Bunge lako Tukufu. Pili, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, maafa utayakuta katika kifungu kuanzia 101 mpaka 105. Nia yangu ya kwanza, ni kuzungumzia suala la maafa ya Boti ya Tanga. Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kabla ya kulizungumzia hilo, nieleze mashaka yangu kuhusiana na hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na maelezo yaliyoko katika kifungu 102. Kwa maoni yangu, naona kuna upungufu mdogo hivi ambao Serikali ilipaswa itupe maelezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukikiangalia kifungu cha 102 ambacho kiko katika ukurasa wa 70, hapo yameelezwa maafa mbalimbali na ukiangalia maafa kama ya machimbo ya madini katika kijiji cha Mgusu, Geita, inasema kuwa waliokufa ni zaidi ya watu 6, inaendelea ajali ya treni watu 7, ukumbi wa starehe watoto 19. Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini unapokuja chini kabisa ya kifungu hicho utakuta ajali za kuzama kwa Boti huko Tanga na Meli Zanzibar, hapa hapana idadi, hapana maelezo hata mafupi ambayo yalistahili kuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inanidhihirishia kuwa inaoneka Serikali hawakuwa karibu sana na suala hili, angalau kutuarifu sisi kuwa katika ajali hasa hasa iliyotokea Tanga, kwa sababu Meli ya Zanzibar, naamini Serikali ya Zanzibar itakuwa ina taarifa kikamilifu. Lakini hata Boti ya Tanga ilipaswa Serikali itueleze janga hili lilitokea na hali ilikuwaje japo kwa ufupi kama ambavyo imeelezwa katika maafa ambayo yameelezwa hapo juu. Serikali ilipaswa kwa kweli itueleze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuchukua nafasi hii, kuelezea suala la maafa yaliyotokea Tanga. Tarehe 14 mwezi wa nne mwaka huu, boti inayojulikana kwa jina la Amana Pemba, iliondoka usiku wa tarehe hiyo 14 kwenda Pemba katika bandari ya Mkoani ambapo ndilo Jimbo langu. Kufikia saa saba za usiku wa siku hiyo, au itakuwa tarehe 15 tena hapo, chombo hiki kikiwa nje kidogo ya bandari ya Tanga, kilipata matatizo na kuanza kuungua. Yuko mwananchi mmoja wa Tanga ambaye anaitwa Mustafa Talib Ali, alipewa taarifa hii bila shaka na abiria ambaye alikuwemo ndani ya chombo. Mwanchi huyu alikwenda moja kwa moja kwa Diwani wa Ngamiani Kusini, ambaye ni Mheshimiwa Musa Bakari na wao kwa pamoja wakatoka wakaenda bandarini Tanga na kutoa taarifa pale kuhusu ajali hiyo. Kwanza, ilionekana kuna ubishano baina ya wafanyakazi wa pale na hawa waliopeleka taarifa. Lakini wao waliwaambia sisi

wajibu wetu ni kuleta taarifa kuwa kuna wenzetu wako katika hali ngumu kwa hiyo, ni juu yenu kama mtakwenda au hamtakwenda, sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Diwani huyu pamoja na mwananchi huyu mwema, kwa kweli hawakuishia hapo, wakaenda Kituo cha Polisi cha Chumbageni kutoa taarifa karibu kwenye milango ya saa nane. Pale Kituo cha Polisi cha Chumbageni, Polisi wakawasiliana na *Marine Department*, lakinii ilionekana mawasiliano hayapo. Walitumia *redio call* hawakuwapata, walitumia simu za mkononi, hawakuwapata, hiyo ndiyo hali ya nchi yetu ilivyo, huku wananchi wanateketea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasemekana boti ilitoka ikaenda usiku ule, lakini haikufika katika eneo la tukio na tetesi ambazo sisi tulizipata pale Tanga, walidai kuwa kulikuwa na hali ya hewa ngumu. Lakini cha kusikitisha, ni kuwa boti ndogo ya kuvulia dagaa ambayo kule Zanzibar tunaita ngwanda, ikiongozwa na Nahodha Abdi Kombo Abdi, ilithubutu kwenda katika chombo kile na kuokoa watu saba lakini Boti ya Serikali ambayo ipo pale, naamini ilikuwa katika umbile la chuma na ni chombo kikubwa, haikufika katika eneo lile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kusikitisha zaidi ni kuwa, nilitegemea Mamlaka zinazohusika pale Tanga, kwa sababu tukio limetokea saa saba, angalau basi tukio lile waanze kulishughulikia alfajiri ya tarehe 15. Lakini jambo la kusikitisha, ni kuwa walianza operesheni ya kwenda katika eneo la tukio kuanzia saa nne za asubuhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kukwambia, sikwambii suala la bahari, hata ingelikuwa suala hili ni ajali ya barabarani, kama mtu anatokwa na damu (*bleeding*), basi huwezi ukamwacha mtu masaa, ukaenda asubuhi saa nne ukamkuta yuko hai. Wakaenda saa nne baada ya juhudu kubwa ya Kamanda wa Mkoa wa Tanga, Ndugu Siro ambaye mimi huyu nampa sifa kweli kweli, lakini waliobakia wengine wote, kwa kweli Serikali inabidi walishughulikie ili ionekane wapi kumetokea tatizo hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamekwenda katika eneo tarehe ile saa hizo, lakini hakuna walichokikuta, hawakukuta maiti au watu hai. Kilichotokea, kwa sababu kuna chombo tarehe 15 asubuhi kilikwenda kule, cha mtu binafsi vile vile, kikaokoa watu nane na wakapelekwa hospitali ya Bombo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwishowe nilipata maelezo, kwa sababu habari hizo zinatokea, mmi niko Tanga, kuwa chombo kinachotoka pale kwenda Pemba, wanapozama, basi hali inabakia hivyo hivyo, haishughulikiwi. Hili ni tatizo! Bandari zetu zinaonekana haziko makini katika uokoaji wa watu wetu. Kwa hiyo, ninaomba Serikali wachunguze suala hili ili ijulikane ilikuwaje kwa kweli. Hali hii ndio inaonekana katika kifungu 102 ambapo hakuna taarifa ambayo angalau inatupa mwanga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, chombo hiki kwa taarifa za awali za Polisi, ilisemekana mna watu 40, lakinii baada ya kudadisi watu hapa na pale, tukagundua kuwa kilikuwa na watu wasiopungua 52 wakiwemo watu wazima 43 na watoto 9.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu wananchi walikosa huduma ya uokozi, cha kusikitisha, kilichotokea ndani ya chombo, wanawake, baada ya moto kuwazunguka, yuko mmoja aliyeokoka ambaye yuko katika Jimbo langu, muda mrefu alilazwa Abdallah Mzee Hospitali, kaeleza kuwa wanawake waliamua wafe na watoto wao, wakawakumbatia. Yeye alipoona moto umeishamuunguza miguu yote miwili, akaamua akafe kwenye bahari. Akaja mwingine ana mtoto, akaona bahari hakuendeki, juu hakukaliki, kafa. Hii ndio hali ya watu ambao wamepewa mamlaka hata kuchukua juhudui, hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifo huwezi kukizua, lakini Serikali ina wajibu wa kuona kuwa inapotokea janga, basi inashughulika, hayo mengine tumwachie Mwenyezi Mungu. Lakini boti inapotoka na inarudi, boti ya mtu binafsi inaokoa, kwa kweli hili linasikitisha sana. Huo ndio mchango wangu wa kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wa pili, nizungumzie suala la Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Tume ya Taifa ya Uchaguzi, imeacha uwakala katika uandikishaji kwa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar. Sawa! Lakini nilichokibaini, tatizo lililopo, ni kuwa Wakala huyu anatumia Sheria za Zanzibar kwa sababu wamo wanaochaguliwa kwa misingi ya kuwa ni Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Zanzibar. Tunapozungumza Rais wa Jamhuri na Wabunge, kwa hiyo, ilitegemewa kuwa sheria zitakazotumika ziwe za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Katiba. Sasa unapoacha uwakala kwa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, uandikishaji wao huwa wanachukua sheria za Zanzibar. Hili ni tatizo. Ndio utakuta manung'uniko ambayo yanakuja kuwa, kwa mujibu wa Sheria za Uchaguzi Zanzibar, huwezi ukaandikishwa pamoja na masharti mengine kama huna Kitambulisho cha Ukaazi hata Cheti cha Kuzaliwa hakikubaliki, kama huna hicho basi huandikishwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tulitegemea sisi anaachiwa Tume ya Uchaguzi Zanzibar, watafuata sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Unapokataa vitambulisho vingine katika kuandikisha hususan kwa uchaguzi unaohusu Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kweli unakwenda kinyume na Katiba ya Jamhuri ya Muungano na hili ndilo linalotendeka Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ushahidi, ukurasa wa 16 wa Katiba unaeleza, Ibara namba 5(1), naomba ninukuu:-

*“Kila raia wa Tanzania aliyetimiza umri wa miaka kumi na nane anayo haki ya kupiga kura katika uchaguzi unaofanywa Tanzania na wananchi. Na haki hii itatumiwa kwa kufuata masharti ya Ibara ndogo ya (2) pamoja na masharti mengineyo ya Katiba hii na ya Sheria inayotumika nchini Tanzania kuhusu mambo ya uchaguzi”. Hapo hapana matatizo.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 5(2) inasema:-

*“Bunge laweza kutunga sheria na kuweka masharti yanayoweza kuzuia raia asitumie haki ya kupiga kura kutokana na yoyote kati ya sababu zifuatazo, yaani raia huyo:-*

- (a) .....
- (b) .....
- (c) .....
- (d) *kukosa au kushindwa kuthibitisha au kutoa kitambulisho cha umri, uraia na uandikishwaji kama mpiga kura... ”* Hii hapa, unaweza ukakosa haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaposema kitambulisho cha umri, unaposema sawa, Kitambulisho cha Ukaazi ni kitambulisho ambacho kinakubalika, lakini unaposema ni hicho tu, hukubali Cheti cha Kuzaliwa, kwa kweli mantiki haipo. Kwa sababu mimi kwanza nimezaliwa kama Ali, napata Cheti cha Kuzaliwa, baadye ndio hicho Kitambulisho cha Ukaazi. Sasa ile asili yangu mimi yakataliwa, chachukuliwa kile cha juu! Hili halieleweki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunapoandikisha wapiga kura kwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano, sijui Zanzibar, kwa kweli kuwakataa wananchi kujiandikisha kwa Cheti cha Kuzaliwa, basi kwa kweli tunavunja Katiba. Kwa hiyo, ninashauri Tume walione hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipengele kingine cha sheria kinachoonyesha kuwa haipasi kwa kweli Tume ya Taifa ya Uchaguzi kuendelea kuwaachia Tume ya Zanzibar, ni kuwa iko sheria inasema kuwa kuna suala la uhamisho wa wafanyakazi wakati wa uchaguzi. Wakala ambaye kapewa kazi na Tume ya Taifa ya Uchaguzi anakuwa analisimamia ipasavyo. Hii ina maana gani? Kuna uwezekano wa kuhamishwa watu wakati wa uchaguzi kwenda katika maeneo mengine ili kujiandikisha kwa muda wa uhamisho. Nitoe mfano katika Jimbo langu la Mkoani, kuna eneo la Makombeni, kuna kambi, katika hali ya kawaida, huwa ni watu 20/25 KMKM pale, lakini uchaguzi wa mwaka 2000 kwa kutumia kipengele hiki wakaletwa karibu watu 1800. Haya pia yanatokea Mkanyageni, yanatokea Wawi, yanatokea Chonga. Sasa leo Tume ya Taifa ya Uchaguzi...

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Ahsante Mwenyekiti.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hotuba hii. Lakini, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuniwezesha kupata nafasi ya kufika siku ya leo, ili na mimi niweze kuwa mmoja wa wachangiaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napnda nitoe pongezi nyingi sana za dhati kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa jinsi alivyoiwasilisha hoja yake na zaidi mno kwa jinsi

alivyomshirikisha Waziri wa Nchi, TAMISEMI, Mheshimiwa Celina Kombani, katika kuiwasilisha hotuba ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba hii ama hotuba zote mbili kwa pamoja, zilionyesha dira na mwelekeo mzuri ambao umetuwezesha wachangiaji kupata namna nzuri ya kuchangia. Napenda niwasifu na niwapongeze kwa utendaji wao bora wa kazi, kwa usikivu na ufuutiliaji. Kwa kweli niwasifu kwa jinsi ambavyo wanatutia moyo unapokuwa na haja ya kuwaona, unajisikia mwepesi na unaweza kupata majibu sahihi kwa kadri inavyowezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niishukuru Serikali kwa jinsi ambavyo imeturahisishia sisi Wabunge kazi yetu kwa kusaidia kuboreha huduma za Waheshimiwa Madiwani. Hali za Madiwani hazikuwa nzuri, lakini kwa sasa hivi posho zao zimeboreshwa, sasa hivi wana Bima ya Afya, sasa hivi vyombo vyao vya usafiri watakavyovihitaji vitakuwa havina kodi mbalimbali ambazo zilikuwa zinakuwa tatizo. Lakini, pia katika hilo hilo, naomba niombe Serikali iweke urahisi wa kuwezesha Madiwani hawa kupata vyombo vya usafiri. Uwepo mpango mzuri katika Halmashauri kuweza kuhakikisha kwamba Madiwani wote wanapata vyombo vya usafiri na isiwe hisani bali iwe ni haki yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Serikiali ijithahidi kuboresha hali hizi zinazotofautiana katika Halmashauri za Wilaya. Katika Wilaya ambazo ziko mipakani kama ya Muleba, tunahitaji tusaidiwe hata watendaji wetu wa kata, walau tuanzie wa kata, wapate vyombo vya usafiri. Zamani walikuwa wanapewa vyombo vya usafiri lakini sasa hivi hawapewi. Watakapokuwa wamekubaliwa kupewa, *view* vya kwao, wavichukue kwa kulipia kidogo kidogo ili waweze kuvitunza na waweze kudumu navyo katika kazi kwa sababu kuna utendaji mgumu tunapokuwa na watendaji wanaohudumia kata lakini hawana usafiri kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda pia nishukuru kwa jinsi ambavyo Serikali imeendelea kutufahamu na kutusaidia. Kwa mara ya kwanza kabisa, haijawahi kutokea Muleba tumepata Boti. Hii inathibitisha kwamba sasa Serikali imefahamu kwamba Muleba si kwamba ina nchi kavu tu, lakini pia inavyo visiwa vinavyounda kata tatu katika Wilaya na ambavyo tumeviombea vipate tarafa kwa sababu ya mazingira magumu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara ya kwanza mwaka huu, tumeanzisha sekondari katika visiwa hivi vilivyo katika Jimbo la Muleba Kaskazini. Tunayo sekondari inaitwa Bumbile na tayari imesajiliwa. Nilikuwa napata hofu sana jinsi ambavyo uendeshaji utakuwa mgumu katika shule ile, lakini sasa kwa kupata boti hii kwa kuanzia, naamini hali itakuwa nzuri na ikifika kwenye Wizara ya Elmu, ningeliomba waangalie shule hii kwa upkee kwa sababu ni shule iliyio katika mazingira ya kipekee na ni shule ya kwanza katika visiwa, namimi katika Mkoa wa Kagera ili hawa wanafunzi wasipatishwe tabu, Walimu wao wasipatishwe tabu ili iweze kuwa ni shule inayopendeka na inayokubalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru pia kwamba tumeweka katika orodha ya kupata nyumba kwa ajili ya watumishi walio katika mazingira magumu, lakini pia posho za watumishi walio katika mazingira magumu zizingatiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninacho kisiwa ambacho kwenda kwangu inanichukua siku nane ili niweze kufika. Kisiwa hicho kinao watumishi wa Serikali amba mara kadhaa wanapotea ndani ya maji, wanaokotwa Uganda, wengine hata hawajulikani kabisa. Kumekuwa na ugumu wa mtu kufuata mshahara wake Makao Makuu ya Wilaya na kurudi katika eneo hilo. Kwa hiyo, kwa kutufikiria kwamba sasa hawa wapate posho za mazingira magumu, naamini ni moja ya njia zitakazosaidia kutoa ari ya utendaji kazi kwa hao watumishi watakaokuwa wamepangwa katika mazingira hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina tatizo pia la eneo linaloitwa Lutolo, ni moja katika kata zangu ambalo mtumishi wake akitaka kuchukua mshahara, anachukua zaidi ya wiki moja. Kwa hivyo, naamini kwamba sasa watakuwa na moyo wa kufanya kazi. Kwa hali hii, naamini kabisa Walimu wa Muleba, Waratibu wa Elimu wa Kata, watumishi wa afya, watumishi wa mifugo na uvuvi amba wako katika mazingira magumu katika Wilaya ya Muleba, watakuwa wametiwa moyo na naamini mazingira haya ambayo wengi walikuwa hawaendi, sasa watakwenda kufanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia nishukuru kwa ujenzi wa Ofisi ya Mbunge yenye viwango katika Jimbo la Muleba Kaskazini, nashukuru sana. Naiomba Serikali sasa iipatie huduma za muhimu kama za watumishi ili kusudi iweze kufanya kazi. Kama mnavyofahamu, Mbunge peke yake si ofisi inayojitegemea akiwa peke yake hasa baada ya kuwa mmeshamjengea, kwa sababu Mbunge kama hayupo, Katibu wa Mbunge pekee hawezи kuendesha ofisi, inahitajika iwe na mhudumu, inahitajika iwe na karani na inatakiwa iwe na mlinzi ili ilindwe, ipandishiwe bendera na isafishwe mazingira. Haya ni mambo ya muhimu, lakini pia isikose kuwa na kompyuta kwa sababu huu wakati tulionao, mitando ni muhimu na pale kuna umeme, ni lazima *internet* pale iwepo. Kwa hiyo, huduma hizi naomba ziwe ni sehemu ya kuboresha ofisi za Wabunge ili waweze kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya shukrani zangu nyingi sana, ni mengi siwezi nikayamaliza, lakini napenda niseme ninatiwa moyo na nafarijika kusema kwamba Jimbo la Muleba Kaskazini, kiutekelezaji wa Ilani, ni shwari, kazi zinaendelea vizuri, wageni wote wanaopenda kulikagua na kujionea maendeleo na kujipima nguvu, wanakaribishwa wakiwa wanafahamu kwamba Jimbo hili liko salama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, naomba niwasilishe kero. Ninayo kero ya muda mrefu sana, nadhani kipindi changu cha pili nimeingia katika Ubunge huu, kero hii haijapatiwa majibu. Ni kitu ambacho naomba Serikali sasa inisikilize kwa makini. Tulikubaliana katika Bunge hili hili na mimi nikiwa Mbunge kipindi kilichopita kwamba baadhi ya ranchi tuzibinafishe ili tuweze kuboresha ufugaji bora, tulikubaliana. Lakini tulikubaliana kwamba tutakapofanya hivyo, hatutakwenda kuharibu miundombinu wala kuhamisha wananchi walioko kwenye vijiji labda kama ni mtu mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimeathirika na uamuzi tulioamua sisi wenyewe hapa. Nilikuwa na vijiji vitatu vinajulikana jina la Lutolo, Ngenge na Kishulo vilivyosajiliwa na ambavyo wanaishi wananchi. Vijiji hivi bila kujua, nimekuwa navyo tangu mwaka 1995 nilipoanza kuwania mara ya kwanza, nilivuju na nilikuwa nashirikiana navyo lakini mwaka 2006 wakati wa kuingizwa kwenye ranchi, ndio mara ya kwanza mimi nafahamu kwamba hivi vijiji vilikuwa ni sehemu ya *NARCO* kwenye ranchi ya Kagoma. Tumeanza kuhangainka kuomba kwamba Serikali isitenge zile *block*, isizimilishe, lakini mpaka leo hii kinachoendelea kufanyika hawa wamilikishwaji wadogo wadogo waliopewa, sasa wamepewa hati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kinachonisikitisha na kilichofanya kwa nini leo nizungumze; nilipoleta hoja hii kuomba kwamba baadhi ya vitalu vifutwe kwa sababu viko katika makazi ya wananchi wengi, nikaambiwa kwamba hapa kuna kesi, nenda waambie walioweka kesi Mahakamani waifute. Nikajaribu kuwatafuta, nikakuta watu wenyewe ni watu ambao akili zao ziko kama walivyoumbwa na Mwenyezi Mungu na wanavyoweza kujisimamia wenyewe, wana haki yao, wakasema sisi hatuwezi kufuta kesi kwa sababu tuna hakika gani kwamba Serikali tukifuta itatoa hivyo vitalu kwa ajili ya wananchi? Mimi nikasema jambo ambalo limesemwa na Mkuu wa nchi, mpaka Bodi yenyeve ameituma *NARCO* ije kuangalia kama hili suala limekaakaaje, wakasema sisi hatuwezi, tukakubaliana. Nikasema si neno, tutaendelea kusubiri hadi kesi yenu imalizike kusudi hao wananchi waweze kupata haki yao. Lakini sasa kesi hii haijamalizika, sasa inakuwaje tena Serikali inakwenda kutoa hati? Naiomba Serikali itangaze kwamba hati hizo ni batili, kwa sababu kama wananchi hawajasikilizwa, hawa wananchi wakaambiwa ile kesi wanashinda ama wanashindwa, Serikali haiwezi kuendelea kutoa hati. Inapotoa hati, inahalalisha kwamba hivi vitalu viendele, wananchi wahame, waendelee kupata shida, kupigwa na kunyanyaswa wakati kesi bado haijamalizika Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba suala hili liangaliwe na naomba hati hizo 14 zilizotolewa zifutwe. Wananchi wanaambiwa waende wakaishi kwenye vitalu viwili ambavyo vitalu hivyo tangu kuundwa kwa dunia havijawahi kukaliwa, ni vitalu ambavyo vina mawe, vina milima na havikaliki, ni *barren land*. *Who can live on a barren land?* Nani atakwenda kuishi pale? Nani atakayeweza kulima pale? Ni mahali pasipowezekana. Hapa ambapo hawa wanataka kuweka mifugo yao, ndipo ambapo tayari panafaa pia kwa kukaa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Serikali, suala hili iliangularie. Kama kesi imeisha, mimi sijui, ni jambo la kushukuru pia, lakini ninaomba basi taratibu zifuatwe, wananchi wapewe nafasi, watoe mapendekezo yao kwa Serikali, ile nafasi walivyonyimwa mwanzo, wapewe sasa ili Serikali inapokwenda kumaliza maamuzi yake ya mwisho, yawe ni yale ambayo inakubaliana walau kwa asilimia zinazotaka kulingana kimizani. Nina hakika, haiwezi kuwa asilimia 100, lakini walau kimizani, zinaweza zikalingana. Hiyo ilikuwa ni kero yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kero ya pili, naiomba Serikali, nawaasilisha maoni ya wananchi hasa wanawake wa Muleba Kaskazini na watoto wangu wasichana wanaosoma

shule za sekondari. Wanaomba Serikali inapotaka kuleta hii hoja ya wasichana kuzaa na kurudi mashulen, iwe makini isije ikafanya hawa wasishana wakawa sasa ni kitalu cha kuchezewa na wote wanaotaka kuchezea watoto wa kike na kuliharibu taifa la Tanzania. Ninaomba wanaume wanaoharibu watoto wa kike, wasiachiwe kwa kusema kwamba zaeni mtasoma, hakuna, jambo hili haliwezekani!

Mheshimiwa Mwenyekiti, akina mama wanasema hivi, wao wana shida ya kulea watoto wao wenye we waliowapeleka shule, hao wajukuu mnaotaka kuwaletea, mmewaandalia mahali pa kuwalelea? Mmewaandalia huduma? Mna mipango gani? Wanasema tuboreshe huduma za wasichana shulen, kuwe na hosteli, kuwe na mabasi ya shule, kuwe na huduma nzuri shulen ili watoto waweze kutulia shulen na kusoma. Lakini sheria hii inayotaka kuja kuwaumiza watoto wa kike na kuleta watoto wengi wanaozaliwa bila kujulikana baba zao, hali hii itakuwa ni ya kuwakandamiza zaidi akina mama wanaozaa wale wasichana waliobebeshwa tena mimba, kwa hiyo inakuwa ni mzigo juu ya mzigo mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda hautanitisha, lakini basi nilipenda niyaseme hayo na nimalizie na maombi. Tunaomba yafuatayo, maji Muleba Kaskazini, daraja la Kishara, nyumba za Walimu, maabara na Walimu wa kutosha katika shule zetu. Mwisho, tunaomba tutembelewe, Mheshimiwa Waziri Mkuu ututembelee, uje uyaone maendeleo yetu, lakini ushiriki na sisi kuona jinsi tunavyoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nkipata nafasi katika Wizara zinazofuata, nitawenza kuzungumza mengine ambayo natakiwa niyawasilishe kutoka kwa wananchi wa Muleba Kaskazini. Ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi, namshukuru Mungu kwa kuniwezesha kuzungumza kwa sababu niliamini sitawenza kupata nafasi, ahsante sana. Naunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

**MHE. MARTHA M MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi hii. Awali ya yote, napenda kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kupata nafasi hii ili nami niweze kuwasilisha maoni ya wananchi wa Mkoa wa Singida. Lakini pia kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Singida, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Waziri wa TAMISEMI na Manai bu wote kwa hotuba nzuri aliyoitoa ambayo imejaa neema na matumaini mazuri kama itafanyiwa kazi vizuri na usimamizi mzuri, italeta tija na faida kwa taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia ninaomba niipongeze Serikali ya Awamu ya Nne, kwa kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi vizuri. Mwenye macho haambiwi tazama. Ujumbe ndio huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia ninaomba nichukue nafasi hii ya kipekee kabisa, kumpongeza Masoud Kipanya kwa ubunifu wake mzuri kwa kuandaa kipindi cha *Maisha Plus*. Kipindi hiki, kimeleta faida kubwa sana hasa katika jamii na watoto wetu. Lakini pia kwa kumpata mshindi huyu Abdul, nimefurahishwa sana na ninapenda kumpongeza kwa wazo lake zuri ambapo amekusudia kupanda Mlima Kilimanjaro kwa

ajili ya kuchangisha fedha kujenga kituo cha watu wenye kisukari. Ninaomba wote wenye mapenzi mema na jamii ya Kitanzania, imuunge mkono. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea, ninaomba nimnukuu Mshairi mmoja wa Kiingereza anayeitwa William Shakespeare katika Julius Caesar, Mshahiri huyu alisema:-

*"I come to burry Caesar, not to praise him.  
The evil that men do, lives after them.  
"The good is oft, interred with their bones"*

Akiwa na maana kwamba:-

*"Nimekuja kumzika Caesar, na sio kumsifu.  
Mabaya yafanywayo na mwanadamu, hudumu baada yao.  
Mazuri mara nyangi, huzikwa pamoja na mifupa yao.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama hapa kwa kutoa mfano huu au nimenukuu maneno haya nikiwa na maana ya kwamba, ninasikitishwa sana na kauli za baadhi ya Watanzania, Mheshimiwa Rais mstaaafu Benjamin William Mkapa, wakati anaingia madarakani mwaka 1995, alitutangazia kwamba tufunge mikanda, mimi binafsi nilijiandaa kufunga mkanda. Wakati tumefunga mkanda na mkanda bado haujakolea, mambo yakaanza kuwa barabara chini ya uongozi wake. Ninashangaa sana kuona watu wanataka kumhukumu kiongozi huyu. Maneno Matakatifu yanasema kwamba:-

*"Usihukumu usije ukahukumiwa, kwa maana hukumu hiyo ndiyo utakayohukumiwa wewe. Ulitoe kwanza boriti katika jicho lako ndipo uweze kukiona kibanzi katika jicho la mwenzako. Kama Mungu wetu angehesabu makosa yetu, ni nani angeweza kusimama mbele au katika Tanzania hii".*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba tumheshimu kiongozi huyu, yale mema tutsiyazike, tuyafanyie kazi ili tuweze kusonga mbele, yale mabaya tuachane nayo na tumheshimu Mungu wetu, roho ya namna hii ninasema ishindwe katika jina la Yesu. (*Makofi*)

**WABUNGE FULANI:** Amen!

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya salamu hizo, ninaomba sasa niendelee kuhusu maendeleo ya Mkoa wangu wa Singida.

**MWENYEKITI:** Baada ya neno hilo Mheshimiwa Martha Mlata, nimemwona Mchungaji Rwakatare ameruka kabisa.

**MHE.MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, amen.

Kwanza kabisa, kama nilivyotangulia kusema, ninaishukuru Serikali kwa kutekeleza vizuri Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Mkuu wetu wa Singida sasa hivi unapaa chini ya *pilot* wetu, Mkuu wa Mkoa, Mheshimiwa Kone. Ninasema haya kwa sababu nina uhakika ukifika ofisini kwa Mkuu wa Mkoa, utakuta ana ratiba ya mwezi mzima kwa ajili ya utendaji wa kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hafanyi kazi peke yake, anashirikiana na *RAC*, Wakuu wa Wilaya wote, Wakurugenzi wote, Makatibu Tarafa, mpaka viongozi wa vitongoji na vijiji. Kwa hivyo, hii imefanya Mkoa wa Singida kupaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwapongeza wote pamoja na Madiwani na viongozi wa Chama cha Mapinduzi, lakini pia niishukuru Serikali kwa kutukubalia kutuweka kwenye mpango wa kujenga Hospitali ya Rufaa ya Mkoa. Hivyo ninaomba pesa ambazo tumeomba, tuidhinishiwe ili tuweze kuendelea na mipango yetu mizuri.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo lingine ambalo ninapenda kulizungumzia, ni kuhusu orodha ya majedwali yanayoambatana na hotuba ya Waziri Mkuu, ukurasa wa 57. Haya ni maombi ya kuongezewa idadi ya vijiji. Katika Mkoa wetu wa Singida, kuna matatizo kidogo *may be ni typing error*. Singida vijijini, vijiji vilivyopo ni 146, walivyoomba ni 58, kwa hiyo, jumla yake ingekuwa na 204, lakini hapa wamevipunguza kabisa jumla vilivyopo ni 146 lakini wamesema kuna vijiji 117, ninaomba hiyo *typing error* irekebishwe. Lakini pia Iramba wana vijiji 126 wameomba 17 wanatakiwa wawe na 143, hapa naona hizi *figure* badala ya 126 zinasema ni 118. Kwa hiyo, naomba hilo lizingatiwe ili tuweze kwenda sambamba na hotuba hii ilivyoelezea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina tatizo, Mkoa wa Singida, wananchi wameitikia kilimo kwanza kabla ya tamko hili. Wananchi wa Mkoa wa Singida, wamejipanga, wamekuwa wakilima zao la alizeti kwamba ndio zao lao mkombozi katika maisha yao na uchumi wao. Tumekwishapata mwekezaji ambaye atakuja kujenga kiwanda kikubwa sana na atasaidia wakulima na kutoa mikopo kwa ajili ya wakulima wa alizeti, lakini kunakuja tatizo, tatizo la ushuru huu uliofutwa wa 10% ya mafuta ghafi kutoka nje, hii itadidimiza sana azma ya Mkoa wa Singida kwa sababu tunajipanga lakini sasa, hiyo 10% ambayo inaondolewa, itakuwa tatizo. Ninaomba Mheshimiwa Waziri Mkuu tusaidie. Wewe ni mtoto wa mkulima, wasaidie wakulima wa Mkoa wa Singida ili waweze kusomesha watoto wao vizuri kama ulivyoweza kusomesha wewe na wakulima wenzao, kwamba hii 10% iendelee ili kusaidia zao hili la mafuta ya alizeti kuleta tija na uchumi wa Mkoa wa Singida pamoja na wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo moja pia, tatizo la wimbo wa barabra ya Isuna – Manyoni. Mimi nasema mikataba mibovu inaturudisha nyuma. Mkataba miezi 36 kilomita 54 yaani, miaka mitatu, mimi sikuufurahia sana. Ninamshukuru sana Mkuu wa Mkoa, vinginevyo tungekuwa hatupiti, amechukua jukumu la kumsimamia mkandarasi yule angalu aweze kuboresha ile barabara ya vumbi iweze kupitika wakati wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote wanaoitumia ile barabara kwenda Mwanza, Shinyanga, Nzega, wanaona ni juhudzi za Mkuu wa Mkoa. Hivyo, ninaomba Ofisi yako Mheshimiwa Waziri Mkuu, uhimize kwa dhati kabisa, hata kama barabara hii inatakiwa ikabidhiwe mwaka kesho mwezi wa kumi na mbili, ninaomba basi ajitahidi mkae kikao ili muweze kuzungumza afanye haraka ili barabara hii imalizike tuanze na mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia napenda nizungumzie suala la mambo haya ya barabra kwa nchi nzima. Unapotaka uchumi uende mbele, ni lazima uangalie *Geographical location* ya miundombinu, huwezi ukasema unaboresha bandari wakati reli huboreshi, huwezi ukasema unaboresha bandari wakati barabara huzitambui, ni zipi zinazofungua mianya ya uchumi kupeleka nchi za jirani? Naomba sana suala hili lizingatiwe ili twende sambamba. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudi upande wa elimu. Tunapozungumzia *quality* na *quantity* sasa hivi Serikali imejikita sana katika kuongeza shule nyingi pamoja na kuhakikisha watoto wengi wanaingia shulenii lakini bado ule ubora wake wa elimu kuna utata. Hebu sasa hivi Serikali kwa ushauri wangu ijikite katika kuboresha elimu hii ambayo tayari tumeshaweka madarasa mengi ili kupeleka vifaa pamoja na Walimu amabao wana *qualify* kufundisha watoto wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini bado hata suala la michepoo katika shule za sekondari hizi za kutwa, naomba litazamwe. Utakuta shule michepoo wake wanasema ni sayansi, lakini hakuna hata Mwalimu mmoja wa sayansi. Mimi naomba kusiwe na ulazima wa kuweka michepoo pale ambapo hakuna Walimu, kama hakuna basi shule iendane na michepoo wa Walimu waliopo pale, kama ni shule za sayansi basi zitengwe chache wanafunzi wapelekwe pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini bado tuna suala la watoto wenyewe ulemavu. Naomba Waziri wa Elimu, atakapokuja kuwasilisha bajeti yake, atueleze fungu la watoto wenyewe ulemavu liko wapi na linasimamiwa na nani ili tujue hawa watoto wanasaidiwaje. Watoto wanazidi kuongezeka, wengine wamepata ulemavu juzi tu kwenye mabomu ya Mbagala hapa, nani anawatazama? Kwa hiyo, naomba suala hilo lizingatiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudi kwenye Bodi ya Mikopo. Mimi nilishangaa sana kuona kwamba bajeti inayokwenda kwenye Bodi ya Mikopo, ni pungufu bilioni themanini, mimi sielewi hiyo bajeti ilikusudia kitu gani! Ninawaomba hilo pengo ambalo linaonekana, Serikali iwe makini tusiwasumbue vijana wetu wanapokwenda shulenii. Tunaposema elimu bora, ni pamoja na kuwatimizia mahitaji yao yote watulie, wasome, sio kila siku kwenda kuangalia fedha kama imengia mara hamna, wameenda Bodi ya Mikopo, mara leo wamegoma, watasoma saa ngapi? Hata hawa Walimu hawata-*enjoy* kufundisha ile fani yao. Kwa hiyo, naomba Serikali ihakikishe mwaka huu hakuna mgomo wowote utakaotokea kwa sababu eti mtoto amekosa pesa ya kwenda shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwa muda wangu umebakia kidogo, naomba kuzungumzia *National ID*. Sielewi hili jambo limechukuliwa namna gani kwa

sababu naona kama bado linapigwapigwa danadana, ni jambo la msingi katika Taifa letu. Katika nchi zilizoendelea, vitambulisho ni muhimu. Sasa hivi sisi tumesema eti Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, juzi tu kuna mtu kapewa kiwanja wala sio mzawa, kwa hiyo, *National ID* ni nzuri kwa sababu kila Mtanzania atajulikana ni nani, yuko wapi na anafanya nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata katika ulipaji wa kodi, itakuwa ni rahisi, wananchi wale wanaoambiwa wakakope kwenda kwenye mabenki sio lazima apeleke nyumba atakuwa anajulikana yuko kwenye *data base*. Wanawake vijijini kule na wakulima wetu vitawasaidia. Kwa hiyo, naomba suala hili lisimamiwe kwa makini liendelee kwa haraka zaidi.

Mheshiwa Mwenyekiti, naomba kuunga hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofî*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Martha Mlata kwa mchango wako, sasa kabla sijamuita Idd Azzan, niombe kukabidhi kwanza Kiti kwa Mheshimiwa Spika.

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alikalia Kiti*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama kawaida, nashukuru sana Wenyeviti wanapotusaidia. Namshukuru sana Mheshimiwa Job Ndugai, kwa muda wake hapa nadhani mambo yalikuwa shwari, namshukuru sana. Tunaendelea, sasa ni Mheshimiwa Idd Azzan.

**MHE. IDD M. AZZAN:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia katika bajeti hii ya ofisi ya Waziri Mkuu. Nami niungane na wenzangu kupongeza kwa dhati kabisa bajeti hii kwa sababu imegusia maeneo mengi sana.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza mchango wangu, niseme jambo moja. Katika wachangiaji ambao wamepita nafasi ya kuchangia na hasa wenzetu wa Upinzani, mara nyingi walikuwa wakihoji miaka arobaini na nane tangu tumepata uhuru kana kwamba nchi hii hakuna kilichofanyika kwamba Serikali hii ambayo inaongozwa na Chama cha Mapinduzi kama vile hajifanya kitu, sijui wanalinganisha na nchi gani kwa sababu zipo nchi ambazo tulipata nazo uhuru pamoja hebu waziangalie zilivyo. Somalia wamepata uhuru lakini angalia wakoje hivi sasa. Rwanda, Burundi wamepata uhuru lakini anagalia wakoje?

Mheshimiwa Spika, lakini niseme tu Serikali yetu tangu uhuru yapo mambo mengi sana yamefanyika lakini kubwa zaidi la kujivunia ni hili la amani na utulivu ambavyo viro katika nchi yetu. Kwa hiyo, wanapajaribu kubeza wasiwe kama yule mtoto ambaye anamtukana baba yake kwa kusema baba yangu mlevi. Unaposema baba yako mlevi, unatakiwa umshukuru pia angalau kwa kukuzaa kwa sababu kama sio hivyo usingetokea hapa duniani, kwa hiyo, mengi sana yametokea.

Mheshimiwa Spika, ilani ya uchaguzi imetekelozwa, takribani Wabunge wengi ambao wamesimama hapa wameelezea. Zile ahadi za Rais wengine walizisema ziko mia na arobaini na nne sijui, lakini niseme nyingi zimetekelozwa tena kwa kiasi kikubwa sana na hazikubagua, yapo Majimbo mengine ni ya Wapinzani na wenyewe walismama hapa jana kusifia na kupongeza kwamba kwao kumejengwa barabara nzuri, hizo ni ahadi za Rais, kwa hiyo, zimetekelozwa. Mheshimiwa Rais, amefanya kazi kubwa sana katika ahadi zake ambazo ameahidi nyingi amezitekeleza, kama bado, ni chache sana na bado ana nafasi ya mwaka na nusu tena kumalizia. Kwa hiyo, tufike mahali tuseme ukweli. Tuna macho basi tuone, kama huna macho basi hata husikii, watu hawakuambii? Kwa hiyo, ifike mahali tusema kwamba Rais wa Awamu ya Nne amefanya mambo mengi na mazuri na lazima tumpe sifa yake.

Mheshimiwa Spika, aliahidi suala la ajira na wakikaa wanazungumza, ooh, aliahidi ajira mbona hamna, Rais hakuahidi ajira kwa Watanzania wote, aliahidi ajira kwa watu milioni moja na asilimia kubwa ya hao tayari wapo kwenye sekta mbalimbali. Kwa hiyo, niseme tu kwamba ahadi za Rais zimetekelozwa tena kwa kiwango kikubwa sana.

Mheshimiwa Spika, nichuke nafasi hii pia kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, amekuwa ni msaidizi mkubwa sana wa Rais kwa kazi ambazo amezifanya. Mambo mengi yamefanyika na amesimamia vizuri sana, hongera sana. Hata Mawaziri hao, Waziri ndio wasaidizi wa Mheshimiwa Rais na wenyewe nao wamefanya kazi kubwa sana, lakini ajabu inatokea watu mwanalaani wanafanya hivi lakini mimi nawaambia Mawaziri fanyeni kazi wala msiwe na wasiwasi na hizo laana mnazopewa kabla hazijafika kwenu, zitawafikia hao wanaowalaani kwa sababu kazi kubwa mmeefanya na wengine wanahoji hata magari mnayotumia, oh, Mawziri wanatumia ma-V8, wangetumia gari gani? Wapande Bajaji? Hebu jiangalie na wewe Mbunge unayesema neno hilo kabla ya Ubunge ulikuwa na kitu gani au ulikuwa unatumia gari la aina gani? Wengine tulikuwa tunatumia *Mark Two* lakini sasa tuna Maprado, mbona hukununua Bajaji? Kuwa na gari nzuri maana yake ni ya kufanya za watu, nchi hii ni kubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kabla sijasahau, pamoja na kumpongeza Rais kwenye kazi anazozifanya, nimpongeze sana kwenye suala la michezo. Mheshimiwa Rais amefanya kazi kubwa sana kwenye michezo lakini nichukue nafasi hii kwa makusudi kabisa kumpongeza Rais wa TFF, Ndugu Leodiga Tenga, amefanya kazi nzuri, michezo wa mpira wa miguu sasa hivi kiwango kimepanda, na niseme wazi Ndugu Tenga siyo mnafiki, siyo jeuri, wala hana kiburi, ni mchapa kazi mzuri.

Mheshimiwa Spika, suala la kuchukua kombe, kombe hile ni moja, tunashindania watu wengi sana na unapoingia kwenye michezo hii, lazima ukubali kuna kushindwa pia. Kwa hiyo, inapotokea tumeshindwa, ni suala la kujipanga tena vizuri ili tuweze kushinda tena baadaye, lakini si kwamba tumekosa kombe basi ionekane kwamba soka halikupanda, michezo umepanda vizuri sana na Ndugu Tenga amefanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, nirudi kwenye kilimo kwanza, napongeza sana Serikali kwa kuamua kutoa kipaumbele kuhusu kilimo lakini nimuambie tu Mheshimiwa Waziri Mkuu, sisi wa Dar es Salaam hatulimi na hasa pale kwangu Kinondoni, lakini hicho chakula kwa asilimia kubwa kinaletwa Dr es Salaam na Mheshimiwa Waziri Mkuu hilo unalijua na hata kule kijiji ni kwako Kibaoni na vile Vijiji vya Usevya, Majimoto na Mamba *Vision* na wenywewe wanapolima huwa wanaleta vyakula vyao Dar es salaama kuja kuuza, vingi vinaletwa Dar es salaam na vingi vinaletwa katika soko la Tandale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi juzi ulitembelea Tandale pale sokoni, umeona hali ya Tandale jinsi ilivyo hairidhishi, Halmashauri ya Kinondoni haina uwezo wa kujenga mabanda pale, barabara unayoingia pale sokoni ni mbaya mno na wakati wa mvua haifai, sasa hivi vyakula vinavyotoka Mkoani, unaleta pale Tandale ndio soko kubwa ukija pale barabara hakuna, hebu tusaidie Kinondoni hata kwa kutukopesha angalau tujenge barabara ya kutoka pale Tandale sokoni kutokea kwa Tumbo ili iwe nzuri kwa kiwango cha lami. Magari haya yanayoleta mzigo pale huwa yanalipa ushuru, ushuru ule ukikusanya tutapata pesa nyingi sana ambazo hata kama ukiamua kutukopesha, tutaweza kukulipa hilo deni. Kwa hiyo, tunaomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na mwenywewe ni shahidi, soko la Tandale liboreshwa na barabara ambazo zinaingia na kutoka katika soko lile na zenyewe ziboreshwu kwa sababu ni soko ambalo wananchi wengi wanaolima huwa wanakuja kuuza bidhaa zao pale. Kwa hiyo, niombe sana Mheshimiwa Waziri Mkuu utusaidie kwenye suala hilo.

Mheshimiwa Spika, lingine ni tatizo la maji. Tunalo tatizo la maji Dar es salaam hususani katika jimbo la Kinondoni, Mheshimiwa Waziri Mkuu ni shahidi kwa sababu mitaa ya Ananasifu anajua. Kabla ya miaka miwili nyuma, mwaka mmoja na nusu nyuma maji yalikuwa yanapatikana vizuri sana lakini hivi sasa maji imekuwa ni tatizo kubwa sana na chanzo ni kwamba bomba lile ambalo linapeleka maji Ananasifu la nchi sita limekwenda kuunganishwa tena na bomba la nchi nane kuchukua maji yale kuyapeleka kwenye kiwanda cha bia. Wananchi wetu wakosa maji, maji yale yanapelekwa kwenye kiwanda cha bia, mnataka sisi wote tuwe tunakunyuwa bia iwe ndio maji yetu? Kwa hiyo, niombe kabisa, Mheshimiwa Waziri wa Maji, yuko hapa tuangalie ni jinsi gani ya kufanya kuondoa tatizo la maji katika jimbo la Kinondoni. Nimezungumzia Ananasifu lakini tatizo la maji lipo maeneo mengi, ukienda Mgomeni, Tandale, Mwananyamala, Ndugumbi, kote huko kuna matatizo ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishukuru sana Serikali kwa mradi mkubwa sana wa maji waliouweka kutoka Ziwa Victoria kwenda Kahama. Ni mradi mkubwa sana ambao umetumia pesa za ndani, za Tanzania kutengeneza maradi ule zaidi ya bilioni mia mbili na hamsini zimetumika. Hivi kweli Dar es Salaam hamuoni kwamba kuna haja sasa kutenga pesa za ndani kuhakikisha maji Dar es Salaam yanapatikana? Kwa sababu miradi yote ambayo mnaipanga Dar es Salaam, mnaweka kwa fedha za wafadhili ambazo hazipatikani matokeo yake tunaendelea kutaabika na ukosefu wa maji katika jiji la Dar es Salaam. Mlituahidi bwawa la Kitunda litajengwa kwa fedha za wafadhili, hazikupatikana na halikujengwa na tunaendelea kukosa maji. Kwa hiyo, niombe Mheshimiwa Waziri

Mkuu, kwenye hili tatizo la maji la Dar es Salaam, hebu tuangalie pesa za ndani tuone tunafanyaje.

Mheshimiwa Spika, tumejapata maji mengi sana ya kisima pale Kimbiji. Yanatakiwa yasambazwe sasa Dar es salaam lakini utasikia, ooh, tunatafuta hela za wafadhili. Hivi hawa wafadhili mpaka lini? Miaka mingapi imeshapita hivi sasa hela ya wafadhili hazipatikani? Kwa nini tusitenge makusudi kabisa pesa za ndani ili ziweze kuleta maji kwa wananchi wa Dar es Salaam ili na sisi angalau tukioga tuoge tukiwa tumesimama maana tunatafuta maji ya kwenye ndoo ndio tunaoga sasa tuoge angalau maji yanatoka kwenye bomba la mvua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunalo tatizo la Hospitali, tumeahidiwa hapa na nitaomba kwenye bajeti itakapowasilishwa na Wizara ya Afya watueleze, Dar es Salaam tuna matatizo makubwa sana ya hospitali. Dar es Salaam hatuna hospitali ya Mkoa, wananchi wetu wanapata tabu. Tuliahidiwa hapa kwamba *CCBRT*, ndio itakuwa hospitali ya Mkoa lakini mpaka leo hakuna kinachoendelea, kwenda kutibiwa pale, ni lazima ulipe pesa, lakini wakati huo huo, Serikali tayari imeshaanza kulipa wafanyakazi wa *CCBRT*. Lakini huduma kwa wananchi wetu, zinakuwa haziridhishi na wananchi wetu wanaendelea kutaabika na suala hili la hospitali maana Mwananyamala kumeja, Amana kumeja, Temeke kumeja. Dar es Salaam sasa hivi ina wakazi zaidi ya milioni tano, kwa hospitali hizi tatu hazitusaidii. Kwa hiyo, tunaomba hili la hospitali tupate maelezo ya kutosha na ni lini wananchi wa Dar es Salaam watapata Hospitali ya Mkoa.

Mheshimiwa Spika, tuna tatizo la mifereji ya maji hasa wakati wa mvua. Wakati wa mvua Dar es Salaam inakumbwa na mafuriko makubwa sana. Mitaa ya Kinondoni Shamba, Kinondoni TX, kulijaa maji kupitiliza hata njia ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu ambayo huwa anapita kwenda Kanisani, kulijaa kupita kiasi. Sasa niombe basi kwa sababu Halmashuri ya Kinondoni inaonekana wazi uwezo wa kukabiliana na suala hili ni mdogo na kwa sababu ya ukosefu wa pesa, Serikali itusaidie angalau basi kuboresha au kujenga mifereji kwa ajili ya kuondoa maji ya mvua. Hivi sasa tunazungumza kwa sababu jua linawaka lakini itakaponyesha mvua panakuwa hapakaliki kwa sababu wananchi wetu wanataabika sana. Kwa hiyo, niombe Serikali iangalie kwa jicho la huruma suala hili la mifereji ya mvua wakati wa mvua katika jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kidogo *EWURA*, kweli tulitunga Sheria hapa na niwashukuru sana wanafanya kazi nzuri, wale wanaochanganya mafuta hivi sasa wanadhibitiwa vizuri sana. Lakini hebu tuangalie ile adhabu ya kuvifungia vituo hivi kwa mwaka mzima. Unapovifungia vituo hivi mwaka mzima, wapo wafanyakazi pale ambao wanakosa ajira lakini wapo baadhi ya wale wenye vituo wamekopa, wanashindwa kulipa madeni yao. Kwa hiyo, tujaribu kuangalia adhabu ambayo tunaweza tukawapa hawa wanaochanganya mafuta kwa sababu sasa tunawaadhibu waliokuwemo na wasiokuwemo. Wale ambao wameajiriwa hivi sasa wanakosa ajira wanakaa, wanasubiria mwaka uishe.

Mheshimiwa Spika, lakini baya zaidi, kuna wale ambao wanapigwa faini, amechanganya mafuta anapigwa faini milioni 3.0 lakini yale mafuta yanafanywa nini?

Yanaachwa yaendelee kuuzwa. Kwa hiyo, inaonekana kwamba baada ya kupata milioni 3.0 mafuta yanaendelea kuuzwa wakati yamechanganywa. Mimi nafikiri, ifike mahali yale mafuta ambayo yamechanganywa basi uamuzi uchukuliwe ama kuyamwaga, ama kufanya kitu chochote Kuliko kuchukua faini ya milioni 3.0 halafu unawaachia waendelee kuyaiza, wanaendelea kutuathiri na kuharibu vyombo vyetu ambavyo tunavitumia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kupongeza tena Awamu ya Nne, kwa kazi ambazo wamezifanya kwa kutekeleza Ilani ya Uchaguzi na sina wasiwasi, Wabunge ambao tumo ndani ya Bunge hili, wengi tutarudi kwa sababu tumeonyesha dhamira ya wazi kabisa ya kuwatumikia wananchi wetu na kazi kubwa imefanyika. Waheshimiwa Mawaziri, fanyeni kazi tunawategemea sana. Haya yote, ambayo yanapangwa yanawategemea ninyi. Bajeti nzuri hii ambayo imetangwa na Serikali itakapokosa usimamizi mzuri, utekelezaji ukiwa mbovu maana ya bajeti hii haipo. Kwa hiyo nina hakika mtakaposimamia vizuri na utekelezaji utakavyokwenda vile ambavyo ilivyokusudia, yale ambayo yamewkwa kwenye bajeti hii yatatekelezwa kwa ufanisi mkubwa sana na wananchi wetu kwa kweli watakuwa wamefaidika kwa kiasi kikubwa sana. Maisha bora kwa kila Mtanzania inawezekana na kweli imeonekana wazi inawezakana. Unapojenga barabara ya kutoka Mwanza mpaka Mtwara, unatembea kwa *taxis*, inatusaidia katika maisha bora kwa sababu maisha bora si kwamba utaletewa pesa nyumbani kwako. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, zipo nchi ambazo zimetutangulia, wako Waingereza ambao walitutawala hapa, pamoja na maendeleo yao, huwezi kwenda kwao ukakuta wananchi wamekaa tu ama Serikali inatoa pesa kuwapa wale wananchi, ni lazima wananchi wafanye kazi, ni lazima tufanye kazi ndiyo tunapata maisha bora. Ilani imetekelizwa kwa sababu mambo mengi yaliyoahidiwa yamefanyika.

Mheshimiwa Spika, niungane na wenzangu kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja, ahsante sana. (*Makofi*)

## **HOJA YA KUTENGUA KANUNI ZA BUNGE**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, zimesalia dakika chache sana lakini hata hivyo ninaona kwa matangazo nitakayotoa na hatua zitakazofuata zinaweza kuchukua kama dakika tano au saba hivi, kwa hiyo, itakuwa imepita ule muda wa kanuni. Sasa namwomba Waziri wa Nchi, aweze kusimama na kutoa hoja ili tuweze kutengua Kanuni husika, tukae kidogo ili tumalize shughuli za leo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, ili kukamilisha shughuli muhimu za wakati huu, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako liendelee hadi shughuli ambazo zinatakiwa kufanywa sasa hivi zikamilike.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuiliwe*)  
(*Hoja iliamuliwa na kuafikiwa*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja hiyo imetolewa ya kuendelea na shughuli kwa muda mfupi tu ili tumalize shughuli za mchana huu, hoja imetolewa na kuamuliwa.

Waheshimiwa Wabunge, ninayo matangazo matatu, la kwanza linahusu suala la Mheshimiwa Selelii na hoja yake kwamba inawezekana barabara ya Chalinze - Segera fedha zilianza kutumika kabla hata ya kuidhinishwa. Nimechelewa kutoa uamuzi na hata leo siwezi kuutoa kwa sababu Mheshimiwa Mbunge alikwenda katika Maktaba ya Bunge, akatafuta vitabu vya makadirio vya mwaka 2006/2007 na 2007/2008 na 2008/2009. Serikali kwa upande wake, nayo ikanipa taarifa kwenye vivuli za hiyo hiyo, sasa nakala ya Serikali zinaonyesha kwamba fedha zilitengwa, vitabu vilivyopo Maktaba ya Bunge vya Makadirio hususani Kitabu cha Nne cha Maendeleo, zinaonyesha sifuri (0) kwa miaka husika, ndiyo maana kumekuwa na utata, sasa tunafanyaje?

Waheshimiwa Wabunge, leo nimeagiza kwamba baada ya kuonana pia na Waziri wa Miundombinu na Katibu wa Bunge, waangalie mtiririko mzima wa vitabu, mtaona kwamba mathalani mwaka huu imebidi marekebisho yafanywe, kwa hiyo, mtu aliyechukua kitabu cha Kamati tulivyokutana mwezi Mei Dar es Salaam hakina usahihi kwa sababu kwa baadhi ya sehemu kimebadilika. Kwa hiyo, limebaki hilo tu, kulinganisha hivyo vitabu na baada ya hapo basi nitatoa ufanuzi na uamuzi wangu kuhusu kilichotokea, hii ndiyo sababu lakini wenzetu wauza magazeti wanasesma Spika sijui anapambana na Serikali, vitu vya namna hiyo ni vya kipuuzi.

Waheshimiwa Wabunge, hii ni Serikali yetu, mimi siwezi kupambana na Serikali, nipambane na Serikali kutafuta kitu gani, ni jambo tu la uhakika kwa sababu linalotamkwa hapa likija kugundulika kwamba Spika naye alilolisema hakulifanyia utafiti, tunaweka msingi mbaya sana wa utawala wa Bunge, ndiyo maana imenichukua muda, kwa hiyo tuwe na subira hilo litakwisha hivi punde.

Waheshimiwa Wabunge, jana kulitokea tukio la pili sasa la Mheshimiwa Mbunge mmoja kukaidi maelekezo ya Kiti, hili ni jambo ambalo halikubaliki kwa sababu Kanuni zetu zinavyosema ni kwamba, kama hukubaliani na Kiti, basi eleza hivyo na ukate rufaa siyo ubishane tu hapo na kusema mimi sitaki. Nachunguza tukio hili na pia nalazimika sasa nitoe Mwongozo mzuri tu wa lugha Bungeni kwa Mujibu wa Kanuni ya 64, kuna kutokuelewana kwenye hili, wengine wanasesma fulani ametoa lugha ya kashfa, mwengine hivi. Katika mizania ya kupima uhuru kamili wa Mbunge chini ya Katiba Ibara ya 100 na kuangalia kwamba lugha humu haiwezi kuja kuleta matatizo, ni jambo ambalo limeshughulikiwa na Mabunge mengi sana, sasa inabidi nilitolee mwongozo ili sisi wote tunaokaa hapa, tunapotoa uamuzi uwe ni wa aina moja, kwa hiyo hilo nalo nitalitolea uamuzi wiki ijay.

Waheshimiwa Wabunge, jambo la mwisho, ni ratiba ya vikao vilivyobaki katika Mkutano huu, Kamati ya uongozi imeketi leo kwa dharura na imezingatia mambo yafuatayo:-

Kwanza, kesho jioni saa kumi na moja, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma, atatoa hotuba ya Makadirio ya Bajeti kwa mwaka 2009/2010, ukiifuata hii ratiba maana yake hii itakuwa ni nusu siku ni ngumu hiyo.

Pili, tumezingatia rai ya Waheshimiwa Wabunge kwamba Wizara ya Nishati na Madini kupewa siku moja haitoshi.

Tatu, tumezingatia pia rai kwamba wakati wowote Muswada wa *CDCF* utaiva, ukishaiva tunauweka wapi sasa.

Kwa kuzingatia hayo, Waheshimiwa Wabunge, Kamati ya Uongozi, tumependekeza kwenu kwamba baadhi ya siku za Jumamosi zitumike kwa vikao vya Bunge na itatusaidia kwa sababu hata hivyo tulikuwa tunazitumia kwa semina lakini baada ya rungu la *PM*, semina sasa zimekauka, kwa hiyo, bora tutumie tu muda vizuri angalau nusu siku au zaidi na niseme tu kwa lugha ya Kibunge kwamba itifaki yote ya mikutano hiyo imezingatiwa. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, ili tufanye hivyo, inabidi kanuni husika iweze kutenguliwa kutuwezesha kuanzia Jumamosi hii, kesho kutwa, tuweze kukaa kumalizia makadirio ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na baada ya hapo ikishaiva *CDCF* tutakaa Jumamosi moja, tumelenga kwenye tarehe kumi na moja hivi Julai, tuimalize, Nishati na Madini tarehe 24 tutaendelea mpaka 25 ambayo nayo ni Jumamosi ili tumalize masuala ya madini, basi vyovyote itakavyojitokeza ili tuweze kuwa na lengo letu la kumaliza shughuli za Bunge tarehe 31 Julai basi tutazitumia hizo Jumamosi kwa njia hiyo.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, namwomba sasa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, aweze kutusomea Azimio la Kutengua Kanuni ili kuwezesha haya niliyoyatangaza.

## AZIMIO LA KUTENGUA KANUNI ZA BUNGE

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa maelezo ya hoja ya kutengua Kanuni za Bunge kwa mujibu wa Kanuni ya 150(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Mwaka 2007.

**KWA KUWA** kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Vikao vya Bunge hufanyika siku zote za wiki isipokuwa siku za Jumamosi, Jumapili na siku za mapumziko;

**NA KWA KUWA** Mkutano huu wa 16 wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania unaoendelea, umepangwa kufanyika kwa siku 38 ambapo Wizara zote zimepangiwa siku moja moja ukiondoa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika na Wizara ya Miundombinu ambazo bajeti zao zitajadiliwa kwa siku mbili;

**NA KWA KUWA** siku za Mkutano huu wa 16 wa Bunge unaoendelea, haziwezi kuongezwa kutokana na sababu zilizoainishwa tarehe 11 Juni, 2009 wakati niktoa hoja ya kutengua Kanuni mbalimbali za Bunge;

**KWA HIYO BASI** Bunge sasa liazimie kwamba kwa madhumuni ya kukamilisha shughuli zote zilizopangwa kwa ajili ya Mkutano huu wa Kumi na Sita, Kanuni ya 28 (15) inayoelekeza kwamba Vikao vya Bunge vitafanyika siku zote za wiki isipokuwa Jumamosi na Jumapili au siku za mapumziko, sasa itenguliwe na badala yake utaratibu ufuatao utumike.

*"Iwapo shughuli zote zilizopangwa kwa ajili ya kikao hazijamalizika, Spika atalihoji Bunge kuhusu hoja ya kuahirisha Bunge au Kikao cha Bunge na baada ya hoja hiyo kuafikiwa basi ataahirisha kikao hicho hadi siku inayofuata hata kama siku hiyo itakuwa ni Jumamosi, isipokuwa kwamba siku hiyo ya Jumamosi hakutakuwa na kipindi cha maswali."*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)  
(*Hoja iliamuliwa na kuafikiwa*)

*(Azimio la Kutengua Kanuni zilizotajwa Lilikubaliwa na Bunge)*

**SPIKA:** Ahsante sana Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, kama Kanuni inavyohitaji, ametusomea hoja inayotokana na Azimio ambalo amelitolea maelezo kwamba tutengue Kanuni ya 28 ili inapobidi tukutane hata Jumamosi, hoja hiyo ameitoa na imeungwa mkono.

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Mwongozo, Mheshimiwa Yahya!

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Bunge hili ni Bunge la nchi mbili ambalo ni Bunge la Jamhuri ya Muungano na katika Wizara zetu hizi, kuna Wizara ambazo zinahusika na Muungano, mmefikiria vipi katika kuchangia ili nafasi zote mbili za

Muungano ziweze kupata nafasi na kwa kuwa zote zimepewa siku moja moja, naomba mwongozo wako.

**SPIKA:** Kwanza Mheshimiwa Yahya Issa, umekiuka Kanuni, kwa sababu wewe unajaribu kutanguliza shughuli iliyombele yetu, tuijadili leo. Kwa hiyo, hatuwezi kuijadili leo, tutatoa maelekezo tunapokaribia. Jambo hili si jambo geni, tumewahi kulifanya hata siku za nyuma, itategemea wachangiaji na kwa hakika Azimio hili ambalo mmelipitisha leo linaweza kusaidia katika hali kama hiyo, kwa sababu mmetupa unyumbulifu kidogo sisi tulipo huku kuweza kupanga mjadala wowote ambao utakuwa unaendelea ukaweza kwenda siku nyingine ambayo pengine tungebanwa na Kanuni, isingewezekana.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, ni hivyo. Nashukuru kwa hayo na nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa yote ya leo.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Serekamba, Mwongozo!

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Pamoja na kwamba leo tunajadili namna ya kufanya kazi vizuri katika majadiliano yetu, nilikuwa na jambo dogo ambalo niliomba nalo huko mbele tuenze kulifikiria.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Elimu, ni Wizara muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu, tuna Elimu ya Juu na Elimu ya Msingi na Wizara hizi huko nyuma zimekuwa ni Wizara mbili na siku zote zilikuwa zinapewa siku tatu, kwa maana ya Elimu ya Juu siku moja, na Elimu ya Msingi siku mbili, lakini sasa Wizara hii kubwa inafanywa kuwa siku mmoja na elimu ni jambo kubwa sana kwa maendeleo ya nchi yetu, ninaomba tafadhali hili nalo tulifikirie.

**SPIKA:** Majibu yangu ni yale yale kwamba siku itakapokaribia, tutaona, kwa sababu mara nyingine tunashangaa, mathalani wiki iliyopita waliouliza maswali kwa Waziri Mkuu, walikuwa ni watano tu, lakini tulianza mwanzo na orodha ya watu ishirini mpaka inabidi tuwaache, uendeshaji wa shughuli hizi unategemea hali halisi lakini ni lazima tupange awali, tukifika hapo na tukaona ile orodha inatisha kabisa tutajua la kufanya na ndiyo maana tumeomba nafasi hii ili baadhi ya Wizara ziweze kwenda. Mtaona hata Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, ilikuwa imepangwa pamoja na Wizara ya Masuala ya Afrika ya Mashariki, lakini kwa hili mlilotukubalia rasimu yangu hapa inaonyesha sasa Wizara ya Afrika Mashariki tutajadili siku ya Jumamosi tofauti kabisa na Wizara ya Mambo ya Nje, kwa hiyo tumekwishapata hapo nusu siku ya kuweza kufanya kazi.

Waheshimiwa Wabunge, huo ndiyo utaratibu.

Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru, sasa tumeshapitiliza muda, kwa hiyo, nasitisha shughuli za Bunge hadi hapo saa kumi na moja jioni.

(*Saa 7.11mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni*)

(*Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia*)

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, majadiliano yanaendelea na bila kupoteza muda, mchangiaji wetu wa kwanza ni Mheshimiwa Maria Hewa, atafuatiwa na Mheshimiwa Shoka Khamisi Juma. Mheshimiwa Maria Hewa, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Mwanza.

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nipende tu kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuniweka hai mpaka wakati huu wa jioni ili niweze kutoa mawili, matatu, katika michango yangu ambayo nimejiandaa, kwa maana ya kuzungumzia vitengo mbalimbali ambavyo vinawagusa wananchi hasa wa Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende kutoa shukrani zangu za pili kwa Hotuba ya Waziri Mkoo, pamoja na Manaibu wake, kwa sababu hotuba ndio dira ya utekelezaji mkuu wa shughuli zote za ndani ya nchi hii. Hotuba ikiwa mbovu, ujue kwamba basi na mambo mengine yote yatakwenda vibaya, lakini katika hotuba hii, ukweli jinsi ilivyoandaliwa nipende tu kusema wazi kwamba; ni nzuri, yenye mwelekeo na yenye dira. Kama kweli watendaji wataitekeleza kikamilifu, nchi yetu itatoka mahali ilipo kwenda kwenye maendeleo ya kikweli kweli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda pia nipende kutoa tu shukrani kwa sababu Wakuu hawa wa Mikoa huwa wanatoka Ofisi ya Waziri Mkoo. Sisi Mwanza tumeletewa Kandoro, ametoka Jiji anakuja Jiji. Hiyo ni sifa kwamba, alifaa kwenye Jiji kwa hiyo aendelee ndani ya Jiji. Tunamkaribisha kwa mikono miwili, Mheshimiwa Kandoro, anakuja kwa watani zake lakini ni watani wachapakazi. Mkoa wa Mwanza ni wachapakazi, kwa hiyo, ye ye ajisikie tu vizuri, akiwa na Wakuu wake wa Wilaya wapatao wanne nao ni wapya. Kwa hiyo, tunawakaribisha sana, Mkoa wa Mwanza hauna matatizo, sisi tunachotaka ni kazi na mnaujua Mkoa wa Mwanza ulivyo mzuri. Mkoa wa Mwanza una kila kitu, ukitaka dhahabu zipo, ukitaka almasi zipo, karibuni na tunamkaribisha kwa mikono miwili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huo huo labda niende tu moja kwa moja kwamba, kwa vile Serikali imekamilika sasa kwa maana ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa, niiombe tu Ofisi ya Waziri Mkoo kama nilivyoanza kwamba, Mkoo wa Mikoa ametoka kwenye Jiji anakuja kwenye Jiji, ombi letu la kila siku ni kuwa na Manispaa mbili Mwanza. Sasa alivyoviona Dar es Salaam ni vyema basi hebu visimikwe Mwanza kwa nia njema kabisa, lakini kama aliona kuna dosari labda leo tupatiwe majibu au wakati atakapokuwa anahitimisha basi muhusika ndani ya Ofisi ya Waziri Mkoo; tunapaswa kufanya nini ili kukamilisha zoezi hili? Tumekaa mpaka Kikao cha RCC

nacho kikapitisha; sasa ni nini ambacho tunapaswa tukifanye ili tutoke mahali tulipo kama ni ushauri utoke basi, kama ni nini tukisikie ili tuweze kupata Manispaa zetu hizo mbili? Pamoja na kwamba, mpaka sasa Mwanza ni nzuri, tunataka iwe nzuri zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, nataka niongelee suala zima la upande wa viwanda. Mwanza kama Mwanza, tunapenda maendeleo; siku zote huwa tunawaambia sisi nguvu ni bure. Sifa za Mkoa wa Mwanza ni watu wenye nguvu, watu wazito na ukimwona utajua huyu ana nguvu. Sasa kitu ambacho tunadhalilika nacho kila leo ni bei ya simenti kuwa juu sana na sielewi sababu. Leo ngoja niliseme na hili nitalisema hata mpaka mwaka kesho nitasema kama sitapata jibu sahihi wakati wa majumuisho ya Ofisi ya Waziri Mkuu; hivi kile kiwanda ambacho kiliandaliwa miaka ya nyuma kilikuwa kijengwe Kanda ya Ziwa, kama sikosei kilikuwa kiwekwe Shinyanga; kuna wakati niliuliza swali hapa nikaambiwa ni ukosefu wa malighafi; hivi kweli kila kiwanda nchini hapa kinajengwa kwa sababu kinazungukwa na malighafi iliyopo? Mimi siamini hata kidogo; wengine ardhi zao ni maskini, wasingekuwa na kiwanda.

Kwa Mwanza eti tunakosa malighafi ya kuweza kukamilisha hicho kiwanda cha simenti; tutaendelea kuishi kwenye nyumba za tope mpaka lini? Mfuko wa simenti Dar es Salaam ni kama nusu ya bei tunayoununua Mwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jamani hata kama ni kwa muda wa miaka mitano, wengine leo wameomba Chuo Kikuu hapa wakasema jiandaeni, sisi na eneo lipo; mtaendelea kutusema watu wa Kanda ya Ziwa hatutaki maendeleo, nimesema mwanzo na nguvu tunazo. Tunaomba hicho kiwanda sasa kianze kuzungumzwa, walau tufarijke kwamba sasa kimeanza kuzungumzwa. Tupate na sisi simenti kwa bei nafuu, tumechoka kuruka jamani. Ardhi tunayo, kila kitu tunacho. Kuna mzunguko wa fedha mzuri tu Mkoa wa Mwanza, lakini tununue nini ili na sisi tupate nyumba bora? Ofisi ya Waziri Mkuu, itufikirie na sisi wa Mwanza, tuwe maisha bora na huko ndiko kwenye *population* kubwa. Lilikuwa ni ombi langu kwamba, hebu tusije kuweka sababu ya malighafi, isombeni hata kwa malori au kwa treni. Uzuri sisi tunazungukwa na aina zote za usafiri; mkitaka kuleta kwa maji, treni au barabara inawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili ni suala la Kilimo Kwanza. Tunaongea suala la Kilimo Kwanza, kwa Mkoa wa Mwanza narudia, nguvu tunazo huhitaji kuuliza nguvu Mwanza. Leo tulikuwa wakulima wazuri wa pamba imeshindikana. Hebu kwa kifupi niseme, hivi bei ya mia tatu ni halali au katuona sisi ni wapole mno hatujui kulalamika, hatujui kufanya chochote? Tafadhali, naomba mtuunge mkono katika kilio hiki; toeni hapo mia tatu tupeni hata mia nne hamsini na ikibidi hata mia tano. Mkiona mia tano ni kubwa, basi tupeni hata mia nne hamsini, tutashukuru mno. Watu wa Mkoa wa Mwanza, wana shukrani na nguvu za kulima pamba zipo. Tunaomba sana mtupandishie bei ya pamba, ndicho kilio cha wakulima wa pamba, mtaona pamba italicimwa hata na maeneo ambayo ulitegemea wangelima mpunga watalima pamba. Wakulima wa pamba ni wazuri na kilio chao ni kupandishiwa bei. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu ni barabara. Jamani Serikali ya Awamu ya Tatoo, imejitahidi mno kuunganisha barabara hizi nchi nzima. Tunamshukuru sana Rais. Tunatoka Dar es Salaam tukiwa kwenye lami, kilometra 40 tu zimebaki unaanza vumbi kuingia Mwanza. Lile eneo la Ilula mpaka Mabuki kuna kosa gani kila mwaka lina vumbi? Mtu anatoka amejipamba vizuri, amevaa suti yake, ameniga tai kama ulivyoniga wewe Mwenyekiti, ukifika pale tai inajaa vumbi. Ninahisi huyo mkandarasi anapewa hela kidogo. Fanyeni upembuzi yakinifu mnaousema kila leo ili hela ipatikane vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni aibu kutoka Dar es Salaam eti uko tu kwenye lami tena safi, mnakaribia kuingia Mwanza, tunaanza vumbi, hivi ni kweli! Kuanzia Mwanza mpaka Musoma, kuna lami nzuri tu. Hebu litembeleeni eneo hilo. Waziri wa Miundombinu; naogopa kutaja jina, tuliambiwa tusitaje majina. Tutakushukuru kama utatuwekea lami katika eneo lile. Hapana, naogopa naweza kuchukuliwa hatua. Mwisho, tunaendelea kumshukuru Rais, kwenye Taarifa ya Waziri Mkuu, vivuko havikutajwa vyote.

Sisi Mwanza tunamshukuru mno Rais, tuna vivuko vya uhakika. Juzi tumepata MV Kome, ambayo ni *ferry* mpya, haikutajwa kwenye kitabu hiki cha Waziri Mkuu. Hivi Watendaji mna nia gani na Mwanza na Ofisi ya Waziri Mkuu? Sisi tunatoa shukrani hata kama hamkuandika, tunavijua vivuko hivi. Kwa hiyo, tunamshukuru sana Rais kwa kutuletea vivuko hivi; tuna MV Sengerema, MV Kome, MV Misungwi, ona vyote hivyo. Sisi tukimsikia Kikwete anakuja Mwanza, hata kama ulikuwa unakula unaacha unakwenda kumwona kwa sababu anatutendea mazuri mno katika Mkoa wetu wa Mwanza. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunazidi tu kumshukuru Mheshimiwa Kikwete, kwa sababu ametutendea mema.

Baada ya hapo, ninakumbushia ile barabara ifanyiwe upembuzi yakinifu itengenezwe ili lami itoke Dar es Salaam mpaka Mwanza. Bei ya pamba irekebishwe.

Baada ya maelezo yangu hayo, nashukuru kwa kunisikiliza, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nami nakushukuru Mheshimiwa Maria Hewa, umesema kwamba, Usukumanzi nguvu ni nyingi sana. Nilitaka kukumbushia tu, nguvu ziende na maarifa pia. Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, atafuatiwa na Mheshimiwa Sijapata Nkayamba. (*Kicheko*)

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Awali ya yote, nachukua fursa hii, kwanza, kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujalia kukutana jioni hii tukiwa wazima na salama.

Baada ya hapo, napenda vile vile nichukue fursa hii, nikushukuru na wewe kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kutoa maoni yangu japo kidogo. Nilikuwa nimeshakata tamaa, lakini tunatakiwa tusikate tama, unaweza ukaipata bahati wakati wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami kama wenzangu, nichukue fursa hii, kumshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa namna anavyotekeleza kazi zake ingawa jana jioni hapa palizungumzwa na Mbunge mwenzangu, sitaki nimirage jina kuwa, Mheshimiwa Waziri Mkuu ni mpole sana na anamwomba aongeze ukali kidogo. Sisi tunamwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, asiongeze ukali, abakie kama alivyo, maana akiongeza ukali atabadilika atakuwa si yeze tena, atakuwa mwingine. Mheshimiwa Waziri Mkuu, wewe ni rafiki yangu, nakuomba utulie hapo hapo ulipo, *keep it up*, usibadilike. Ukibadilika utakuwa si wewe tena, atakuwa ni mtu mwingine. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, vile vile napenda nimpongeze Waziri wa TAMISEMI, anashirikiana na sisi kikamilifu. Mimi kipindi kilichopita, nilikuwa ninajengewa Ofisi kule katika Jimbo langu la Micheweni. Mheshimiwa Waziri, wakati wowote ukimpigia simu yuko tayari na anakuelekeza na anasimamia mpaka anahakikisha jambo linakamilika. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, ninakushukuru sana.

Baada ya shukrani hizo, ninaongeza kidogo hapo penye sehemu ya Ofisi ya Mbunge. Ofisi ile tayari imekamilika, lakini sasa inahitaji samani za kuhamia kwenye ofisi. Kwa hiyo, ninakuomba ufanye kama unavyoweza ili samani zile zitoke katika fungu lako, yaani kwenye Ofisi ya TAMISEMI, usije ukaniambia kuwa nipewe kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, sijui kwa Mkuu wa Mkoa, sijui kwa nani, huko sitapewa na ofisi itakuwa haihamiliki, itakuwa ni jengo tu lipo pale. Kwa hiyo, naomba ikifika wakati wa majumuisho, nielekezwe wapi nitapata samani za kuhamia kwenye ofisi ile. Baada ya hapo, bila kusahau, natambua kuwepo kwako Mheshimiwa Naibu Waziri. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea kuchangia, kwanza, nataka nianzie kwenye Tume ya Uchaguzi. Tume ya Taifa ya Uchaguzi ya Tanzania, mpaka hivi ninavyozungumza, haina ofisi yake ya kudumu, yaani hii ni Ofisi ya Tume ya Uchaguzi, inakaa katika majumba ya kukodi, Ofisi za Posta ndizo ilizokodi. Hivi kweli jamani, Tanzania tunapofikia tunajisifu tu watu tuna demokrasi na nini lakini hata nyumba ya Tume ya Uchaguzi hatumiliki, tunakodi! Mheshimiwa Waziri Mkuu, mimi ninawaomba hebu hili jambo liangalieni.

Tume ya Uchaguzi inatakiwa iwe na ofisi yake na iwe inajulikana rasmi kuwa hii ni Ofisi ya Tume ya Uchaguzi ya Tanzania. Tusende kwenye majumba ya kukodi au wengine hawajui ilipo, tunataka tujenge jengo la kisasa la Tume ya Uchaguzi ili demokrasia iweze kushamiri Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Tume hii ya Uchaguzi ina Sekretarieti Makao Makuu tu, huko kwenye Majimbo kunakofanywa chaguzi na kwenye Wilaya haina Sekretarieti; kwa hiyo, ninaiomba Serikali iiangalie hii Tume iwe na Sekretarieti kila mahali. Kwenye Majimbo na kwenye Wilaya, tusiazime watu kwenye Halmashauri za Wilaya kutufanya kazi zetu za Tume ya Uchaguzi. Kwa hiyo, ninafikiria suala hili limefika na mliangalie. Kila siku tunasema suala hili, lakini bado liko pale pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitoka hapo sasa nazungumzia Vyama vya Siasa. Tanzania vimesajiliwa Vyama vya Siasa 17, lakini baada ya kusajiliwa vinaachiwa tu

havina kazi ya kufanya. Hivi kweli vyama vya siasa tunavifanyia usajili halafu hatuvisaidii; vitaishi kweli vyama hivi? Kwa hiyo, nashauri kwamba, vyama hivi vya siasa vikishasajiliwa angalau viangaliwe vipewe ruzuku na serikali. Chama ukishakisajili unamwachia Mwenyekiti na Katibu wake basi. Hivi kweli chama hicho kitaishi? Kwa hiyo, ikiwa tumeamua Tanzania iwe nchi ya vyama vingi, vyama hivi vipataiwe ruzuku navyo viweze kujiendesha. Vyama vyenye Rais, Wabunge na Madiwani, vinapata ruzuku lakini vingine ambavyo havina viongozi kama hao wa kiserikali havipati ruzuku. Kwa hiyo, mimi ninatoa rai, tutenge asilimia mbili ya bajeti yetu tuiweke maalum kwenye vyama vya siasa. Vyama vilivyo na Rais, Wabunge na Madiwani, vyote vipewe ruzuku na vilivyokuwa havina viongozi kama hawa waliochaguliwa na wananchi navyo angalau vitengewe japo asilimia ndogo viweze kuishi. Chama kikishasajiliwa ndio basi kimesajiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile ikifika wakati wa uchaguzi, tunashindanisha matajiri na maskini. Vyama vingine havina uwezo, wagombea wao hawana uwezo na vingine vina uwezo, unashindanisha matajiri na maskini; hivi maskini atashinda kweli kwa tajiri? Kwa hiyo, natoa rai; ikifika wakati wa uchaguzi tuangalie tutatumia njia gani ilimradi na hawa wagombea wengine nao waweze kuwa na uwezo angalau wa kutembelea Majimboni wanakogombea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nizunguimzie kuhusiana na suala la Madiwani. Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, amezungumzia kuhusiana na suala la Madiwani. Nami ninaomba nimnukuu pale kwenye ukurasa wa 13, amezungumza mambo mengi lakini ninataka ninukuu mwisho tu anasema: “Aidha, posho mbalimbali za Madiwani, zimerekebishwa na hivi sasa Serikali inaendelea na mchakato wa kuwawezesha kupata unafuu wa kodi wanaponunua vyombo vya usafiri.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hawa Madiwani nao wanachaguliwa kwenye Uchaguzi Mkuu. Anachaguliwa Rais, wanachaguliwa Wabunge na Madiwani. Rais anapata mshahara, Wabunge wanapata mshahara, lakini Madiwani hawapewi mshahara wanapewa posho; kwa nini tunawafanyia hivi? Madiwani kama tulivyo sisi Wabunge nao wanachaguliwa na watu wale wale waliotuchagua sisi, isipokuwa wao wanachaguliwa na watu kidogo zaidi kuliko sisi. Kwa hiyo na wao tuisiwaterenge, tuwape mishahara, hii habari ya kuwa sijui kuna sheria inayozuwia kuwapa mishahara, sijui vipi, ninaomba tuiondoe iletwe sheria hapa Bungeni tubadilishe na wao walipwe mshahara kama tunavyolipwa sisi Wabunge, japo mshahara wao utakuwa mdogo, hautakuwa sawa na wa Wabunge, lakini na wao walipwe mshahara wasilipwe posho. Posho ina matatizo yake, posho ni posho, inaweza ika-stop wakati wowote. Kwa mfano, hivi sasa palikuwa na semina na makongamano na mambo mengine mengi; Mheshimiwa Waziri Mkuu ameyastopisha hakuna semina wala hakuna makongamano. Sasa mimi nasema, posho ni posho na mshahara ni mshahara, hawa wenzetu Madiwani na wao tuwalipe mshahara; wanachaguliwa kama tunavyochaguliwa sisi. (*Makofî*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwa ni uchungu wa kura na wao wanao! Jamani muda huu ndio dakika kumi tayari! Tayari kweli? (*Kicheko*)

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tano.

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa ninapenda hawa Madiwani nao tuwaangalie, tusiwaache kama tunavyowaacha. Muda unakwenda kasi kweli, mimi nalikiria niko dakika ya tano kumbe nimeshafika kumi. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumzie kuhusiana na suala la maafa. Suala la maafa Mbunge mwenzangu amelizungumza vyta kutosha, kuhusiana na boti iliyotoka Tanga kwenda Pemba, ambayo iliungua moto na kwa bahati mbaya kuna wananchi walipoteza maisha yao. Safari hii Serikali ilikwenda pale lakini ilichelewa kidogo. Kwa hiyo, ninawaomba mnapopata taarifa za maafa, m jitahidi kwenda haraka na ile Idara yetu ya maafa iliyopo isiwe Idara ya Kuratibu Maafa iwe ni Idara ya Kupambana na Maafa na ipewe kila kitu; iwe na helikopta, iwe na maboti ya kufuatia watu wanaozama kwenye bahari, iwe na magari ya kuzimia moto. Tuna Tume eti ni ya kuratibu tu; ukipata maafa unapeleka taarifa Polisi wasaidie halafu wale wanaratibu. Kwa hiyo, ninaona hii Tume ya Kuratibu haitoshi, tuunde Tume hasa ya kusimamia maafa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ninaomba kidogo ninukuu Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Nipo ukurasa wa 31, nataka kuzungumzia Sekta ya Sheria, kwa sababu kila anayesimama hapa anasema wengine wana macho hawaoni, hawasikii, sijui hawafanyi vipi! Sasa ninaomba muisikilize Ilani yenu wenye ambayo huwa tunaitekeleza. Naomba mnisikilize inasema: “CCM itazitaka Serikali ziendelee na hatua zinazoanza kuchukuliwa ili kuboresha Sekta ya Sheria kusudi nayo itoe huduma bora zaidi kwa jamii kusudi itoe huduma bora kwa jamii. Yatakayosisitizwa katika kipindi hiki ni pamoja na yafuatayo ...” Sasa mimi nilitaka mseme hili tayari mmeshalitekeleza au bado; kuzifanya marekebisho Sheria za Mirathi na zile zinazoonekana kuwakandamiza wanawake? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili ni la muda mrefu na limo kwenye Ilani; hivi kuna matatizo gani yanayokwamisha hadi sasa suala hili kuwa halifanyiwi marekebisho? Tayari Tume ya Kurekebisha Sheria imaeshafanya kazi yake, lakini bado halijatekelezwa! Hiyo ni nambari moja, naendelea nambari ya pili. Nambari ya pili inasema: “Kulipatia ufumbuzi suala la kuanzishwa kwa Mahakama ya Kadhi Tanzania Bara.” Suala hili linasubiriwa, watu wanalisubiri kwa muda mrefu. Mwaka jana tulipoulizia hapa, tuliambiwa kuwa, limepelekwa katika Tume ya Kurekebisha Sheria na tutapata jawabu wakati wowote Tume itakapomaliza kazi yake. Mpaka hivi sasa, Tume ya Kurekebisha Sheria kazi yake imeshamalizika, lakini bado hatujapata jawabu. Kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, atupe jawabu la suala hili. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisije nikapigiwa kengele ya pili, nashukuru kwa haya niliyoyazungumza, mengine nitayazungumza kwenye sehemu nyingine. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Shoka, Mbunge wa Micheweni na hasa kwa umahiri wako wa kuifahamu vizuri Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Baada ya Mheshimiwa Sijapata Nkayamba, atafuatia Mheshimiwa Maulidah Komu na Mheshimiwa Abbas Mtemvu, ajiandae. Mheshimiwa Sijapata. (*Makofi*)

**MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuweza kunipa nafasi. Kwanza kabisa, nampongeza Rais wetu, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuweza kutuona sisi wananchi tunaokaa Mkoa wa Kigoma, kwa kuufungua safari hii kwa sababu siku za nyuma tulikuwa tuko nyuma kabisa. Mheshimiwa Rais alisema kuwa, atakapomaliza madaraka yake 2015 Mkoa wa Kigoma utakuwa umefunguka na dalili zinaonesha. (*Makofi*)

La pili, napenda kumshukuru Waziri Mkuu, kwa sababu ni mtani wa Waha, kwa kweli anafanya kazi nzuri sana. Nampongeza kwa kwenda Kigoma kufungua Barabara ya Mwandiga - Manyovu; Barabara ya Chakele - Mwamgongo; na Barabara ya Mwandiga - Uvinza. Mheshimiwa Waziri Mkuu, tunakushukuru na tunakupongeza sana. Mungu akujalie na yule anayekuonea kijicho atangulie yeche. (*Makofi/Kicheko*)

**WABUNGE FULANI:** Amina.

**MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA:** Baada ya kusema hayo, hakuna kizuri kisicho na kasoro; wananchi wanaoishi pembezoni mwa Barabara ya Mwandiga - Manyovu, wako kwenye kiwango cha kuwekewa lami katika barabara yao. Siku moja niliwahi kumuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu swal la ana kwa ana kwamba, je, wananchi wale watalipwa?

Aliweza kunitoa kimasomaso na akawaambia kuwa, lazima wananchi hao watalipwa na sasa wameshalipwa. Mheshimiwa Waziri Mkuu, wale wananchi wamelipwa fidia ambayo ni ndogo sana na sasa hivi wanalamika, wanaiomba Serikali iwasaidie ufumbuzi mwengine wa kuweza kuwaongezea kiasi kingine kitakachokuwa kimebakia ili waweze kujenga nyumba za kisasa. Kwa mfano, mtu nyumba yake ina vyumba kama kumi, imewekewa mabati bandali saba, ina milango sita, madirisha kumi, imewekewa *cement*, imekarabatiwa kila kitu, lakini analipwa shilingi milioni 2.5, hiyo milioni 2.5 haiwezi kujenga nyumba. Kigoma mfuko wa *cement* ni shilingi 20,000, sasa uitoe pale Kigoma Mjini uipeleke mpaka Manyovu, itakuwa ni kiasi kikubwa sana; kwa hiyo, naiomba Serikali iangalie upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakwenda moja kwa moja Halmashauri ya Kigoma, kama wanansikia wanisikie na kama wanatioana wanione. Katika Halmashauri yetu ya Kigoma, nadhani wao ndiyo wanaosababisha hata Kigoma Kaskazini ichukuliwe na Wapinzani, kwa sababu katika ziara zangu, nilifika kijiji kimoja kinachoitwa Mayange, nikaenda moja kwa moja Kitongoji kinachoitwa Samwa. Kutoka Mayange mpaka Samwa, nilitembea kilomita nane, gari langu lilikuwa limefunikwa na majani mpaka juu haionekani; na hiyo barabara ilitengenezwa tangu mwaka 2005 mpaka leo haionekani kabisa, kinachoonekana ni matairi ya baiskeli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ina maana wale Viongozi wa Halmashauri, hawafuati Ilani ya Chama cha Mapinduzi, kama wangkuwa wanafuata, barabara ingetengenezwa. Vile vile katika ziara zangu, nikafika katika kijiji kimoja kinaitwa Chabitale, ambako kuna kitongoji kimoja kinaitwa Nkuruba; mwaka 1995 mwenge ulikwenda kufungua daraja pamoja na barabara. Tangu mwaka huo mpaka leo, daraja limebomoka, barabara haionekani, wale wananchi wakati wa kumpeleka mgonjwa hospitali, kwanza wakifika kwenye lile daraja wanapokezana kama vile wanapokezana maiti; mtu mmoja anateremka kwenye shimo wengine wanapanda mlimani, wakashateremka yule mgonjwa wengine tena wanapanda kule mlimani kwenda kupokea machela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unadhani itakapofika 2010 wale wananchi watakwenda kupiga kura kweli kwa sababu wameachwa nyuma wakati Ilani Chama cha Mapinduzi ndio inayotekeleza yote hayo? Kwa hiyo ndugu zangu, naona hawa Watumishi wa Halmashauri hawakitendei haki Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine nataka leo Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu aniambie; hivi wasafiri tunaokwenda Kigoma na wale wanaokwenda Mwanza; sisi Waha na Wasukuma, tunazidiana nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukifika Stesheni ya Dar es Salaam, unachukua chakula chako unakiweka kwenye ndoo ya *plastic*, ukishafika pale mlangoni unaambiwa vyakula vyote vitoe uviweke chini ukapime ile ndoo ya *plastic!* Mheshimiwa Waziri tutafika wapi? Sasa hivi tunakumbuka zama za Marehemu J. K. Nyerere, kwa sababu ukifika pale unaambiwa kitoe chakula kwenye ndoo uipime ile ndoo, ukishapima ndio unapita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasafiri hawatendewi haki, kwa sababu wale wanaokwenda na *third class* wana kilo zao, wanaokwenda na *second class* wana kilo zao na wanaokwenda na *first class* wana uwezo wakubeba hata ndoo nne, lakini wakifika pale wananyanyaswa vibaya sana. Hivi wanataka hii mishahara wanayoidai wao itoke kwenye ndoo au huyu Mhindi kwa nini anatunyanyasa sisi weusi, mbona siku za nyuma haikuwa hivyo? Tunataka Serikali iliangalie hilo. (*Makofi*)

Ukishapanda treni, usiku huo mtakula chakula kwa sababu wamepika wameweka kwenye behewa ambalo ni la *second class* na kinawekwa karibu na choo. Mimi nimechunguza wala si uwongo, minasema ukweli. Ukishakula chakula hicho cha usiku, mkiamka asubuhi hamnywi hata chai, mchana hamli chakula, mkishafika Tabora sasa lile treni linakatwa, kuna linalokwenda Mwanza na linalokwenda Kigoma; wa kwenda Mwanza wanapewa *buffet*, sisi tunaokwenda Kigoma hatupewi; huoni kama huo ni unyanyasaji?

Kwa hiyo, naomba Waziri wa Miundombinu, atuambie leo kwa nini anatutesa sisi wasafiri wa kwenda Kigoma? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sijapata, nakulinda endelea.

**MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nahamia afya; katika matembezi yangu hayo hayo nilikwenda moja kwa moja katika Kijiji cha Mayange, nikafika Kitongoji cha Samwa, ambacho kiko kilomita nane, kina watu karibu 2000 na kitu; wakaniambia Mheshimiwa Mbunge, tunakushukuru sana kwa kuja kutuona sisi hapa ni watoto yatima. Nikawauliza ninyi ni watoto yatima kwa vipi? Wakasema sisi Mheshimiwa Mbunge tuliyemchagua tunamwona kwenye picha tu! Nikasema sawa, mimi nitawapelekea matatizo yenu.

Sasa Mheshimiwa Waziri wa Afya, ninakuomba uwapelekee zahanati wale wananchi walioko Kitongoji cha Samwa, japokuwa kuna zahanati nyingine iliyoko kilomita nane, ambayo ipo katika Jimbo la Mheshimiwa Zitto, Kigoma Kaskazini. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea na Watumishi wa Halmashauri; katika Bunge hili hili nilimuuliza Waziri Mkuu swali la ana kwa ana, nikamwambia katika Halmashauri zetu kuna Watendaji amba ni Watendaji wa Kijiji na Watendaji wa Kata.

Tangu mwaka 2000 mpaka sasa hivi ninavyozungumza, wanadai mishahara yao na hela zao za uhamisho. Katika jibu lako la msingi, ukaniambia kuwa, utamwagiza Mheshimiwa Kombani, amwambie Mkurugenzi ili wale watumishi waweze kulipwa. Katika kufuatilia kwangu, sijasikia Mkurugenzi akiniambia kuwa alishapewa taarifa.

Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, hivi kwa nini hutaki kuwasaidia wanawake wenzio? Hutaki turudi Bungeni? Ninaomba basi kama bado hujampelekea taarifa Mkurugenzi, umpelekee ili wale watumishi waweze kulipwa. Naomba utusaidie na sisi wanawake wenzio. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inapoamua kwenda kupima mipaka ya vijiji, naiomba ifuate mipaka ambayo kijiji na kijiji inaifahamu. Sasa hivi katika Jimbo la Kigoma Kaskazini, Vijiji vya Kizenga na Nyamuhoza, hawapiki ugali ukaiva kuhusu mipaka. Mimi nilipokwenda kutembelea, walimieleza tatizo lao hilo la mipaka, nilishindwa kutatua nikawaambia nitakopokwenda Bungeni nitawasaidia; sasa ndiyo leo nawaulizia; je, ile mipaka yao ya zamani mnaweza mkairudisha ikawa vile vile? Tunaweza tukapoteza Chama cha Mapinduzi, kwa sababu Wapinzani ni wengi sana katika kijiji kile. Jamani wale Wapinzani ni wengi mno, hata ukienda ukawaambia jamani mnatakiwa sasa mjenge sekondari ya kijiji, wanakuwa ni wabishi sana. Wale Wana-CCM wanawaogopa, nikawaambia msiwaogope chukueni hatua, nendeni kwa Mkurugenzi au kwa DC, lakini Mwenyekiti wa Kijiji anawaogopa. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Serikali irudishe ile mipaka kama ilivyokuwa zamani ilivyopimwa na Serikali. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kuna wanafunzi waliomaliza *form four* mpaka *form six* tangu 2000 wako nyumbani, lakini kunapotokea ajira za Jeshi la Kujenga Taifa, Magereza, Jeshi la Polisi au shekta nyingine, unakuta wale wanafunzi wanaachwa, wanachukua wa miaka ya hivi karibuni, kwa mfano, waliomaliza mwaka 2007/2008. J e,

wale wanafunzi waliomaliza kuanzia mwaka 2000 - 2006 mtawapeleka wapi? Kwa kuwa hii ni Serikali ya Chama cha Mapinduzi, jamani wasaidieni vijana hao; ni wa kwenu na bila wao hatuwezi kupata kura za kutuleta hapa Bungeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi fani yangu ni mganga, nilianzia kazi katika kijiji kimoja kinachoitwa Simbo. Nimekaa pale kwa miaka 25. Nilikuta kuna Mahakama ya Mwanzo, sasa hivi ina miaka 12 haifanyi kazi. Hawa mahakimu wanaomaliza masomo yao huwa mnawapeleka wapi? Hamkumbuki kuwa kule wanatakiwa watu wanaohukumiwa kwa sababu kuna wezi wengi? (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi kutoka Ilagala, Mwakizenga, Simbo, Kaseke na Nyamoli wanapata shida sana kwenda Mahakama ya Mahembe na ninashangaa kwa nini Mahakama hiyo kila siku inakarabatiwa na inapoteza pesa za Serikali! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na ishirini. (*Makofi*)

**MWENYEKIDI:** Ahsante Mheshimiwa Nkayamba, kwa kuunga mkono hoja hii kwa asilimia 120 na kwa kusema kwamba, anayemuonea kijicho Mheshimiwa Waziri Mkuu, atangulie mwenyewe kwanza. (*Kicheko*)

**MHE. ANNA MAULIDAH KOMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii nzuri na nzito iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 10 Juni, 2009, Mheshimiwa Rais wa Nchi, hii alilihutubia Taifa hili. Kilio kikubwa kilichokuwa kikitoka ndani ya moyo wake ni kuyumba kwa uchumi duniani. Bahati nzuri, siku si nydingi Waziri wetu wa Fedha na Uchumi naye alileta bajeti. Baada ya hapo, Mheshimiwa Waziri Mkuu naye ametuletea bajeti yake, akifuatiwa na Mawaziri wake. Kauli kubwa iliyomo ndani ya hotuba hizo zote ni kuyumba kwa uchumi ndani ya nchi yetu, tuache wenzetu kwa sababu wao wameendelea, wana njia ya kuweza kujikwamua kwa haraka zaidi.

Nilitegemea vichwa vya wasomi waliojaa ndani ya ukumbi huu, tutachangia ili tumwambie Mheshimiwa Rais, Waziri Mkuu wetu, Waziri wa Fedha na Mawaziri tunaowatuma kazi, nini wafanye ili tusije tukaangamia ndani ya nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kila anayesimama hapa kama hapigi vijembe anagomba, anafika mpaka kufanya Mawaziri wetu waonekane si lolote si chochote; hiki ni kitu ambacho nashindwa kukielewa! Niliongea ndani ya Bunge hili nikasema, sawa ushabiki wa vyama uwepo lakini wakati tunashabikia, tuwe tunaangalia nani waliotutuma hapa na wametutuma tufanye nini ili tuweze kuwapelekea kile wanachokihitaji kwetu. Sasa labda leo nitaona CHADEMA, CCM au CUF tunakwenda wapi wenyewe kwa wenyewe! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila Chama ambacho kinaitwa Chama cha Siasa, dhumuni lake ni kukamata madaraka ya nchi, kushika Serikali. Kwa hiyo, sababu dhumuni hilo lipo, kila Chama lazima kiwe na ilani yake, unapokama Serikali unaangalia

macho yako kwenye kisima kikuu cha fedha ili kutekeleza yaliyomo ndani ya ilani yako, wananchi wasije kukusuta. Hiyo ndiyo kazi muhimu ya Chama chochote cha Siasa. Tunaposimama hapa tunasema ilani, ilani, kama hatutatoa michango ya kutosha jinsi ya kupata hizo pesa, hutaweza kuitekeleza. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba uniruhusu leo nimwagize Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa Rais; naomba sana Waziri Mkuu mwambie Rais, kuna kilio kikubwa sana cha akina mama. Zamani ukishika mimba ilikuwa furaha, siku hizi ukishika mimba unakuwa na simanzi, hujui kama siku ya kupanda kitandani kumleta huyo kiumbe kama utateremka pale. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilio ni kikubwa, akina mama tunakufa kwa sababu wakati wa kujifungua *clinics* ziko mbali mpaka tunachorwa vikatuni na akina mtu kwao. Akina mama wajawazito tunatembea kilomita na kilomita hatufiki *clinic*; ni hatari lazima tuyaaangalie haya.

Hiki ni Kitabu cha Maendeleo, mwaka jana tumezungumzia vifo vyta akina mama na watoto wachanga, pamoja na watoto walio chini ya miaka mitano. Mwaka huu tunaendelea, hivi nchi hii tutakuwa tunaongea mpaka tutafika wapi? Lazima tuhakikishe tunatekeleza kwa kiwango gani. Tulizungumza hapa kwamba, hospitali ambayo wale wenzetu wa vijiji ndiyo kilio chao, hawana *clinics* karibu, wanatembea mwenendo mrefu. Wenzetu walioko mijini wanapofika kwenye hospitali, vifaa vyta kuzalia havipo, tukaambiya vinapatikana nasema hivi havipo. Sasa nani wa kuangalia kama vipo? Mtu wa kuangalia hayupo sijui mpaka wapi?

Serikali inatoa hivi vifaa, kama inatoa kwa sababu aliyezungumza ni Naibu Waziri, lazima nimwamini; sasa nani anaafuatalia kwamba vitu kweli vinatumika kwa wale ambao wamekekewa vitu hivyo ili viweze kuwaffaa? Leo unafika hospitali unaumwa uchungu, umekukamata sawa sawa, unaambiwa lete pesa kwanza tutafute pamba na *gloves*; ni hatari. Lazima tuangalie haya, wanaozaliwa na wanaozaa wanaangalia taifa la kesho, kama hatutaangalia leo; kwa kweli watu 100000 wanaozaa 578 wanakufa, hatari; mbona wenzetu wamefika mahali pazuri sana. Mimba inaanza kuangaliwa tangu mwezi mmoja mpaka inazaliwa, sisi tunashindwa nini na kwa nini huko nyuma tuliweza? Kwa nini hatukai kitako tukajiuliza? Hiki ni kilio na ni huzuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kuna vilio vingine vinavyotanda humu vyta ajali za magari; hatujakaa sawa watu wamekufa kwa ajali ya gari, hatujamaliza mwezi watu wamekufa kwa moto; hizi ajali kwa nini wanaohusika hawakai kwa udhati wa nafsi wakasema tuzitafutie ufumbuzi? Hakuna lisilowezekana katika dunia hii, nawaomba sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niongelee kuhusu madawa ya kulevyta. Katika Hotuba ya Waziri Mkuu, ukurasa wa 75 unazungumzia kuhusu madawa ya kulevyta. Madawa ya kulevyta ni hatari, yanababishi hata UKIMWI. Leo huzuni yangu kubwa niliyonayo ni kwamba, hawa wanaoshughulika na haya madawa ya kulevyta, wamepewa shilingi 1,210,762,000 lakini wenzetu wa TACAIDS wamepewa shilingi bilioni nne.

Chanzo cha hawa kuwa wengi ni kwa sababu wanaotumia madawa ya kulevy ya wanazidi kuongezeka badala ya kupungua. Sasa tuwaongezee hawa fungu ili waweze kufikia lengo. Ninafurahi ninaposikia wamechoma mashamba ya bangi, wenzetu wengine wanasema bangi ni mboga; je, tutakwenda nao vipi hawa?

Wakuu wa Mikoa na Wilaya na Wenye viti wa Vitongoji na Vijiji, wana ukaribu gani ili kuweza kujuu makundi yanayotumia madawa ya kulevy ya kama bangi? Sidhani kama shilingi bilioni moja hiyo itaweza kumaliza mashamba ya bangi yaliyomo ndani ya nchi hii, haitawezekana hata kidogo, lazima tufikirie kuwaongezee fungu hawa. Kama tumeweza kuweka shilingi bilioni nne kwenye TACAIDS, basi na hawa tuwaongezee angalau shilingi bilioni moja basi iwe bilioni mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mirungi, Serikali ya Kenya, wala sisiti kuizungumza, kwa sababu siwasemi vibaya; kwao mirungi ni kitu cha kawaida, leo Tanzania sisi mirungi ni pombe lakini kuna uhusiano wa kibiashara baina ya Tanzania, Kenya na Uganda, nchi ambazo zimeingia kwenye Umoja wa Afrika Mashariki; je, bidhaa zitakapoanza kutoka Kenya au zinavyoendelea kutoka Kenya kuingia Tanzania tuna uhakika gani na tumejiwekaje kupamba na mirungi isijae Mtaa wa Lumumba? Mirungi ni pombe na sisi tumejiga marufuku, basi ningewataka hawa ndugu zangu waniambie; wamejiwekaje katika kulinda mirungu isiingie katika nchi yetu kiholela?

Ndiyo pale pale ninaporudi kukwambia, lazima fungu liongezwe ili tuweze kupambana na mambo haya. Watoto wetu wanaangamia, afadhali wangekunyuwa gongo, kwa sababu bia zinapanda kila siku hawana uwezo, kuliko madawa ya kulevy. Wanajipiga sindano za ajabu, jamani tuwaongezee fungu hawa ili waweze kupambana na hali hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakwenda kwenye mazingira, nitaongea kila siku hapa kuhusu kukinga kabla maradhi hayajawa mengi, kwa sababu kama tutashindwa kukinga sidhani kama tutaweza kuponya. Nimesema hapa, tufanye utaratibu wa kuteremsha bei ili watu waweze kutumia mafuta ya taa na gesi, mkaa unachomwa sitaki masihara; ukitoka hapa mpaka ukifika Dar es Salaam, wenzetu hawana biashara nyingine sasa hivi kwa sababu ya hali mbaya ya maisha. Tukae tuwafikirie tutawasaidiaje ili wasiendelee kuangamiza mapori na tutawasaidiaje watumiaji wa mkaa ili wasiendelee kukata miti kabla nchi yetu haijawa jangwa. Tutawakataza tutasema msichome mkaa na sisi tunaokaa mijini tutatumia bei ya mafuta ya taa hatuiwezi, tunaambiwa hapa bei za mafuta hazipandi tena, lakini sasa hivi bei ya *petrol*, *diesel* na mafuta ya taa imepanda na inaendelea kupanda. Hatutaweza kumudu kupikia mafuta ya taa wala gesi.

Ndugu zangu hatuwezi kupata pesa kama hatujatumia pesa, lazima tukubali kutumia pesa ndiyo tutapata pesa. Sasa tunapokaa tukisema hatuna, itaingia kwa kupitia njia gani; lazima tuhakikishe tunapiga marufuku kabisa, tuwape kazi nyingine ndugu zetu wa vijijini wafanye ili waweze kujitosheleza na maisha yao na wa mijini tuwateremshie bei ya gesi na mafuta ya taa ili tuachane na kuchoma mikaa hali ni mbaya. Hebu jamani angalieni hali ilivyo, magunia yamejaa barabarani na wale hawana lingine la kufanya.

Siwalaumu, wanachoma mkaa ili waweze kupata mlo wao, lakini tunapokwenda hivi miti inakwisha. Nani anajua hili? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudi kwa Wapangaji wa *NHC*, Mbunge wangu wa Ilala alilizungumzia, lakini naona hakulizungumza vizuri. Mimi ni mdau wa kukodisha nyumba za *NHC*; miaka 35 au 37 iliyopita wakati Serikali imepita ili tuweze kuingia humo ilikuwa imedhamiria kwamba, Watanzania walio na hali ngumu, Wafanyakazi na Serikali na Masharika ya Umma, waweze kukaa karibu na maeneo yao ya kazi na kodi ilikuwa nafuu, watu waliweza kuimudu japokuwa shilingi inakwenda ikishuka miaka na miaka lakini sio hivyo.

*National Housing* walipokuja kuamua kupandisha kodi, walituletea *tape* wakatupima, wakasema wanapima zile nyumba ili kodi iende kwa vipimo ambavyo wamekuja navyo, wakatuongeza kodi kutokana na ukubwa na upana wa nyumba. Leo kodi imepanda mara tatu, maana ukilia mara mbili wengine wanakwambia kwangu imepanda mara tatu. Uampandishia Mtanzania yupi kodi hiyo; una hakika kwamba ataiweza? Mshahara wangu ni shilingi laki mbili au laki mbili na nusu, unaniambia nilipe kodi ya nyumba shilingi laki mbili nitaishije?

Kwa hiyo, ndugu zetu hawa wanaoshughulika na hizi makazi, wazungumze na watu wa *National Housing* ili waangalie mara mbili upandaji huu wa kodi; hatukatai, kwa sababu kila mmoja anaendelea na kila shirika linataka kukua, kwa hiyo, kupandisha kodi wameona wao ndiyo itakuwa na manufaa kwao. Tuelewe kwamba, kuna akina mama wajane humo ndani na watoto wao, hawana pa kwenda. Hawakujaliwa kujenga, kwa sababu kujenga ni kujaliwa wamo humo wanakaa. (*Makofi*)

Tunaomba sana, sheria iliyopita hapa imesema kwamba, Nyumba za *National Housing* zitauzwa; waambiwe kwamba wale amba ni wapangaji wamo mle ndani, wapewe *priority*. Kusema kwamba, wanamudu kununua au hawamudu, sidhani kama hilo litakwenda kwa sababu kama alivyosema Mbunge wangu wa Ilala kwamba, kuna hatari kubwa ndani ya Shirika la Nyumba. Naomba tuyaaangalie sana haya mashirika yetu, kuna siri kubwa humo ndani; tusipofanya hivyo tunakwenda pabaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia kwa kusema hivi; kufa ni kufa, ajali ni ajali, damu ni kumwagika ni kumwagika; nimesema kuhusu akina mama na kuhusu ajali zilivyojaa barabarani, lakini pia kuna makuzi ... (*Makofi*)

(*Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa naambiwa ni kengele ya pili.

**MHE. ANNA MAULIDAH KOMU:** Ni ya pili?

**MWENYEKITI:** Ndiyo.

**MHE. ANNA MAULIDAH KOMU:** Ahsante.

**MHE. ABBAS Z. MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, sisi hatukutarajia leo kusimama hapa kuzungumza, lakini kwa moyo wake wa ukarimu, baada ya kupata zile barua ambazo zilitoka mstari huu akatusikia, akatuelewa na akatupa nafasi. Mheshimiwa Waziri Mkuu, tunakushukuru sana wewe na Spika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitoe pongezi nyingi kwa hotuba nzuri ya Waziri Mkuu na Msaidizi wake, dada yetu na Naibu Waziri, kwa kazi nzuri. Nalipongeza Baraza lote la Mawaziri, kwa kazi nzuri. (*Makofi*)

Nawapongeza Wakuu wa Mikoa wote na Wakuu wa Wilaya, kwa sababu haya yote tunayoyasema hapa mazuri, yanatokana na usimamizi wao mzuri. Kwa hiyo, muono wangu, tunawapongeza sana. Wabunge tupo karibu 300 na zaidi, Mawaziri wako 26, kwa hiyo, ndugu zangu mnajua ni namna gani hatuwezi wote tukaangia kwenye tanuri lile. Tumpongeze pia Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuwachagua na kwa kufanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nianze na kumkumbusha Waziri wa Mambo ya Ndani, ingawa wakati wake haujafika; kulikuwa na suala la kifo cha Ndugu Minde na Ndugu Hija, kwa sababu mpaka leo jibu halijatoka, wakati ukifika nitaomba tupate jibu kwani wale wazee wanasubiri. Safari hii nitalisimamia kwa nguvu zote, hata ikitakiwa hoja binafsi itabidi niwasilishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze sana Serikali kwa kazi nzuri, miaka mitatu na miezi sita nilipochaguliwa pale Temeke, nilikuta shule ya sekondari moja tu ya Sandari, kata zangu 11, lakini leo nina shule 12 kwa kazi nzuri ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi.

Lipo tatizo la walimu, lakini nawaambia kila siku wananchi wangu kwamba, serikali inatupenda, imejenga Chuo Kikuu hapa Chang'ombe kwa ajili ya walimu, tufanye subira tutapata walimu. Liko tatizo la maabara, nimewaambia nalo lipo katika utaratibu linakuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kidogo tatizo la umeme Temeke. Temeke tunao umeme, lakini tatizo kuna wakati unaweza kuishi kwenye nyumba yako ukapata umeme kwa wiki mara nne au mara tatu tu na unakuwa hauna nguvu. Hilo si tatizo, nawaambia wananchi wangu wafanye subira mambo yatakuwa mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo tatizo ambalo ni lazima nilisemee; wananchi wale sasa wana matatizo makubwa sana, bili wanazoletewa ni kubwa mpaka imefika wakati sasa amechaguliwa mtu kwenda kufuatilia bili zile. Cha ajabu, mwananchi anadaiwa milioni tatu na umeme wenywewe hakupata kwa wakati, lakini yule mtu anataka kuza nyumba ya milioni 30. Huu ni uonevu wa hali ya juu, wananchi wangu wengine wamepata presha kwa ajili hiyo. Mimi mwenywewe nimekuwa sina amani, huwezi

ukataka kuiuza nyumba ya mtu ya milioni 40 au 50 kwa bili ya umeme ya shilingi milioni mbili au tatu; siyo sahihi.

Wananchi wa Temeke wote, tunaomba tufungiwe LUKU kama Ilala na Kindondoni. Tunajua utaratibu wa LUKU, ukitufungia tukinunua LUKU ya 20,000 unakata 5,000 mpaka deni linakwisha. Kwa hiyo, hili ni ombi rasmi la Wananchi wa Temeke ili waondokane na tatizo ambalo linawakabili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisahau jambo moja muhimu sana; kuipongeza Timu ya Temeke TMK, iliyoshiriki kwenye fainali na Timu ya Ilala, wakatufunga bao moja la shida na la ujanja ujanja. Nimesema kwa sababu Zungu jana alisema amesema Timu ya Ilala ililala Lamada, lakini walikuwa wanalala chumba watu wanne. Timu ya Temeke ililala Lemila Kurasini, hoteli nzuri ya kissasa ya ghorofa tatu, ambayo inatazama bahari, kila chumba mchezaji mmoja. Kwa hiyo, sijui Zungu alifulia naye? (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Temeke tulipata maafa makubwa sana ya mabomu, lakini wakati umepita. Nataka kuzungumza nini? Huu ni wakati wa serikali sasa kuangalia umuhimu wa Kambi za Jeshi zenyelaha kuwa mbali na miji. Bila kuangalia hilo, tunaweza kupata maafa mengine makubwa. Lingine, tuhakikishe wananchi wale wanapata fidia zao walizoa hidiwa mapema iwezekanavyo ili tukienda kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu, Chama cha Mapinduzi kiweze kushinda bila tabu yoyote na kule watu wengi ni wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze sana serikali kwa kuona umuhimu wa kilimo. Tukisimamia ipasavyo tutavuka na tutafanikiwa na lile suala la kupeleka chakula cha njaa kwenye maeneo ya mikoa ambayo imepata njaa litakwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijui tunaitazamaje Dar es Salaam? Wenzangu wamesema, takriban pale tuko watu milioni tano. Uchumi wa nchi hii 75% unatoka Dar es Salaam. Sisi ndiyo wanunuvi wa chakula hicho kwenye mpango kama huu mzuri, tulitaraja tungetenga fungu la kutosha, kuwawezesha wafanyabiashara wakubwa na wadogo wa Dar es Salaam nao waweze kuwa na njia rahisi ya kupata mikopo ya kuweza kufanya shughuli zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchumi wa Dar es Salaam umeyumba zaidi; watu wa Dar es Salaam walikuwa wanakula milo mitatu tena kwa mboga mbili mbili, sasa hivi wanakula mlo mmoja kwa shida. Wenzangu wamesema hapa mirabaha, wanapata asilimia zao, tuitazame na Dar es Salaam isiwe eneo la watu kuja tu kuchangisha michango ya harusi, michango ya mikoa yao, lakini tunaposema habari ya barabara umuhimu huo hamuujuji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri Mkuu kwa kuitembelea Stendi ya Temeke Mwisho. Baada ya kutoka pale, ikaamuliwa Stendi ya Tandika ihame yote ihamie Temeke Mwisho. Mimi niseme, hatukukubaliana hivyo na mimi nikiwa Mbunge wa Temeke, katika hilo la kuhamisha kabisa Stendi ya Tandika pale ilitakiwa tushauriane. Kuiiondoa Stendi Tandika ni madhara makubwa kwa Wananchi wa Temeke,

Yombo Vituka, Makangarawe na Sandari. Tuangalie uwezekano wa kuhakikisha Stendi ya Tandika inatumika na ya Temeke muhimu inatumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiwanda cha Serengeti Bia kinaingiza mapato mengi kwenye nchi hiil tunashukuru, lakini maji taka yake ni kero kwa Wananchi wa Temeke. Maji yale yananuka na yanaleta maradhi, sasa inawezekana wakawa wanaingiza pesa nyingi lakini watu wanaotibiwa wakawa wanatumia madawa kuliko zile pesa wanazoingiza katika serikali yetu. Kwa hiyo, naomba tuangalie, isije ikawa kama Kiwanda cha Nguo cha KTM cha Mbagala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Devis Corner - Yombo Vituka – Makangarawe, imetangazwa mwezi wa nne hadi leo hatujajua inajengwa lini na pale ndiyo kwenye mtaji wangu mimi na CCM. Naomba Waziri wa Miundombinu atakaposimama, awatangazie watu wa Yombo Vituka na Makangarawe, barabara ile itaanza kujengwa lini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasikia kuna chombo kinataka kuanzishwa Dar es Salaam kuwa juu ya Madiwani na Wabunge. Tunaomba mtupe heshima yetu Dar es Salaam, msituletee vyombo vya kuja kuongeza gharama badala ya kuzipeleka kwenye Halmashauri zetu zikajenga mji. Kwa hiyo, mtakapokileta mkilete kwa utaratibu mzuri, sisi wa Dar es Salaam ni wanyonge lakini tunajua kusema kweli. Nami nataka kusema kwamba, katika hili tutasema mpaka mwisho, msituletee vyombo vya ajabu ajabu; Dar es Salaam kuna Wabunge na Madiwani, tupeni heshima yetu. Mara kwa mara mnapoanzisha mipango yetu muwasiliane na sisi, mara nyingine mnafanya mambo tu sisi tunapata lawana kwa wananchi. Dar es Salaam kuna shughuli kubwa pale, msione hivi jamani, wakati wa uchaguzi tunapata tabu, kila mtu atakwenda kwenye Jimbo lake mtatuachia sisi. Kwa hiyo, tunaomba chondechonde mnapounda vyombo tuwasiliane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliambiwa mabasi yaendayo kasi yataanza 2008, leo ni 2009 hayajaanza; SUMATRA wanazuia watu kusajili mabasi. Tunaomba muwaruhusu watu wasajili mabasi wasaidie usafiri. Chombo kile kitakapoanza, yale mabasi yatatafutiwa maeneo mengine yaende lakini tunaomba chondechonde mabasi yasajiliwe yachukue watu, kwani watu wetu wanapata tabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mradi pale Chang'ombe wa CIUP; kuna mtu amejenga kwenye barabara ya mradi wa 350, ana *building permit* na hati. Nakuomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, ufuatilie pale Manispaa ya Temeke, mtu ambaye katoa hati kwenye mradi wa barabara ya wananchi hastahili kuwa Temeke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwa mapenzi makubwa, nimalizie na TBC.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwape nguvu....

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mtemvu tunakushukuru sana.

**MHE. ABBAS Z. MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naunga mkono hoja kwa asilimia mia mbili kwa mia mbili. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mtemvu, kwa mchango wako. Kama nilivyosema mwanzo, Mheshimiwa Sanya atafuatiwa na Mheshimiwa Joyce Masunga, *Maziwa Fresh*.

**MHE. IBRAHIM MUHAMMAD SANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, baada ya muda mrefu kutokusikika katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, kwa heshima zote nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa tabia ya uvumilivu, uchapakazi, busara na hekima katika maamuzi yake. Ninaamini ataendeleza maamuzi hayo hadi kufikia uchaguzi mwakani na uwe uchaguzi huru na wa haki, kwa pande mbili zote za Muungano. (*Makofi*)

Sitamsahau Mheshimiwa Celima Kombani na hakuna asiyeelewa *capacity* yake katika Bunge hili, sifa za pekee zimwendee Mheshimiwa Kombani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwanri ye ye wala tusizungumze mengi, kwa sababu mafunzo mengi kayapata na vitabu vyake vingi ni vya Lenin na Carl Marx. Kwa hiyo, utendaji wake bado unaendelea ule ule wa Kikomunisti, ukitaka usitake utafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo kubwa sana kwa Viongozi wa Tanzania, baadhi yetu tumejenga na kuweka mbele ubinafsi kuliko maendeleo ya nchi yetu na ni sumu kubwa sana hiyo. Ukiona mnaanza kugawanyika ama kwa Chama Tawala au Vyama vya Upinzani, kwa upande wowote ule katika nchi mmekwisha kiuchumi na mmefilisika kisiasa. Tuachane na tabia hii, kwa sababu tumeletwa kwa kura za wananchi ili tusimamie maendeleo yao waondokane na dhiki walizokuwa nazo. Tukumbuke kuna Watanzania toka wanazaliwa mpaka wanakufa, hawajui kuvala kiatu na kama Mungu asingeujalia unyayo wa miguu kuishi, ungekuwa unamalizika, leo nusu ya Watanzania wangkuwa hawana miguu katika nchi hii. (*Makofi*)

Tuna tabia ya kusahau, kuna *psychiatrist* mmoja alitembelewa na mgonjwa, mgonjwa alipokwenda kumwona huyu daktari, daktari akamuuliza unaumwa na nini? Akamwambia nina maradhi ya kusahau. Dokta akamuuliza maradhi haya yameanza lihi? Mgonjwa akamuuliza Dokta maradhi gani? Ameshasahau! (*Kicheko*)

Sasa na sisi tunasahau kwamba, tunafika hapa kwa ajili ya kuwatetea na kuwaletea maendeleo Watanzania wenzetu ambao hali zao ni mbaya kabisa. Nitakupa mfano mmoja mzuri sana wa nchi ya Ghana. Ghana katika miaka ya 70 mwanzoni, walipatwa na tatizo kubwa sana la utapiamlo mpaka maradhi ya kwashakoo yakajulikana kama ni *Ghanaian Disease*, lakini viongozi wake wakasimama imara hasa General Jerry Lawrence alipoingia madarakani akaleta Green Revolution na akaibadilisha Ghana.

Yeye mwenyewe alikuwa anashiriki kwenda vijijini, kuwahimiza, kuwasimamia na kufanya kazi na wananchi wake hata kwa kupanda mihogo, viazi, mahindi ili kuwaonesha namna gani wanaweze wakajikomboa kiuchumi.

Mimi sikatai package hii ya 700 millions, lakini katika 80% ya Watanzania, ambao wengi wao tunasema ndiyo wakulima, ni wangapi kati ya hao watafaidika na hizi milioni 700? Tusiwe mahodari wa kupamba vitabu hivi, lazima utekelezaji na ufuatiliaji uwepo. Baada ya kumaliza Bunge siyo wakati tena wa kupongezana ni wakati wa kupeana pole, kwa sababu majukumu tuliyoyabeba ni mazito ili kumkombo Mtanzania katika dimbwi la umaskini. (*Makofi*)

Tujue hizi bilioni 700 zinakwenda kwa Watanzania wangapi? Watapata nguvu gani? Siyo suala la mathekta tu, suala zima la ukulima litasimamiwa vipi? Fedha hizi zisije zikamalizika katika mikono ya wajanja wachache na mtupe *assessment* hasa Serikali imetoa *700 billions in return*, tunategemea baada ya muda gani tutarejesha hizi fedha na faida itakayopatikana katika hicho kilimo ambacho tunakiita Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tuna machungwa yanaozeana, tunapiga kelele kila mwaka *small scale industries* zingewakomboa vijana wetu wangepata kazi. Tungetengeneza juice kwa ajili ya Watanzania na nyingine tukasafirisha, matokeo yake soko letu limetawaliwa na vitu vya Kenya, Dubai na Ulaya lakini sisi wenyewe tunayaacha machungwa Muheza yanaiza, tunaacha mananasi yanaharibika, tunapiga kelele na bei ya pamba.

Nawapa historia ya pamba nchini India wakati wa Mahatma Ghandi. Iangalie bendera ya kwanza ya India kabla ya hii iliyokuwepo, utaona ndani yake kuna alama ya *hand loom* ya kutengenezea nguo. Watu walipokuwa wakitembelea Mahatma Ghandi nyumbani kwake, walikuwa wanamkuta anatengeneza nyuzi na nguo anazovaa yeye mwenyewe ule winda wake na aliwahi kuwaambia kwamba kila familia, yaani kila kaya ya India, kama itakuwa na *hand loom* hakuna Mhindi ye yeyote atakayetembea bila nguo kwa pamba ya India. Waka-*advance*, leo India wanasa firisha nguo dunia nzima. Tusipige kelele kwamba, pamba haina thamani, tutengeneze vitambaa, tuchukue mfano wa nchi kama Mauritius, wanachukua vitambaaa wanatengeneza nguo na wana soko wanapeleka Spain, Portugal, Italy na uchumi wao ni mzuri. Wananchi wa kawaida, hawa Watanzania wenzetu, utakapowaelezea kwamba, Tanzania bajeti yake imetenga bilioni, trilion, sijui GDP; hawa elewi chochote, wanachoelewa wao waone soda bei imeshuka, asubuhi wanakunywa chai na watoto wao, wanawavalisha viatu watoto wao na wanawapa madaftari ili waende shule na hawashindwi kulipa karo, hapo ndiyo watajua kwamba wamekomboka kiuchumi.

Tulikuwa na Bodi za Mazao ya Vyakula Mchanganyiko kama NMC, CAPETS; ziko wapi? Haikuwa walimu leo walikuwa na wakaguzi katika mashule, hatuna wakaguzi katika mazao ya chakula.

Mimi nasema, tunapomaliza hili Bunge kama tulivyomaliza mwaka jana na mwaka juzi, tukitoka mlangoni pale tuna jukumu lingine jipya, hakuna tena

kupongezana; tukaze buti tutoke nje twende vijiji ni tukafanye kazi na wakulima ili tuwainue na tuinue kiwango cha maisha yao ya kila siku. Kwa upande wa kilimo nimemaliza.

Nakuja kwenye Jeshi la Polisi. Jeshi hili linafanya kazi nzito kabisa na wanastahili sifa za kila namna katika nchi hii. Wao ndiyo wanaolinda mabenki, minara ya simu ATMs, lakini vipato vyao ni vidogo sana. Uhamisho ni haki ya Askari kutoka sehemu moja ya Jamhuri ya Muungano kwenda sehemu ya pili, mkoa na mkoa au hata kituo kwa kituo, tunashindwa kuwapatia fedha zao za uhamisho na wanapata usumbufu mkubwa kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda Jeshi la Polisi liangaliwe kwa jicho la huruma, wengine wanakula risasi wanapoteza viuongo na kuna baadhi ya askari mpaka leo wana risasi katika miili yao, lakini inashindikana kuwapeleka hospitali zinazofaa nje ya nchi kuondolewa risasi hizo. Kwa nini tuwafanye hivyo? Idadi yao ni ndogo, *population* ni kubwa, wao ndio wanalinda vitega uchumi, wafanyabishara, mabenki na kadhalika. Polisi ndiyo wa kwanza kupelekwa lakini tumewatupa.

Jeshi letu lina wastaa fu wengine 146 waliopigana katika Vita vya Uganda wanalipwa shilingi 50,000 kwa mwezi, yaani shilingi milioni 7,460,000 kwa mwezi. Hivi tunashindwa kuwaongezea angalau wakapata shilingi 100,000? Ndiyo hawa waliokwenda mbele kuikomboa nchi ya Uganda, wakaonesha ushupavu wao na nidhamu yao, wakaleta ushindi kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, baada ya kumfukiza Nduli Idd Amini. Wengine hawana mikono na wengine hawana miguu; ni 146 tu. Mimi ningependa mwakani suala hili liangaliwe tena ili waongezewe pensheni zao. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni hawa Wachina walioivamia Tanzania; mlitegemea vijana wetu wafanye kazi gani kule Kariakoo? Leo mpaka Karanga wanaauza Wachina? Eti Watanzania tumefika mahali pa kujipamba na maua ya *plastic!* Waondoshwe, tunataka wawekezaji ambao watakuja na *capital, technology* na watatoa ajira; hatutaki watu wa namna hiyo kuja kuchukua nafasi za Wamachinga. Hii ni hatari kwa taifa, kwa sababu leo tukiwaachia wauze *plastics*, kesho watakuja kukwambia nimekaa Ilala miaka 20 nataka kugombea Ubunge; hapo kazi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kingine kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki. Tunachukua maziwa lita zaidi ya 200,000 kwa mwezi kutoka Kenya, lakini wanatuzuia kuuza Kenya lita 20,000, kwa misingi gani? Urari gani huu wa biashara uliokuwepo? Sasa tujenge misingi imara ya kuthamini vyetu, maziwa yalikuja juzi hapa ya Tanga Fresh na ya Musoma, tununue maziwa yetu; kwa nini tuagize Kenya? Tunatumia karibu shilingi bilioni tano kila mwaka, kuagiza maziwa kutoka nje ya nchi na tunaambiwa tuna ng'ombe milioni 19.8 katika nchi yetu ya Tanzania ambayo ni ya nne katika Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, pensheni iliyowekwa ya kupandishwa kiwango mpaka shilingi 52,000 na kitu bado ni ndogo. Haidhuru mwaka huu na itolewe

hiyo hiyo, lakini mwakani pensheni itolewe kwa kima cha chini cha mshahara. Unapompa mtu shilingi 50,000 ina maana umempa shilingi 1,600 kwa siku; jamani hetu tuijulize shilingi 1,600 ananunua nini? Ana chana moja ya ndizi; hana kuni, chumvi, binzari, samaki, dagaa, nyama, ana watoto watatu wanamongojea, hana matibabu, hana nguo, wala sabuni na bado hajasomesha mtoto.

Wanajeshi hawa wamelitumikia taifa hili, ningeomba kitu kimoja; katika hali kama hii ya kuinua uchumi wetu na kuokoa katika hii hali ambayo ni ya dharura tufanye kitu kimoja; tufanye *political and economic partnership* baina yenu CCM na sisi Wapinzani. Tuna mengi ya kuwaambia, tuna wataalamu huku hakuna ubaya, tunataka kuikomboa nchi kiuchumi. Utakapofika wakati wa uchaguzi, kila mmoja atajinadi kwa kitabu chake na ukweli wake utadhihirika na kuthibitishwa na Wananchi wa Tanzania, lakini sasa hivi lazima kuwe na *political and economy partnership* baina ya CCM na Upinzani, la sivyo Upinzani mnakuja huku na sisi tunakaa huko. Ndiyo! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka kunyanya ari za wanasiasa ili tuonekane wanasiasa bora, tutakaojenga nchi kwa misingi ya uchumi imara. Kila mmoja leo kaingia kiwewe sijui mmewekewa watu watatu jimboni hakuendeki; unaogopa nini? Kama hukurudi atakayerudi si ni Mtanzania mbona mimi sina wasiwasi na hilo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, huyo ni Mheshimiwa Muhammad Ibrahim Sanya, Mbunge wa Mji Mkongwe Zanzibar. Mheshimiwa Joyce Masunga, atafuatiwa na Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha.

Mheshimiwa Masunga, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Shinyanga.

**MHE. JOYCE M. MASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii, kwanza, kushukuru maana kama alivyosema Mheshimiwa Mtemvu, leo ilikuwa wengine tusizungumze. Nichukue nafasi hii, kuwashukuru sana kwa kutupa nafasi na sisi tupate kuzungumza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nichukue nafasi hii kumshukuru sana Waziri Mkuu, kwa hotuba yake; ni nzuri na nimeikubali. Mimi nina neno moja tu kwa Waziri Mkuu; Watanzania siku hizi inapofika Siku ya Alhamisi, kila mtu anafungua Bunge haraka sana, jinsi anavyojibu maswali ya papo kwa papo, Watanzania wote wanaamini kweli akili yako iko timamu. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusema ni kwamba, mnapomwona Waziri Mkuu ametulia, Mama Tunu, anafanya kazi. Kama Mama Tunu Pinda angekuwa hamsaidii, anambughudhi bughudhi kila siku, leo tungesema Waziri Mkuu hawezi kazi. Nachukua nafasi hii kumshukuru sana Mama Tunu Pinda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwashukuru sana Waziri wa TAMISEMI, Mama Kombani na Naibu wake, kama mtu anafanya kazi anaonekana; Wabunge wote hapa wa

Vyama vya Upinzani na sisi wa CCM, ukifika pale ukimwelezea tatizo, haraka analitatuwa na unaondoka kufanya kazi. Kwa kweli mama huyu na Naibu wake, wanastahili pongezi. Mimi nasema, Waziri Mkuu umepata wasaidizi wazuri sana katika ofisi yako. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nirudi nyumbani; kwa niaba ya Wanawake wa Mkoa wa Shinyanga, Wabunge wa Majimbo ya Mjini na Kahama wamesema, lakini kwa sababu Maji ni Mwanamke na Mwanamke ni Maji, lazima nizungumze. Mheshimiwa Vulu, kasema hapa, ooh! tunataka maji na sisi tuoge kwa kusimama. Nataka nimwambie, Shinyanga tunaoga maji kwa kusimama. Mheshimiwa Iddi Azan, sisi wenzako tunaoga maji kwa kusimama sasa. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii, kumshukuru sana Rais Mstaafu, Mheshimiwa Mkapa, ndiye aliyelianzisha hili; mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni. Nami nataka niseme Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, kaa, starehe kwa amani, kunywa *wine* na lala usingizi, Watu wa Shinyanga tunakushukuru sana kwa yote. Kwanza, tunakushukuru kwa maji, lakini mwisho tunakushukuru sana kwa barabara, nalo nitalisemea baadae. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, terehe 20, Wanawake wa Shinyanga, waliandamana kwa furaha kubwa kwa kusema kwamba, Ilani yetu ya Uchaguzi kwa Mkoa wa Shinyanga, imefanya kazi. Tulikuwa kila wakati tuna kipindupindu, Wabunge mliokuwa humu awamu iliyopita, Mbunge wetu alikuwa Mzee Derefa, kila akija hapa analalamika Shinyanga kipindupindu, lakini ilikuwa ni kwa sababu ya maji machafu.

Sasa wanawake wanafurahi, wametakata na wanamshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu, maana yake kuna mwingine unapewa kijiti na mwenzako lakini badala ya kukikimbiza unashindwa. Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wetu, amekikimbiza kijiti hicho, badala ya 2010 tumepeata maji 2009. (*Makofi*)

Mimi pia namshukuru, nasema kama Wanawake wa Shinyanga tutaachwa na wanaume zetu, tutaachwa kwa suala lingine, lakini si kwa ajili ya maji. Tulikuwa tunaamka asubuhi kuhangaika kutafuta maji; unaondoka saa tisa, unamwacha mwanaume kitandani unakwenda kutafuta maji, lakini sasa hivi tunalala tunaamka pamoja na tunaoga kwa kusimama. Sasa tunachosema, Wanashinyanga tuko wengi, kwa suala hili msije mkashangaa idadi ikaongezeka. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nianze kuzungumzia habari ya kilimo. Mimi nasema Kilimo Kwanza kinawezekana. Viongozi wetu ambaao ni Maafisa Ugani, sasa waache kukaa ofisini. Nataka nimwambie Waziri wa TAMISEMI, hayo makochi mazuri unayotaka kuweka katika ofisi ya kilimo usiweke; makochi ya nini? Waende shambani na nguo wabadilishe kama wanataka kuvalaa suti, suti hizo wawaachie CRDB Bank, wao wana nguo zao za kazi, waweke buti waende shambani wakawaelekeze watu jinsi gani ya kulima na kila afisa ugani awe na shamba lake la mfano. Sisi tunesoma, mbona tulikuwa tunaona mabwana shamba wako hivyo, leo kulikoni? Wengi wamesoma wako ofisini, maofisini kule wamejaa maafisa kilimo kibao, wanafanya nini? Waende mashambani tufanye kazi nao, watuelekeze. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Shinyanga, tunaomba suala la umwagiliaji mlitilie maanani, kwa sababu zifuatazo: Shinyanga hatuna mvua nyingi kama mikoa ile sita tuliyotangaziwa, hakuna sababu ya kupoteza muda, mnaifahamu. Shinyanga tuna mito mingi, mvua inaponyesha mito ile inajaa, kila Wilaya ina mito ya kutosha. Mjini pale tuna Mto Manonga, unajaa kweli kweli, tunachoomba hebu Serikali itusaidie kutuwekea mabwawa ili yale maji yasikauke bure tupate maji sasa tuanze kumwagilia. Tukipata kilimo cha umwagiliaji, tunasema ile mikoa sita, chakula kitakuwepo kwao na sisi Shinyanga tutakuwa na chetu na kitatutosha. Mimi ninasema kwamba, mvua ikinyesha vizuri tunapata mahindi, mtama na mpunga wa kutosha, kwa sababu sisi sio Mungu, tunaomba mambo ya umwagiliaji mtusaidie sana na nafikiri ndugu yangu Waziri wa Kilimo, hili analijua vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye Jeshi la Polisi. Mimi nataka niisemee Wilaya ya Bukombe. Wilaya ya Bukombe ni mpya na iko pembezoni. Asilimia 60 ni pori, lakini Wilaya hiyo haina kabisa gari la Polisi. Katika Ukurasa wa 81, mnazungumza kwamba, wananchi tuwe na ulinzi shirikishi wa jamii, tutafanya hiyo kazi. Hivi unavyokwenda kumwambia Polisi kwamba, sasa kuna jambazi mahali fulani, huyo Polisi anakwenda na nini? Tunaomba sana Bukombe isaidiwe, kuna pori kubwa wananchi wanaumia, lakini Polisi hawana jinsi ya kukimbia, hawana gari. Hebu tusaidieni basi, pelekeni magari ili mapolisi wetu waweze kufanya kazi vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende katika suala la JKT. Kati ya mambo yaliyonifurahisha ni kurudishwa kwa JKT. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wetu sasa hivi; na Wabunge wote hapa ni mashahidi, vijana si wakakamavu, nidhamu hakuna, migomo tele, lakini yote hii ni kwa sababu watu hawakupitia JKT.

Sasa baada ya kusema JKT irudi, mimi nasema yafuatayo: Leo namshukuru sana Kiongozi wa Maisha Plus kuja hapa, naomba JKT ifanane na Maisha Plus tuliyokuwa tunaona kwenye runinga. Vijana wa sasa hivi wako tofauti na sisi wa zamani, maana mkianza kusema waende pale, muanze kuwapikia maharage ya kuoza, hapo watu watakimbia. (*Kicheko*)

Vijana waende JKT, walime kwa matrhekta mnayosema Kilimo Kwanza, yale matrhekta yapelekeni kule ili vijana wakitoka huko wajue kuyatumia walime na wajue kwamba, mambo anayosema Rais wa nchi ndiyo haya. Mkianza kusema sasa muwapeleke kule, muanze tena mambo mengine, watasema kumbe JKT yenyewe ndiyo hiyo? Yale ya kwetu yaacheni, JKT ya sasa iwe ya kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina maswali ya kujiluza; zamani mlikuwa mnasema mtu asipokuwa na cheti cha JKT hapati kazi na hii ya sasa hivi ndiyo hivyo? La pili, watoto wanaokwenda huko lazima wawe wa aina zote kama tulivyokuwa tunakwenda sisi, watoto wa wakubwa na watoto wa maskini. Watoto wote waende huko, msije mkabagua yakawa tena mambo ya kulalamika.

Kama mwanamke, naomba nizungumzie habari ya unyanyasaji wa jinsia, kwa sababu na mimi nilikuwa JKT. JKT ya wakati ule, kama wewe afande anakufuata utapata mateso mpaka apate anachotaka yeye. Sasa hivi kuna Ukimwi, hatutaki. (*Makofi/Kicheko*)

**MBUNGE FULANI:** *Message imefika.*

**MHE. JOYCE M. MASUNGA:** *Message imefika.* Tunataka watoto wetu wanapokwenda kule, Jeshi lazima liangalie kuna Ukimwi, watoto wa kike waende kule wafanye kazi zinazotakiwa kufanywa sio tena mtu kuanza kumsukuma sukuma mtoto wa watu mpaka ufanye hivi, mpaka ufanye vile aah! hiyo hatutaki. Nasema kama Mbunge Mwanamke. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nataka nizungumzie barabara. Nimesema nampongeza sana Rais Mstaafu, Mheshimiwa Benjamin Wiliam Mkapa na baadae Rais wetu wa sasa, kwa kweli kazi inafanyika, barabara yetu ya Shinyanga ni nzuri, nafikiri na Mkuu wa Mkoa yuko pale anashuhudia kwamba, kweli barabara ni nzuri. Tunapofika hapa Manyoni, tunahangaika kama alivyosema Mheshimiwa Mlata, lakini ni nini tunachohangaika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba Waziri wetu wa Miundombinu na watu wote wa TANROADS, hebu waangalie, kuna hawa vibarua wanalamika na ndiyo maana wanaiba vitu mle kama *cement* na nini, kwa sababu hawalipwi inavyostahili. (*Makofi*)

Mimi nimepita Barabara ya Manyoni, wale vibarua wakanisimamisha nikiwa na Bendera inapepea. Wakaniambia wanalipwa malipo kidogo na wanasantini lakini fedha hazionekani kwenye karatasi wanayosantini. Walisema tunaonewa. Kamati nzima tulikwenda Kigoma tumeliona. Kwa hiyo, tunaomba viongozi waangalie wale wauja jasho hasa wenyewe wanaoumia, wanaopata vumbi, hela wanayopata ni stahili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba Mheshimiwa Mama Kombani, anisaidie yafuatayo wakati anajumuisha: Alikuja akatembelea Shinyanga Mjini, Manispaa, akaona madaraja mawili; Daraja la Mshikamano na la Ndala. Alisema kwamba atatusaidia. Sasa nataka atupe jibu ili Wananchi wa Shinyanga wajue; je, haya madaraja hela zimepatikana maana wanawake wanateseka? Madaraja haya ndiyo wanawake wanapopita wakiwa wajawazito kwenda Hospitali Kuu ya Mkoa. Pili, alituahidi barabara za mjini, ingawa zinajengwa lakini mwaka huu anasemaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja. Ahsante. (*Makofi*)

**MHE. MWADINI ABBAS JECHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi nami nichangie hoja iliyoko mbele yetu. Awali ya yote, napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu, ambaye ametupa uhai na uzima siku ya leo, kukutana katika jengo hili na kuweza kufanya kazi ambayo wananchi wametutuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nitoe shukurani zangu za dhati kabisa kwa Mheshimiwa Waziri Mkoo, Waziri wa Nchi katika Ofisi yake na Naibu Waziri, kwa kweli wanafanya kazi nzuri. Ukweli husemwa na sina budi kusema kwamba, wanajitahidi na kazi ambayo wananchi wanawapa kuifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri, ofisi hii takriban kuanzia Waziri Mkoo mwenyewe mpaka Naibu Waziri, ni marafiki zangu sana; na kwa sababu ya urafiki tulionao, sitopenda kuzungumzia yale mengi ambayo yamezungumzwa. Mazuri waliyoyafanya, nimeyaafiki na nimewapongeza na ninawaombea Mwenyezi Mungu, awape nguvu waendelee kuyatekeleza. Mtu anayekupenda, anakwambia lile ambalo lina upungufu ili upate fursa ya kulirekebisha hali iweze kunyooka na maendeleo yaweze kuzidi kile kiwango ambacho kimefikiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mengi yamezungumzwa na kadiri ambavyo utataka kuzungumza, utataga mle ambamo mwenzako wamezungumza. Kwa mantiki hiyo, nitajaribu kuzungumza kile ambacho kwa mbali sana Waheshimiwa Wabunge, hawakuwahi kukigusia ama wamekigusia kijuu juu.

Kwanza, ningependa kuipongeza hii Kampuni ya *Rubana Construction*. Mheshimiwa Spika, alitualika hapa tukahudhurie katika mafunzo ya teknolojia hii mpya ya ujenzi wa nyumba za gharama nafuu, tumejifunza mengi. Ninawashauri wenzangu kwamba, teknolojia hii tuipeleke katika majimbo yetu, itatusaidia kuweza kujenga nyumba za Walimu, Mahakimu, Madaktari na Watendaji na tukaweza kuondoa tatizo la nyumba kwa Watendaji wa Serikali, ambao wanafanya kazi katika majimbo yetu. (*Makofi*)

Nachukua nafasi hii pia kumlaumu sana Waziri Mkoo na Waziri wake wa TAMISEMI na Naibu wake. Wamekuwa wanafanya maoneshao yao hapo nje, labda wengine mmeyagundua; wanafanya maonesho ya ujenzi wa barabara ya kokoto kwa gharama nafuu. Wanaanza pale kwenye Round About ya Scandinavia mpaka kwenye Round About ya kwa Shabiby. Maonesho haya hawajatualika, tunataka na sisi tujifunze jinsi ile barabara inavyotengeza ya kutandika kokoto asubuhi, jioni wanapita akina mama na *broom* wanazikusanya, kesho asubuhi wakazitandika tena, akapita mwenye *blow* akatoa vumbi, keshokutwa wakakusanya tena wakatia kwenye magari wakaondoka nazo. Sasa utaalamu huu nadhani na sisi mngetufundisha, tukaweza kupata barabara nzuri huko vijijini. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepata bahati ya kuitembelea Tanzania sana na nimetembelea takriban mikoa yote isipokuwa mkoa mmoja ambao sijafika ni Mkoa wa Kigoma peke yake. Nimejionea mengi, nimejifunza mengi, ndio nikasema kwamba, Ofisi ya Waziri Mkoo na Watendaji wake, wamefanya kazi kubwa sana huko vijijini, ambayo ni ya kupigiwa mfano; isipokuwa kuna upungufu ambao ninataka kuuzungumzia ili nanyi mpate nafasi ya kuyarekebisha ili kuweza kuondoa matatizo ambayo yanaonekana kule vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna utofauti wa maendeleo baina ya Mkoa na Mkoa na hii inazungumzwa kila siku katika Bunge hili. Huwezi kuuangalia Mkoa wa Arusha ukaulinganisha na Mkoa wa Kigoma, baina ya Wilaya na Wilaya, huwezi ukaiangalia Mbeya Mjini, ukalinganisha na Mbeya Vijijini, baina ya Kata na Kata, huwezi kuiangalia Nakapanya na Nalasi kule Tunduru, kadhalika baina ya Kata na Kata, huwezi kuiangalia Pansiansi ukailinganisha na Kata ya Sangabuye. Hii ni mifano midogo tu, ambayo nimejifunza katika ziara zangu katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utofauti wa maendeleo baina ya Mikoa, Kata, Tarafa na Wilaya, unatokana na sababu nyingi, pengine ni jiografia, pengine ni fursa za uchumi zilizopo katika Kata, Tarafa au Wilaya ile, ujanja wa Watendaji wenyewe, kuwahi kwa wanaotendewa, lakini kuna kitu kinaitwa upendeleo katika utendaji kazi wa kutekeleza yale maamuzi ambayo Serikali inatakiwa kuyatekeleza. Naacha kwenye Mikoa, Wilaya na Tarafa, nakuja kwenye Kata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejifunza kitu kimoja kwamba; na hii mtanisamehe nitalisema kwa sababu ni ukweli; kuna baadhi ya Kata ambazo Madiwani wake wanatoka katika Vyama vya Upinzani na ushahidi ninao, wananyimwa maendeleo ya makusudi. Nitatoa mfano wa Kata moja tu ya Kigera iliyoko Musoma Mjini. Ndani ya miaka mitatu (2006/07, 2007/08 na 2008/09), Kata hii imepewa fedha za maendeleo shilingi milioni 17 tu. Hiyo ni *average* ya milioni 5.666 kwa mwaka mmoja, sasa niambie Kata ambayo inataka kuleta maendeleo; kujenga madarasa, kununua madawati, kujenga sijui zahanati na vitu kama hivyo, kwa ajili ya kuleta maendeleo ya wananchi, unampa milioni tano kwa mwaka, afanye nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukiangalkia Kata nyingine ambazo zinaongozwa na wenye kuongoza, miradi ni mingi kiasi ambacho inatia huruma. Hili ni tatizo ambalo nakuomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, uliangalie kwa undani sana, ndugu zetu Watendaji, Wakurugenzi, wanafanya upendeleo katika baadhi ya Kata, ambazo pengine zinaongozwa na Madiwani ambao ni wa Vyama vya Upinzani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo lingine hapa; unajua kule kuna Kamati, kama ambavyo sisi Wabunge tuna Kamati hapa. Kuna Kamati ambazo zinakutana miezi sita mara moja, kuna Kamati ambazo zinakutana miezi mitatu mara moja na kitu kama hicho, lakini pia kuna Kamati wanaiita Kamati ya Fedha, wengine Kamati ya Fedha na Maendeleo, wengine Kamati ya Fedha sijui na Mipango, kila pahali na jina lake. Sasa nimejifunza kwamba, takriban mahali pengi kabisa, hii Kamati ya Fedha wanaogopa, sijui wanaogopa au hawataki, kuwashirikisha Madiwani wa Vyama vya Upinzani? Kwa hiyo, hili ni tatizo. Hii ipo nimeiona Kata ya Kigera, niliiona Kata ya Kigumu Serengeti, lakini pia Sengerema walipigana mpaka hii juzi ndiyo kaingizwa Diwani mmoja kwenye hiyo Kamati. Hili si jambo zuri.

Inawezakana pia Sheria haijaaelekeza kufanya hivyo, lakini busara zinaweza kutumika. Mheshimiwa Waziri Mkuu, kabla hajawa Waziri Mkuu, alipokuwa Waziri wa TAMISEMI, aliwahi kutembelea baadhi ya hizi Halmashauri na nakumbuka aliwahi kupita pale Musoma Mjini, Madiwani wa Upinzani, wakamlalamikia kwamba, hawa

waungwana hawataki kutushirikisha katika Kamati ya Fedha. Waziri Mkuu, wakati huo alikuwa ni Waziri wa TAMISEMI akaagiza, jamani tumieni busara, hawa ndugu zetu Wapinzani waingizeni katika Kamati hii ili kusaidia kuleta maendeleo ya haraka.

Sasa wajifunze hapa Bungeni kwamba, Kamati hizi muhimu (*Watchdog Committees*), zina wapinzani, zinaongozwa na Wapinzani na kazi inakwenda vizuri. Kwa hiyo, nadhani ni funzo zuri Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Kombani, mjitahidi na hawa jamaa muwaelekeze kufanya hivyo, wasione vibaya tupo kusaidiana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania tunapaswa kuchangia maendeleo yetu na hii inakuja kutokana na kodi ambazo tunatoa ama michango ya kawaida ambayo tunachanga. Kodi zinatumika kitaifa, lakini pia kuna kodi na michango katika ngazi ya Vijiji na Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tabia ya baadhi ya Watendaji, ambao hukusanya michango kutoka kwa wananchi kwa ajili ya maendeleo. Nasema kuna baadhi ni wabadhirifu, wanakusanya michango lakini inatumika kimizengwe mizengwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu ulio mzuri ni baada ya mwisho wa siku, kuwaambia wananchi mmekusanya kiasi gani, mmetumia kiasi gani na mmetumia nini. Katika hili mnaondoa dhana mbaya, lakini pia linampa mtu hamu ya kuweza kuchangia zaidi maendeleo, kadhalika watu wanapata fursa ya kuipenda serikali yao kwa sababu inawafanya jambo ambalo wao wenye we wanajua wanafanyiwa. Mimi nadhani ipo haja kabisa ya kusisitiza kwamba, ni lazima Watendaji wawaeleze Wananchi kiasi cha michango wanayochanga na waeleze kiasi gani wametumia katika miradi ya maendeleo ili kuweza kujuu hatua wanayoipiga katika kuleta maendeleo ya sehemu zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ukurasa wa 55 unazungumzia suala la Ulinzi na Usalama. Sitaki kurudia kulizungumzia, kwa sababu muda wenye we umeshakuwa mchache, lakini ni kweli kwamba, ulinzi katika nchi hii ni muhimu. Watu wametumika kama hivyo tumezungumza, tumetumia Jeshi letu kukomboa baadhi ya nchi huko Kusini mwa Afrika, lakini pia tunafanya kazi nyingine kama Comoro na mahali kwingineko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuseme akimaliza Mwanajeshi huyu amestaafu, tunamuenzi vipi? Tusimsifie tu kwamba, kaikomboa Anjuan, tusimsifie tu kwamba kaikomboa Namibia, kaikomboa South Africa, sijui kaikomboa Msumbiji na Uganda, lakini mwisho wa siku ikawa anaadhirika mitaani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule jimboni kwangu katika Wilaya yangu ya Wete, kuna Wanajeshi wengi mno ambao hadi hii leo hawajalipwa viinua mgongo vyao. Wapo baadhi ya Wanajeshi walipokea mafao yao kwa mkupuo. Nakumbuka kuna siku hapa ilizungumzwa kwamba, baada ya kuonekana kwamba, wanaadhirika mitaani, basi wakatakiwa waorodheshwe upya wale watu ili waingizwe katika *Payroll* wawe wanasaidiwa Pensheni kwa ajili ya kuwaondolea ugumu wa maisha. Kule jimboni

kwangu, wapo wengi ambao hadi hii leo hawajaorodheshwa na bado wanapata ugumu wa maisha na kila siku wananiuliza ni lini tutaweza kuorodheshwa na sisi turudi katika *payroll* kuweza kujiondoa katika ugumu wa maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi na leo, Mheshimiwa Spika hapa alitutambulisha Wakurugenzi wa Maisha Plus na washiriki. Leo hii akatuonesha mshindi wa Maisha Plus. Mheshimiwa Spika mwenyewe alionesha kuvutiwa na ile shughuli, bila shaka na Wabunge tumevutiwa vile vile na tumejifunza mengi katika kipindi kile, tofauti na ile *Big Brother Africa* inavyotazamwa. Sasa mimi nilipata hamu moja kwamba, Wabunge hawashiriki kikamilifu kwenye Maisha Plus, tukajua nani mshindi wa Maisha Plus mionganoni mwa Wabunge?

Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninakuomba tuitizame hii, kama inawezekana Wabunge tufanye shindano hili la Maisha Plus, tujuue nani hasa ana uwezo wa kuishi kijijini. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzangu wamepata bahati wameshajengewa ofisi. Mheshimiwa Shoka, anadai samani, wakakae kwenye ofisi zao. Najua katika utaratibu huu kuna awamu, lililonishangaza mimi, siku moja nilipigiwa simu na Mkandarasi akaniambia bwana nimepewa kiwanja nikujengee ofisi yako, sasa unaona vipi? Nikamuuliza kiwanja hicho kiko wapi? Kiwanja hicho kimetafutwa kiwanja ...

(*Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha*)

**MHE. MWADINI ABBAS JECHA:** Aah! Ahsante Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jecha, hujaunga mkono hoja. Baada ya Mheshimiwa Jecha, atafuata Mheshimiwa Castor Ligallama na Mheshimiwa Sinani ajiandae.

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie katika Hotuba hii ya Waziri Mkuu. Awali ya yote, napenda niwashukuru Waziri Mkuu, Waziri wa Nchi (TAMISEMI) na Naibu wake na Katibu Mkuu. Kwa kuwa ni Hotuba ya Waziri Mkuu, nawashukuru pia Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Mkuu wa Wilaya ya Kilombero na Mkurugenzi wa Kilombero, kwa shughuli wanazofanya katika kuleta maendeleo ya Mkoa wetu na Wilaya yetu. (*Makof*)

Mimi nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwanza, kwa kupenda kilimo. La pili, nimpongeze kwa Wimbo alioimba wa *Power Tillers*, sasa waitikiaji ni wengi. Wananchi wamehamasika kweli, sijui tutafanyaje kama upatikanaji wa zana hizi utakatika?

La tatu, napenda nimpe salamu kutoka kwa Wananchi wa Kilombero, husasan Tarafa ya Mlimba na Mgeta. Wamesema nikupe salamu kwamba, ni vigumu sijui nitumie lugha gani kwa sababu kama Baba yako amekupa kazi, huwezi kumwambia kazi hii siitaki. Wanataka kusema kwamba, kazi uliyowapa ni ngumu, wale wananchi wako pua

na mdomo kutoka Kituo cha Umeme cha Kihansi, nifananishe umbali ni kama vile kutoka Inyonga mpaka Mpanda Ndogo. Inyonga kuwe na kituo Mradi wa Umeme uwe pale, vijiji vinavyoanza Mpanda Ndogo ndio hawana umeme. Umeme uliwashwa tarehe 24 Novemba, 1999 sasa ni mwaka wa kumi, wamenituma nikueleze kwamba, tuwaonee huruma, REA ianzie pale; wanalinda nguzo za umeme, wanalinda vyanzo nya maji, hamjawahi kusikia Kihansi imekauka, wametoka kule milimani wameteremka wanahifadhi mazingira maji yanapatikana siku zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu isitoshe kiutaalamu pale mahali pana kila kitu; pana *line* ya 33KV ndio inayopeleka umeme kilomita kama 15 katika Mji wa Mlimba. Wana *circuit breaker* yenye njia tatu, ile *line* ya Mlimba inatumia moja; mbili ni *spare*. Wana *transformer* yenye uwezo wa megavolt ampere (MVA) kumi, lakini Mji wa Mlimba unatumia 0.75 ya megawatt, kwa hiyo, unakuta *transformer* ile iko *dormant*. Kwa hiyo, hawa wanakijiji wa pande zote; njia ya Mlimba, njia ya kwenda Ifakara, wangeweza kupata umeme kwa kujenga *line* ya 33KV na kudondosha *transformer* kila kijiji wakapata umeme kwa gharama nafuu. Hivi vifaa vyote viko kwenye *switch yard* katika mgodi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgodi ule unazalisha *megawatt* 180, una mashine tatu, kila mashine inatoa *megawatt* 60. Sijui kama Mheshimiwa Waziri Mkuu, unafahamu kwamba ule mgodi una *phase* mbili? Tumeongelea sana habari ya DOWANS lakini pale pana *Phase II* ingetupa *megawatt* 120. Wale waliotengeneza mgodi ule walishaanza *Phase* ya Pili na ukienda kwenye mgodi unakuta kabisa kwamba, hapa ndio tulitegemea *Phase* ya Pili ianze, ambayo tunapata *megawatt* 120. Kama tungejikita kwa miezi mitatu, minne au mitano, tukatafuta fedha pale tungezalisha tena *megawatt* 120 na 180 tungepata *megawatt* 300. Hali ya mazingira ya Kihansi sio ya kuleta ukame hata mwaka mmoja, kwa miaka yote kumi bwawa lote lilikuwa linajaa kama kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye kilimo; Miradi ya ASDP ingetusaidia sana katika vijiji lakini utekelezaji wake ukilinganisha na lengo lile la kufikia shilingi trilioni 2.7 kwa mwendo huu tunaokwenda hatutafikia. Mwaka huu tumetenga shilingi bilioni 83.8 na ugani tumetenga shilingi milioni 841, lakini ukiangalia lengo la mpango mzima ni kutumia shilingi trilioni 2.7. Nimedadisi nikaona kwamba, ile Miradi ya TASAF, pamoa na PADEP imefanikiwa Wilayani, kwa sababu kulikuwa na utaratibu. Kwa hiyo, nafikiri ASDP tufanye mpango, tumuweke Mratibu Wilayani ili *a-coordinate* ASDP Makao Makuu na kule Wilayani, aweze kufanya kazi ambazo zitasaidia kuibua Miradi ya *DADPs*, kutengeneza mpango kazi, kuibua miradi itakayoanza katika vijiji. Hali kadhalika, pale ambapo kuna umuhimu wa umwagiliaji maji, kumtafuta mtaalamu huyu awe mtu wa umwagiliaji maji, itatusaidia sana kwenda haraka na mpango mzima huu wa ASDP. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, Wilaya yetu ya Kilombero ilitangazwa kama ni sehemu ya ardhiowevu. Hali ilivyo sasa sio nzuri, kwa taarifa niliyopata hivi karibuni, mazingira yameharibiwa sana. Tangu zoezi la kusitisha mifugo kuhama lisimamishwe, mifugo imeingia maradufu. Sasa tunazungumzia kilimo na huku tena bonde linaharibika. Bonde lile sisi wazaliwa wa kule tuna miiko yetu. Pembeni mwa mito kuna uoto fulani

tunauita mifufu, ilikuwa haiguswi, yale ni mazalia ya samaki. Leo hii mifufu hamna imeharibiwa yote, bei ya samaki katika Mji wa Ifakara inafika shilingi 15,000 kwa samaki mmoja. Baadhi ya samaki *species* zake zinaanza kupotea.

Ninaomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, kuitia kwako Mwenyekiti, twende tukalione Bonde lile na napendekeza Mawaziri wa Maliasili na Utalii, Waziri wa Nchi (TAMISEMI), Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), NEMC, uwape helikopta mpite juu mkaangalie hicho ninachokisema kama ushahidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaki kui-*pre-empty* Ripoti ambayo ameipata Mheshimiwa Waziri Mkuu, lakini wakati unasoma ile Ripoti ya Tume ulioiunda wakati huo, Waheshimiwa Mawaziri hao wangekwenda na helikopta wapite juu waangalie hali ya Bonde lile na baadaye kama itabidi, tuweke maamuzi magumu kuhusu Bonde lile. Kingo za mito zinaporomoka, ndicho kilichotokea Ihefu. Ihefu mito ile inatoka *Livingstone Mountains*, wakati mifugo ilipokuwa Ihefu, inawekwa Bwawa la Mtera, uliokuwa unakwenda Mtera ni mchanga, leo unakuta bwawa linajaa lakini kina kifupi. Kingo za mito zinabomolewa wakati ng'ombe wanakwenda kunywa. Sasa tukiachia hii na hii ni ardhoevu si kusema tu hili ni bonde la ardhoevu, watu hawawezi kulalamika wataelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine la utendaji; mimi siwezi kuwalaumu hawa Mawaziri jamani, anayekuja kwenye Wizara ni Waziri, lakini *machinery* ile imekaa pale miaka. Kama Waziri atakuwa hafanyi ile inayoitwa *Management By Walking Around* (MBWA), akakaa pale juu tu asijue kinachotokea chini, ndiyo maana mnakuta mnawenza kuwalaumu ndugu zetu hawa bure. Mimi nina mfano mmoja mdogo sana, pale kwetu katika Mji wa Ifakara, tuna redio yetu inaitwa Redio Pambazuko, vijana walijikusanya wakaanzisha Salamu Club, sasa wamefika wanachama 800. *Through* Salamu Club, wakaja tena na wazo lingine kwamba, tuanzishe *group* la mazingira linaitwa Boresha Mazingira Group, wamefanya kazi nzuri sana.

Ukienda Kituo cha Polisi wamepanda maua, ukienda Mahakamani wamepanda maua, ukienda *Round Abouts* zetu wamepanda maua na miti kwa kujitolea. Nilipofika mimi Mbunge wao nikasema, basi ni vizuri tukiandikishe hiki kikundi kiwe cha uchumi ili tuweze kupata mikopo. Kwa hiyo, tukaja nao Dar es Salaam kuanza mchakato wa kuandikisha. DC akawapa barua ya utambulisho kwenda Wizara ya Mambo ya Ndani, huu ulikuwa mwezi Februari; wamekwenda mwezi Aprili wamelipa, baada ya kulipa mpaka leo hii hawajapata kile cheti.

Kwa ruhusa yako Mwenyekiti, naomba nisome baadhi ya *message*, alizokuwa ananitumia Katibu wa Kikundi hicho. "Mheshimiwa Mbunge, kama Katibu Mkuu hayupo si kuna Msaidizi wake, maana nikirudi bila cheti wanachama hawatakuwa na fedha ya kuchanga tena kwa mara ya nane; hivyo sirudi mpaka nipate." Siku iliyofuata akaenda tena na ananitumia *message* tena; "Mheshimiwa pole na kikao. Wakati huu mimi niko huku sasa tena na uchovu wa safari ilikuwa tarehe 8 Juni, 2009, nashukuru nimeshinda salama kule Wizarani nimekwenda tena wameniambia niende Ijumaa, nami

sina fedha ya kujikimu mpaka Ijumaa. Mheshimiwa chonde naomba msaada wako najua umetusaidia sana, usichoke malipo yako utalipwa na Mungu.”

*Message* ya tatu; “Mheshimiwa habari za asubuhi, pole na majukumu. Mimi nipo natazama kipindi cha Bunge, naomba kama ikifika zamu ya Wizara ya Mambo ya Ndani, uzungumzie adha tunayoipata.” Wale maskini, non profit making organisation, NGO tunataka tuwainue. Ajira gani tunataka tuwape hawa vijana? Mimi nilitaka kuwa-organise wale baadaye tutafute shamba na *power-tiller* kiwe kikundi cha kiuchumi. Sasa uandikishaji linakuwa tatizo, tangu mwezi Aprili wamelipia fedha yao, fedha yao mmeichukua mpaka leo urasimu huu. Sio kwamba, tunapohangaika Waziri Masha na Waziri Kagasheki hawajui; inawezekana kwa *ku-practise Management By Walking Around*, wangeweza kujua *somewhere* kuna matatizo. Kwa hiyo, naomba Wizara inayohusika itufanyie haraka, sisi tunataka kufanya kazi. Tunaomba hiki cheti kama ni hapa Dodoma kupitia kwa mimi Mbunge wao au kwa wao kuwapigia simu, yule kijana ameacha simu ilibidi nimtafutie nauli arudi tena kwa wenzake, lakini wenzake walisikitika sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana naunga mkono hoja. (*Makofî*)

**MWENYEKITI:** Pole sana Mheshimiwa Ligallama na pole kwa vijana. Mheshimiwa Mohamed Sinani, Mbunge wa Mtwara Mjini, atafuatiwa na Mheshimiwa Maida Abdallah, Mbunge wa Viti Maalum.

**MHE. MOHAMED S. SINANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nilikwishakata tama, lakini Mungu ameniona. Kwanza kabisa, niipongeze Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba, imegusa maeneo mengi. Kwa niaba ya Wananchi wa Mtwara, ningependa kutoa shukrani nyingi sana, hasa pale ilipogusia vivuko. Kivuko cha Mtwara kwenda Msangamkuu na Kivuko cha Kilambo, vilikuwa vinahatarisha maisha ya watu, lakini Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kujali wananchi wake, imeamua kununua vivuko hivi viwili, tunasema ahsante sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine naomba kutoa shukrani zangu za dhati kabisa kwa Serikali, kwa jitihada zake za kuleta umeme Mkoani Mtwara. Nashukuru pia kwa jitihada zake za kuleta Hospitali ya Rufaa.

Tulikuwa tunapata tabu sana, hususan katika masuala ya mgonjwa kuja mpaka Dar es Salaam lakini sasa tumepata imani kwamba, hospitali itajengwa na wananchi watapata matibabu huko huko Mtwara. Kwa hiyo, kwa niaba ya Wananchi wa Mkoa Mtwara tunashukuru sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kikubwa ambacho leo kimenifanya nisimame hapa ni kwamba, nataka nilijulishe Bunge lako Tukufu kuwa, Mtwara sasa hivi kimiundombinu imekamilika. Tuna umeme wa kuaminika, tuna gesi ya kutosha, tuna barabara ya lami kutoka Dar es Salaam mpaka Mtwara, tuna uwanja wa ndege ambao ndege yoyote inaweza kutua, kwa maana hiyo, Mtwara iko tayari kuchangia Pato la Taifa

hili. Serikali imejipanga vipi kuwashawishi wawekezaji kuja Mtwara kutumia miundombinu hii iliyopo?

Serikali ilitumia fedha nyingi sana za walipa kodi, kuacha miundombinu hii bila kutumika kuzalisha mali naona ni hasara kubwa sana. Sasa hivi tutapiga kelele Dar es Salaam; Dar es Salaam sasa hivi naona imeelemewa, barabara zake ni nyembamba mno, kuna msongamano wa magari, kuna msongamano wa watu, bandarini kuna msongamano, imefikia kusema kwamba sasa wanafanya kazi saa 24 na unapomsikia mtu anafanya kazi saa 24 ndio amefikia mwisho, kwa sababu huwezi ukafanya saa 26. Kwa maana hiyo, kwa nini basi Bandari ya Mtwara isitumike kupunguza msongamano wa Bandari ya Dar es Salaam?

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wanapoteza muda mrefu barabarani kwa msongamano wa magari. Leo chukua mfano, Mkurugenzi Mkuu wa TANESCO kutoka Ubungo ameitwa Wizara ya Nishati na Madini, atachukua saa mbili au tatu mpaka kufika Wizarani. Je, watu wangapi ambao wanapoteza muda na ule muda una thamani kubwa sana, ungelitumika kufanya kazi nyingine za kuzalisha mali, lakini msongamano umekuwa mkubwa. Hivi sasa Mji wa Mtwara una *Special Economic Zone* hekta 2,700, kwa hiyo, hata ardhi si tatizo. Hakuna tatizo la ardhi, hakuna tatizo la umeme, hakuna tatizo la gesi, hakuna tatizo la uwanja wa ndege na bandari ipo. Mimi naweza kusema, katika Tanzania hakuna mkoaa ambao umekamilika kimiundombinu kama Mtwara. Sasa ni lini miundombinu hii itatumika kikamilifu? Vinginevyo, tutaishia barabara hii inayojengwa kwa gharama kubwa kuleta soda na bia na kurudisha chupa tupu za bia na soda na umeme labda tugandishe *ice cream* au kuangalia *Ze Comedy* na sio maana yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ili umeme huu utumike kikamilifu, naishauri Serikali iwe na mipango madhubuti sasa ya kuhakikisha kwamba, wanaambiwa au wanashawishiwa wale wawekezaji waje Mtwara kupunguza msongamano sio kila kitu Dar es Salaam. Juzi hapa kulikuwa na *Pilot Project* ya kuweka gesi katika gari nayo iko Dar es Salaam. Jengo la Wamachinga liko Dar es Salaam, lakini Wamachinga wanatoka Mtwara na Lindi. Kila kitu Dar es Salaam, jamani Dar es Salaam hii imechoka sasa iko taabani. Mahali penye jengo la vyumba sita linaporomoka, jengo la ghorofa 10 au 15, sehemu ambayo ilikuwa na nyumba ya vyumba sita. Barabara ni zile zile, *drainage system* ni ile ile, nilikuwa nasikia sijui kama kuna ukweli ndani yake kama wanataka kujenga *flyover* ukitoka *Airport* ukianzia Mandela kuna *flyover*, ukitoka *Airport* unapita juu, ukija Chang'ombe upite juu, ukija KAMATA upite juu, sasa magari haya yote yakija kwa wakati mmoja mjini si unaleta tatizo lingine tena? Tunasikia pia kuna mpango wa mabasi yanayokwenda kasi, yatakimbilia wapi tunaona barabara zote zimejaa magari na watu, kasi hiyo itapatikana wapi? Sijui, pengine utaalamu sasa hivi umeongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata Wanafunzi wa Chuo cha Usafirishaji walipokwenda Bandarini Dar es Salaam hawakuitaja Bandari ya Mtwara, sijui tatizo liko wapi? Sasa hivi Mtwara tunaweza kusema kama ni peponi, kwa sababu zamani mtu akiambiwa kwenda Mtwara anakataa na alikuwa na haki ya kukataa, lakini sasa akija Mtwara hatoki tena. Tunashukuru sana, tunamshukuru Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, aliyejitahidi kuhakikisha kwamba gesi hii inatumika kuzalisha umeme. Gesi hii

imegunduliwa miaka ya 1980, lakini ye ye akishirikiana na Mkuu wa Mkoa wa zamani, Mheshimiwa Shirima walijitahidi na Serikali ya Awamu ya Nne ikatilia mkazo kwamba, sasa hivi umeme upatikane. Tunawashukuru sana. Mheshimiwa Mkapa pia ndiye aliyejenga Daraja la Mkapa na akaona haitoshi akajenga daraja katika Mto Ruvuma, Daraja la Umoja, ambalo mwaka huu litakamilika. Viongozi bora hujenga madaraja kuunganisha watu na viongozi amba ni *fascists* hujenga kuta kutenganisha watu. Kwa hiyo, namshukuru sana Mheshimiwa Mkapa na ninamwombea kila la kheri na afya njema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nige katika Kilimo Kwanza, lakini kilimo bila utafiti naona hatutafika mbali. Ningependa kufahamu kuna mpango gani juu ya watafiti wa kilimo na mifugo amba walihidiwa kwamba, mishahara yao itarekebishwa na ifanane na Taasisi kama hizo kama TPRI na kadhalika. Hawa watafiti wanafanya kazi kubwa sana. Kuna Kituo cha Utafiti ambacho kipo Naliendele, Naliendele ni jimbo langu na mimi huwa natembelea sana pale. Wamefanya kazi ya kufufua Zao la Korosho na wamesaidia kwenda nchi nyingine, wamekwenda Ghana, Msumbiji na wamekwenda katika nchi mbalimbali kuwasaidia wenzetu. Kwa hiyo, Kituo cha Naliendele ni kituo cha maana sana kwetu sisi na majirani zetu. Cha kusikitisha, kutoka *junction Airport* kwenda Naliendele, barabara ile ya kilomita tano ilikuwa na lami, lami imeondolewa mpaka sasa hivi haijarudishiwa. Tunaomba Serikali ijenge barabara ile na irudishie lami ambayo iliondolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukija katika zao la ufuta, watafiti wetu wamefanya utafiti mzuri sana. Kuna ufuta mweupe amba unatoa mafuta kwa wingi na unatoa mazao kwa wingi; hhekta moja inatoa kilo elfu moja mpaka elfu moja na mia tano, ukilinganisha na ufuta huu amba tumeuzoea wa kilo mia tatu mpaka mia nne kwa hekta moja. Haya ni mapinduzi makubwa sana ya kilimo, kwa hiyo, ninashauri kwamba kuwe na asilimia moja ya *export levy*, kuhakikisha kwamba, mbegu zinazalishwa na kusambazwa kwa wakulima wote, nchi hii karibu nzima watu hulima ufuta. Asilimia 75 ya ufuta hivi sasa inalimwa katika Mikoa ya Kusini, kwa hiyo, inachukua nafasi ya korosho kama zao la biashara. Kwa hiyo ni zao la maana sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeshauri kwamba, Wizara ya Kilimo ifanye mpango, asilimia moja ya *levy* ambayo ilikuwa Naliendele katika kufanya utafiti wa Zao la Korosho, wahakikishe kwamba inapatikana. Naliendele ni mahali ambapo panatusaidia sana na ni mahali pa maana sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nige katika suala la uvuvi; wavuvi wetu wana tabu kubwa, wametii amri ya Serikali ya kuacha kutumia zana ambazo hazikubaliki au nyavu ambazo hazikubaliki. Tumeambiwa mara nyingi kwamba, wajiunge katika vikundi ili wapatiwe pesa za MANCEMP, nimehamasisha wapiga kura wangu na vikundi 41 vimeundwa, lakini mpaka leo pesa hawajapewa. Hawa ni watu amba wana watoto wanataka kuwasomesha, wana mambo mengine ambayo wanataka kuyafanya na mvuvi leo ukimwambia aende kufuga ng'ombe ni sawa na kumwambia Mmasai akafuge samaki. Mfano mwingine ni kwamba, nguruwe hunasa katika mtego wa baharini na tasi hunasa katika mtego wa nchi kavu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Mji wa Mtwara tunakula Ng'ombe mmoja tu au mmoja na nusu, tumezoea kula samaki, hatujazoea kula nyama na sasa samaki hawapatikani. Tunaungana na Serikali, kutii amri ya Serikali kuacha kuharibu mazingira ya bahari, lakini pamoja na haya, tunawasaidia vipi hawa wavuvi wetu, tuwasaidie basi kwa kupitia MANCEMP kwani wana pesa nyingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pesa hizi zipatikane, wapewe maboti na zana za kisasa za kuvulia samaki ili wakidhi mahitaji yao. Hawa wazee na vijana wanaathirika, kwani ilikuwa ni ajira kubwa sana, leo wanakwenda pwani wanakaa kwenye mchanga na kuiangalia bahari ambayo walizoea kusafiri wakienda kuchukua samaki na kurudi, lakini sasa hawawezi tena kwa sababu hawana zana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetumwa na wananchi niiambie serikali yao ambayo wanaipenda sana kwamba, wawafanyie jitihada za kuwasaidia, tunaomba sana wavuvi wasaidiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii. Kwanza, napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia uzima na kuweza kuchangia Bajeti ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa hotuba yake nzuri na kama tutaitekeleza, italeta matumaini makubwa na maendeleo kwa Watanzania wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia niwapongeze Waheshimiwa Mawaziri waliopo katika Wizara hii, Naibu Waziri, Makatibu Wakuu, pamoja na Watendaji na Watsalamu wote, walioshiriki kwa njia moja au nyingine katika kukamilisha taarifa hii nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii imelenga utekelezaji mzima wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2005. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa hotuba nzuri aliyoitoa Kilimani, Mjini Dodoma, tarehe 10 Juni, 2009. Mheshimiwa Rais, aliwafahamisha Wananchi wa Tanzania kuhusu hali ya msukosuko wa uchumi ambao umeikumba Dunia na nini kifanyike katika Tanzania hii katika kuleta maendeleo ili tusiathirike na hali hiyo ya msukosuko wa kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nichangie kuhusu Kilimo Kwanza, kama alivyoleza Waziri Mkuu katika hotuba yake. Kaulimbiu ya mwaka huu tunasema ni Kilimo Kwanza, katika miaka ya nyuma tulikuwa tunasema Kilimo ni Utu wa Mgongo wa Taifa letu; ni kweli lakini safari hii ili kukuza vizuri kilimo katika hatua kubwa ya kimaendeleo, tumeingia katika kaulimbiu ya Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo hili limechangiwa sana na Waheshimiwa Wabunge, lakini mimi naomba nichangie maeneo madogo tu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakumbuka katika nchi yetu tunao wakulima wakubwa; wa kati; na wadogo, lakini katika Hotuba ya Waziri Mkuu, pamoja na ile ya Fedha, imeainisha au imesema tutawaimarisha wakulima wetu kwa kuwapatia mikopo, nilitaka nifafanue kuhusu mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, je, tumeshawaelemisha wakulima au tutawaelimisha lini kuhusu hii mikopo? Tuwaelimishe taratibu za mikopo, tusiwaache wakulima kwa sababu kilimo kinakwenda kwa msimu, lazima wakulima wapate elimu mapema kukabiliana na mikopo hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalisema hilo kwa sababu sasa hivi wakulima tayari wameshasikia kwamba, zimetengwa shilingi bilioni mia saba kwa ajili ya mikopo, lakini wao hawaajelewa mikopo hii itakuwa na utaratibu gani. Kuna taratibu za mikopo, mabenki mara nyingi wanatumia vitambulisho vya uraia, labda hati miliki za maeneo au mashamba, lakini kuna wakulima ambao hawana hati miliki za mashamba, wao wanakodi mashamba wanatoka Mkoa mmoja na kwenda mwingine unaozalisha kilimo zaidi na kukodi mashamba; je, mkulima wa namna hiyo atasaidiwa vipi kupata mikopo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wadogo na wa kati, watapata mikopo hii; hivyo, lazima tuwaelimishe wakulima wetu kuhusu suala zima la mikopo ili utakapofika msimu wa kilimo wasihangaike na kuleta malalamiko makubwa nchini; kwani malengo tuliyoyakusudia hayatafikiwa. Wananchi watailalamikia Serikali na tunaelekea mwaka 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nilitaka kusema kwamba, mikopo hii lazima iwe endelevu katika kumwendesha mkulima, isiwe inasita kwa sababu wakulima wameshajenga tamaa na kupewa mikopo na kama mikopo ikisitishwa, huu uchumi ambao unayumba tutaweza kuathirika sana. Kwa hiyo, napenda kusisitiza serikali iangalie mikopo hii iwe endelevu na hizo fedha zikitoka kama zitakuwa kidogo basi ziongezwe tupunguze sehemu moja ili tuendeleze mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri zimepangiwa fedha nyingi kwa ajili ya kilimo na fedha hizo baadhi yake zitawalenga wataalamu wa kilimo. Wataalamu wa kilimo watawezesewa kwa kupewa vyombo vya usafiri, fedha kwa kulipwa mishahara na mengineyo. Lazima Serikali iwasimamie vizuri wataalamu hawa ili kukiendeleza kilimo. Mkulima pia aendelezwе kielimu ili afanikiwe katika kilimo. Kwa upande wa Zanzibar, napenda nimuulize Mheshimiwa Waziri Mkuu; katika kikao cha pamoja ambacho kilikaa kikawashirikisha Wachumi wa Tanzania Bara na Visiwani na kuangalia hali nzima ya mtikisiko wa uchumi ambao unaikumba dunia na nini kifanyike na kuangalia kuwa Kilimo Kwanza ndicho ambacho kitatuendeleza katika taifa hili; je, kwa upande wa

Zanzibar Wakulima wa Zanzibar waliwaangalia kuhusu mikopo hii kwa maana ipo?  
*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule Zanzibar tunayo Mifuko ya Maendeleo ya Jamii, tuna TASAF na Miradi ya PADED na hii imewaendeleza wakulima kwa kiwango kikubwa wakiwemo wanawake, wajane, yatima na miundombinu, imefikia hatua kubwa katika kuendeleza maeneo mbalimbali kule Zanzibar. Je, Serikali haioni umuhimu wa kuweka kipengele hiki ndani ya TASAF kuwasaidia mikopo kule Zanzibar? Naiomba Serikali ilifikirie kwa kina suala hili, kwa sababu sisi ni Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hatuna uwezo wa kwenda kukaa ndani ya Baraza la Wawakilishi, tukazungumza hoja hii, lazima tuzungumze Bungeni na wananchi katika Mikoa yetu tayari wameshasikia hili, tukifika watatupa maswali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kilimo cha umwagiliaji; Mheshimiwa Waziri Mkuu, amelifafanua sana suala hili na amesema kilimo cha umwagiliaji kina uzalishaji mara tatu zaidi kwa msimu mmoja. Amesema kuwa, katika mwaka 2008/2009, tulikuwa na ekari 27,000 na sasa hivi tumefikia 318,745. Je, Mheshimiwa Waziri Mkuu; si vyema suala hili sasa hivi la kilimo cha umwagiliaji likaimarishwa zaidi ili tukaweza kuzalisha zaidi hapa nchini? Naiomba Serikali ifikirie kwa kina jinsi ya kuziongeza ekari 318,745 zilizotajwa na kufikia 5,000 na zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uvezeshwaji wananchi kiuchumi; mwaka 2006 hapa Bungeni ilipotoka kauli ya kuwezesha wananchi kiuchumi, shilingi bilioni 1.0 kila Mkoa tulitoka kama Wabunge wa Jamhuri ya Muungano na kwenda katika Mikoa yetu kuwaelimisha wakulima na wanavikundi mbalimbali, kujiunga na SACCOS na kugharimia wataalamu kwa fedha zetu sisi wenyewe, kwenda kuwapa elimu ya ujasiriamali kule Pemba. Serikali ya Jamhuri ya Muungano, imetoe shilingi milioni 600 kwa ajili ya kuwawezesha kiuchumi wananchi walioko Zanzibar, lakini hadi hii leo katika Mkoa wa Kaskazini Pemba, hakuna mwananchi hata mmoja ambaye amepata mkopo wa aina hiyo. Wananchi wanatuuliza; mltuambia kwamba kuna mikopo na sasa hivi tumeshajunga na SACCOS mbona hakuna mikopo; je, hii si ndoto?

Kwa hiyo, hili niliwahi kumuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kazi akasema, fedha zikishaingia Zanzibar hatujui matumizi yake. Kwa hiyo, naiomba Serikali ifuatilie utekelezaji mzima wa fedha hizi kule Zanzibar, shilingi milioni 600 ambazo zimepelekwa kule na Serikali ya Jamhuri ya Muungano ili kuangalia ni namna gani Wananchi wa Zanzibar wamefaidika na fedha hizi. Umesema hapa utekelezaji katika baadhi ya mifuko umefikia shilingi bilioni 42.8. Huku tupo katika awamu ya tatu, lakini kule hata awamu ya kwanza haijafikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa Ilani katika Mkoa wa Kaskazini Pemba; Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeweza kukarabati Jengo la Ikulu ya Jamhuri ya Muungano iliyoko Wete kwa asilimia kubwa. Nimetumwa na Wananchi wa Mkoa wa Kaskazini Pemba, kuja kutoa shukrani kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano, kwa ukarabati mkubwa uliofanyika katika Ikulu ile. Kwa kweli hatua iliyofikiwa ni kubwa na sasa hivi wanamalizia sehemu ya uzio. Tunaishukuru sana Serikali ya Jamhuri

ya Muungano, kwa kuweza kutukarabatia Jengo lile, kwa sababu lilikuwa katika hali mbaya sana na Wananchi wa Mkoa wa Kaskazini Pemba, wageni wao walipofika hawakujua wawaweke wapi. Hivi sasa tunawakabirisha viongozi mbalimbali kuja kutembelea Mkoa wa Kaskazini Pemba na kufikia katika Ikulu ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa Ilani umefanikiwa katika kujenga majengo ya Askari Polisi pale Limbani Wete. Majengo haya yamefikia katika kiwango cha mwisho wanamalizia. Tunaishukuru sana Serikali ya Jamhuri ya Muungano na NSSF kwa kuingia ubia na serikali na kuweza kutuwekea majengo haya ya Polisi katika Mkoa wa Kaskazini Pemba. Tunaiomba Serikali ifikirie kuyakarabati majengo mengine yaliyopo Police Line Wete, Matangatuani na Konde kwa sababu yapo katika hali mbaya sana na askari waliyopo Kaskazini Pemba hawatoshi kukaa katika majengo hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, serikali pia iangalie uwezekano wa kuongeza viwango vya mishahara kwa Askari Polisi, kwa sababu bado wapo katika viwango vya chini sana ukilinganisha na kazi wanazozifanya. Serikali iwaangalie na kuwapandishia mishahara pia kuwapatia fedha za uhamisho, askari ambao wamepewa uhamisho na wamechukua muda mrefu bila kupewa fedha zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali iangalie uwezekano wa kuanzisha Sheria Maalum ya Kulitambua Jeshi letu la Mgambo, kwa sababu askari hao wanafanya kazi ngumu na wanafanya kazi kama Jeshi. Askari hawa wapo katika hali ngumu sana, kwa sababu hadi leo hii wanafanya kazi kwa kujitolea. Kwa hiyo, naiomba Serikali tuanzishe Sheria inayohusu Jeshi la Mgambo kuwa na Sheria inayowapasa kuajiriwa au kutambulika Kisheria nchini.

Imefikia hatua Askari Mgambo baada ya kuja ajira za Jeshini, anatakiwa aende tena JKU ili apate cheti ndiyo aajiriwe. Tutakapopitisha Sheria hii hapa, basi ajira zitakwenda moja kwa moja katika Jeshi la Mgambo kwani sasa hivi kumekuwa na kikwazo kikubwa kwa Askari wa Jeshi la Mgambo kupata ajira mpaka wapitie tena JKU ambayo huku mnaita JKT na tukiangalia wanayo mafunzo kamili ya Jeshi. Naiomba serikali iangalie namna ya kuliangalia suala hili kwa kuwa serikali ni sikivu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mradi wa Umeme toka Pangani, Tanga hadi Pemba, naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri Mkuu hatua hii imefikia wapi? Wananchi wa Pemba, wanasubiri kwa hamu suala hili, bila shaka atakapofanya majumuisho atalizungumzia suala hili.

Wananchi wa Pemba wanayo shida kubwa ya umeme. Umeme ni wa jenereta, lakini wa kutoka Pangani, Tanga hadi Pemba utawanufaisha sana Wananchi wa Pemba. Tunaishukuru sana serikali kwa kutupatia Mradi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumzie suala la UKIMWI; mara nyingi serikali huwa inatenga fedha nyingi zikiwemo zile za ndani na nje kwa ajili ya maambuki ya UKIMWI. Suala hili huwa halifikiwi kama tulivyotarajia, kuna malalamiko makubwa kwa waathirika wa UKIMWI wamepata dawa lakini chakula hawana hasa wale walioko

vijijini na dawa zina nguvu sana. Kwa hiyo, serikali iangalie fedha hizi kuzipeleka kwa waathirika moja kwa moja kwa ajili ya kupata chakula. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, aliyemaliza kuzungumza hivi sasa ni Mheshimiwa Maida Abdallah, Mbunge wa Kaskazini Pemba.

Waheshimiwa Wabunge, dakika zilizobaki ni chache sana, hazimtoshi Mheshimiwa Charles Keenja kuweza kuchangia; itategemea maandalizi yatakayokuwepo mezani, kwa sababu ratiba ya kesho ni ngumu kidogo kama muda utaruhusu Mheshimiwa Keenja na Mheshimiwa Mama Anna Abdallah wanaweza kupata nafasi ya kuzungumza kesho. Kwa orodha hii, bado kuna Wabunge 26, ambao wangependa kuchangia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ambayo imependwa sana na Waheshimiwa Wabunge wameichangamkia kweli kweli, lakini kwa vyovyyote vile si rahisi hata kidogo, kwa sababu hawa 26 maana yake inahitajika siku nyingne nzima kwa uchangiaji peke yake. Kwa hiyo, utaratibu utakaoendelea kesho ni ule utakaoelekezwa na Mheshimiwa Spika na kumalizia hoja iliyopo mbele yetu kesho.

Mheshimiwa Spika, anawaomba Wakuu wa Mikoa wote na Ma-RAS wote, kwa maana ya kuwaalika katika sherehe iliyoandaliwa na Kampuni ya Zain. Kwa heshima ya Waheshimiwa Wabunge, kesho jioni kutakuwa na hafla kwenye Viwanja vya Bunge, ambayo itahusisha burudani ya muziki wa dansi ambapo mwanamuziki maarufu Mbiliabeli atakuwepo. Wanaombwa Wakuu wa Mikoa hawa wakiongozwa na Mkuu wa Mkoa mwenyeji, Mheshimiwa Dr. Msekela, wasikose kufika kesho jioni.

Waheshimiwa Wabunge, shughuli zilizopangwa kwa kutwa nzima ya leo zimekamilika na muda wetu kama nilivyosema sasa umekwisha. Kwa hiyo, naomba kuahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

(*Saa 1.43 usiku Bunge lilahirishwa mpaka Siku ya Ijumaa,  
Tarehe 26 Juni, 2009 Saa Tatu Asubuhi*)